https://dspace.org/

# Usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu teule za Kenya

**Kurgat, Ezekiel**

**2019**
Jarida la Afrika mashariki la masomo ya Kiswahil
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/224
Kurgat, E., & Mwamzandi, I. (2019). Usemezano Katika Nyimbo za Amani: Athari za Muktadha wa Kijamii Katika Utunzi na Uimbaji wa Nyimbo za Mhubiri Joel Kimetto na Mwinjilisti Philip Rono. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 1(3), 118-128.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

# USEMEZANO KATIKA NYIMBO ZA AMANI MIONGONI MWA JAMII TATU TEULE ZA KENYA

**EZEKIEL KURGAT**

**Tasnifu Hii Imetolewa Ili Kutosheleza Baadhi Ya Mahitaji Ya Shahada Ya Uzamili Wa Sanaa Katika Kiswahili Katika Chuo Kikuu Cha Kabianga**

**CHUO KIKUU CHA KABIANGA**

**2019**

## Ikirari

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawasilishwa kwa ajili ya utahini katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi ________________ Tarehe _________________

**Ezekiel Kurgat**

**PGC/KIS/005/11**

**Idhinisho**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kabianga:-

Sahihi __________________ Tarehe __________________

**Profesa Issa, Mwamzandi**

Mkuu wa Kitivo cha Sanaa na Sayansi Jamii

Chuo Kikuu cha Kabianga

Sahihi: ____________________ Tarehe ___________________

**Dkt. Kisurulia, Emmanuel**

Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Kabianga

**HAKIMILIKI**

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya tasnifu hii inayoweza kuzalishwa tena, kuhifadhiwa katika mfumo wowote, kutafsiriwa kwa njia yoyote, kielektroniki, kimtambo, kunakili au vinginevyo, bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Kabianga.

© Ezekiel Kurgat, 2019

**TABARUKU**

Kwa mama Ziporah na marehemu John Kures,

mlinitunuku kwa nafasi ya kupata elimu japo kwa mapato kiduchu.

Kwa mke wangu Margaret,

mapenzi yako ya dhati, ustahamilivu na maombi kanipa moyo

wa kuendelea. Ulinipa mshawasha wa kusitawisha kisomo changu.

Kwa wanetu Roy, Ron, Joy na Rody,

imani yenu kwangu ilinipa matumaini na furaha hata nyakati za

changamoto anuwai zilizotukumba katika safari hii.

**SHUKURANI**

Mungu Mwenyezi kwa kunipa uhai, afya na kuniwezesha kuikamilisha kazi hii. Hakika Mungu ni mwaminifu na ana wingi wa rehema na neema. Nawashukuru wasimamizi wangu Profesa Issa Mwamzandi na Daktari Emmanuel Kisurulia kwa uelekezi wao mwanana uliofanikisha kazi hii. Pia namshukuru mkuu wa idara ya Isimu Fasihi na Mawasiliano Profesa Ogembo kwa himizo zake muhimu. Nauthamini ushauri kutoka kwa wana idara hususan Daktari Alexander Rotich aliyenichochea kujisajili katika uzamili. Namshukuru Daktari Salim Sawe kwa wosia wake mufti wakati wa kazi hii. Sitawasahau wahadhiri wangu Daktari Omari Ontieri, Daktari Mosol Kandagor na Daktari Samwel Obuchi kwa kuniandalia msingi madhubuti kwa ajili ya kazi hii.

Aidha ningependa kuwashukuru walimu wenzangu kutoka idara ya Lugha katika shule ya Kabianga; hususan Bwana Ben Omwoyo na Eric Haye kwa kunifaa wakati wa kukusanya nyimbo za Abagusii na Dholuo, na kuzitafsiri. Mungu atawafidia kwa huduma hii muhimu. Kwa wazamili wenzangu; Gideon Rotich, Esther Korir, Jane Machani, Anne Kenduiywa na Mercy Moraa, umoja wetu udumu milele.

Mwisho, nashukuru jamaa yangu hususan mke wangu Margaret kwa uvumilivu, mapenzi na msukumo wake usiotetereka. Kwa waumini wa kanisa letu la Kapchebwaber AGC, maombi yenu yaliniwezesha kuendelea hadi tamati. Mungu Mwenyezi awatendee kulingana na mapenzi yake kwenu. Ahsante sana.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza usemezano katika nyimbo za amani za jamii tatu za Kenya. Nyimbo zilizoshughulikiwa ni zile zilizoimbwa baada ya ghasia zilizoshuhudiwa nchini Kenya baada ya uchaguzi wa kitaifa uliofanywa mwaka wa 2007. Kazi hii ilichochewa na uharibifu mkubwa wa mali na vifo vya watu usioweza kumithilika hasa kwa vile nchi ya Kenya ilikuwa haijawahi kuipitia hali kama hiyo wakati mwingine. Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa kubainisha sifa za usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii za *Wakipsigis*, *Wakisii* na *Waluo*. Kwa kufanya hivyo, uchunguzi huu ulilenga kuchunguza athari za mazingira na muktadha wa kijamii katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za amani. Aidha, kazi hii ilidhamiria kufafanua dhana ya shani kama inavyojitokeza katika nyimbo za amani. Hali kadhalika, kazi hii ilibainisha nyimbo kama kauli ambazo hujibu na kutarajia majibu kuhusu amani. Utafiti huu ulishughulikia jumla ya nyimbo ishirini zenye maudhui ya kukuza amani na maridhiano kutoka jamii tatu za Kenya zilizoathirika katika ghasia zilizozuka baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa. Jamii zenyewe ni *Wakipsigis*, *Wakisii* na *Waluo*. Utafiti huu uliendelezwa katika Kaunti za Kericho, Bomet, Nyamira na Nyando na ulishirikisha nyimbo zilizoimbwa baina ya mwaka wa 2008 na 2013. Nyimbo tano kutoka kila jamii husika ziliteuliwa kimakusudi na kisha kuhakikiwa. Nyimbo nyingine tano zilizoimbwa kwa lugha ya Kiswahili kutoka jamii tatu teule katika uchunguzi huu zilishughulikiwa pia katika kazi hii. Nyimbo za wanamuziki kutoka jamii zilizohusishwa zilikusanywa na kuhakikiwa. Kwa hivyo, data za kimsingi zilitokana na nyimbo zilizorekodiwa kwenye sidii. Aidha, uchunguzi maktabani uliendelezwa kwa kurejelea kazi mbalimbali za awali zilizowahi kushughulikiwa kuhusu nyimbo. Habari nyingine zilikusanywa katika mtandao. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya usemezano iliyoasisiwa na Mikhail Bakhtin. Uchanganuzi wa kimaelezo ulitumiwa katika kuchanganua data. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa nyimbo huwa na uwezo mkubwa wa kuielekeza jamii kwa njia mbalimbali. Kwa sababu hii, jamii hupokea ushauri na maelekezo juu ya umuhimu wa kukuza utangamano, amani na maridhiano kupitia nyimbo. Aidha, nyimbo huweza kutumiwa kama njia mojawapo ya kuiponya jamii pindi inapokumbwa na hali tata iletwayo na michafuko.

## ABSTRACT

This study investigated dialogic properties in songs that bear peace building messages and have been produced after the 2007/2008 national elections in Kenya whose outcome sparked skirmishes country wide. This study was prompted by the immense destruction of life and

property visited on Kenya as a country that had hitherto thrived in harmony. The general objective of the study was to potray dialogism in peace songs within the communities involved in the study. By so doing, this study shows how the peace songs were a reflection of what transpired within the communities during the skirmishes in the study. Secondly, this work looked at the element of novelty in peace songs from the communities involved in the study. Last but not least, the study looked at peace songs' addressibility and answerability. The study analyzed twenty songs that bear peace themes. These songs were drawn from three neighbouring communities that got involved in the post-election clashes occasioned by the announcement of the contested presidential results. The communities were the *Kipsigis*, *Kisii* and *Luo*. Five songs were collected from each of the three communities in question for analysis. A further five songs done in Kiswahili by musicians from the communities in the study were also collected for analysis. The study was guided by dialogism theory which was founded by Mikhail Bakhtin and expounded by other scholars. It was from this context that dialogism and reconciliation in peace songs were analyzed amongst the three Kenyan communities i.e. *Kipsigis*, *Kisii* and *Luo* that suffered from clashes occasioned by the 2007/2008 national election in Kenya. The research was carried out in Kericho, Bomet, Nyando and Nyamira counties and covered the period between the year 2008 and 2013.The primary data was obtained from recorded compact discs of the relevant musicians from the aforementioned counties. The secondary data was obtained from previous research works in the relevant area from libraries and internet. The collected data was analyzed by use of descriptive method. The findings of this study will advise the society on the need to co-exist peacefully and to advice on incorporation of peace songs as a healing measure in times of skirmishes.

## VIFUPISHO NA AKRONIMU

**ANC** ______________________________________________ Africa National Congress

**HODI** ____________________________________Horn of Africa Development Initiative

**ICC** ______________________________________ International Criminal Court

**KBC** __________________________________ Kenya Broadcasting Corporation

**ODM** ___________________________________ Orange Democratic Movement

**ODM-K** ___________________________Orange Democratic Movement –Kenya

**PNU** ________________________________________ Party of National Unity

**PPS** _______________________________________ Presidential Press Service

**SPLA** _________________________________ Sudan People's Liberation Army

**TJRC** ________________________Truth, Justice and Reconcilliation Commission

**UKIMWI** __________________________________Ukosefu wa Kinga Mwilini

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Usemezano** Nadharia inayohusishwa na Mikhail Bakhtin ambaye anaitumia kuelezea uhusiano unaokuweko katika mawasiliano. Usemezano ni mtagusano unaohusu zaidi ya nafsi mbili, na mvutano katika mawasiliano.

**Kuhakiki** Uchambuzi wa kinadharia wa kazi za kifasihi. Dhana hii inarejelea uchunguzi wa kazi ya kifasihi unaofanywa kwa makini na kwa utaalamu.

**Matini** Istilahi hii ilitumiwa kurejelea kifungu cha maandishi au usemi wa lugha.

## YALIYOMO

**IKIRARI NA IDHINISHO ______________________________________ ii**

**HAKIMILIKI _______________________________________________iii**

**TABARUKU _________________________________________________iv**

**SHUKURANI ________________________________________________v**

**IKISIRI** **vi**

**ABSTRACT** **vii**

**VIFUPISHO NA AKRONIMU** **viii**

**MAELEZO YA ISTILAHI** **ix**

**SURA YA KWANZA** **1**

1.1 Kitangulizi 1

1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti 1

1.3 Suala la Utafiti 9

1.4 Malengo ya Utafiti 10

1.4.1 Lengo Kuu 10

1.4.2 Malengo Mahususi 10

1.5 Nadharia Tete 11

1.6 Sababu ya Kuchagua Mada 11

1.7 Umuhimu wa Mada ya Utafiti 12

1.8 Upeo na Mipaka 13

1.9 Kihitimisho 14

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI** **15**

2.1 Kitangulizi 15

2.2 Misingi ya Kinadharia 15

2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti 19

2.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Usemezano 25

2.5 Utambulishaji wa Pengo la Kitaaluma 30

2.6 Kihitimisho 30

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ______________________________ 31**

3.0 Utangulizi ________________________________________________31

3.1.1 Uchunguzi Nyanjani ______________________________________ 31

3.1.2 Utafiti Maktabani ________________________________________32

3.2 Sampuli _________________________________________________ 33

3.3 Vifaa vya Utafiti __________________________________________ 34

3.3.1 Runinga ________________________________________________34

3.3.2 Uchanganuzi wa Data _____________________________________ 34

3.3.3 Uwasilishaji ______________________________________________35

3.4 Kihitimisho _______________________________________________ 35

**SURA YA NNE: SIFA ZA USEMEZANO KATIKA NYIMBO ZA AMANI**

4.0 Kitangulizi _____________________________________________ 37

4.1 Jinsi Nyimbo za Amani Zinavyoathiriwa na Mazingira ____________37

4.2.0 Kuathiriana Katika Nyimbo za Amani ________________________47

4.2.1 Athari za Sajili Katika Nyimbo za Amani ______________________47

4.2.1.1 Sajili ya Kidini ___________________________________________49

4.2.1.2 Sajili ya Vijana/ Mtaani _________________________________54

4.2.1.3 Sajili ya Kisiasa ________________________________________ _58

4.3.0 Tanzu za Fasihi Simulizi katika Nyimbo za Amani _____________63

4.3.1 Matumizi ya Methali_____________________________________64

4.3.2 Matumizi ya Sitiari ______________________________________66

4.3.3 Matumizi ya Mbinu za Sanaa _______________________________ 70

4.3.3.1 Mbinu ya Usambamba __________________________________70

4.3.3.2 Mbinu Rejeshi ____ 72

4.4 Dhana ya Shani katika Nyimbo za Amani ____ 73

4.5 Tamko Kuwa Jibu la Tamko Lingine ____ 78

4.6 Kihitimisho ____ 81

**SURA YA TANO: HITIMISHO ____ 82**

5.0 Kitangulizi ____ 82

5.1 Muhtasari wa Kazi ____ 82

5.2 Matokeo ya Utafiti ____ 83

5.3 Mapendekezo ____ 85

**MAREJELEO ____** 86

**KIAMBATISHO:NYIMBO____**90

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii ilinuiwa kuuwekea msingi utafiti huu ambao ulichunguza usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya. Vipengele muhimu kama vile suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada na upeo wa utafiti vilielezwa. Nadharia ya usemezano ambayo ilitumiwa kuuongoza utafiti huu ilifafanuliwa katika sura hii.

## 1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti

Nyimbo ni kipera cha ushairi simulizi katika fasihi simulizi. Ni utungo ambao una mpangilio maalumu wa maneno na una mahadhi. Nyimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi na huhusishwa na maneno kuhusu jambo fulani na pia sauti ya mwimbaji au waimbaji. Utunzi na uimbaji wa nyimbo huongozwa na kudhibitiwa na muktadha katika jamii husika. Kwa mfano, kuna nyimbo zinazoimbwa na wagema, wajenzi wa majahazi au mitumbwi, wavuvi, wakulima na wavunaji wakati wanapofanya kazi zao. Madhumuni ya nyimbo hizo ni kuwatia moyo katika kazi zao. Hali kadhalika, kuna nyimbo zinazoimbwa kwa burudani hasa wakati wa sherehe fulani, kama vile arusi. Nyimbo za arusi huimbiwa bwana na bibi arusi ili kuwapongeza kwa kufunga ndoa yao na kuwapa wawili hao mawaidha ya kutunza familia na watoto ili waishi pamoja. Pia, kuna nyimbo za kidini zinazoimbwa wakati wa ibada kama vile wakati wa kutoa kafara au tambiko. Nyimbo za kidini huimbwa kumsifu Mungu, kuomba au kutoa mafundisho ya kidini. Wakati wa kupasha tohara au jando, unyago na sherehe zingine za kiasili, nyiso huimbwa. Nyiso huimbwa na vijana wanapopashwa tohara. Nyimbo hizi huonyesha ushujaa, na huashiria kwamba anayetahiriwa amekua mtu mzima sasa.

Nyimbo zilianza tu mara binadamu alipopata lugha na kuweza kuzieleza na kuzifumbata hisia zake (Wamitila, 2003, Njogu na Maupeu, 2007). Mbarwa (1996) anaeleza kwamba uimbaji ni njia ya jadi iliyotumiwa na mwanadamu kwa ajili ya kufanikisha mawasiliano. Anaendelea kufafanua kuwa katika zama za kale, wazee walitumia mifupa kama ala za muziki wao kisha pembe za wanyama kuwa ala za kupuliza ili kuunda mahadhi. Kutokana na mpito wa wakati, ala hizi zimeimarika kutokana na maendeleo ya kisayansi na teknolojia duniani na kuwa za kielektroniki.

Nyimbo hutofautiana kulingana na maudhui, lugha na wahusika. Kufuatia vigezo hivi, Matei (2011) anatambua aina 11 za nyimbo, mathalani; hodiya, vita, nyiso, mbolezi, arusi, mapenzi, nyimbo za kuzaliwa na kupatiwa jina mtoto, dini, watoto, siasa na sifo.

Jamii hutumia nyimbo kutimizia majukumu mbalimbali. Kwa mujibu wa Matei (2011), nyimbo hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii iliyozibuni. Fauka ya hayo, nyimbo ni mbinu mojawapo ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii. Rekodi za matukio muhimu katika jamii huweza kuhifadhiwa kwa nyimbo na kupitishwa kwa vizazi. Isitoshe, nyimbo huakisi ujumi na umbuji wa tamaduni mbalimbali. Pamoja na hayo, nyimbo huwa ni njia nzuri ya kuburudisha, kuelimisha na kupitisha maarifa mbalimbali kwa wanajamii. Nyimbo hizi hufanya kazi sio katika kiwango cha msanii binafsi bali katika kiwango cha jamii nzima kwa nia ya kutumika kama kifaa cha kuendeleza jamii.

Nyimbo huwasilisha maudhui ya kila aina yakiwemo ya amani, chuki, mapenzi na hisia zozote zile alizonazo msanii. Nafasi ya nyimbo katika kuielekeza jamii hujipenyeza katika jamii nyingi duniani (Akombo, 2009). Kwa muktadha huu basi, nyimbo huathiri jamii kwa njia mbalimbali. Athari za nyimbo zinaweza kuwa chanya endapo zitatumika kuwaunganisha wanajamii na kuwahimiza watu kuchukua mwelekeo wa kiuadilifu katika tagusano zao za kila wakati mbali na kuwaburudisha. Kwa upande mwingine, nyimbo zinaweza kuwa chombo cha kukuza uhasama unaoweza kuitumbukiza jamii kwenye lindi la vita na maangamizi tele.

Finnegan (1976) anasema kwamba fasihi simulizi huchukua nafasi ya magazeti kwa wale wasioweza kusoma, na kwamba nyimbo huwasilisha masuala ibuka, shinikizo za kisiasa, propaganda na kuushauri umma kwa jumla. Hali hii huwezeshwa katika maeneo ya vijijini ambapo mwimbaji hutagusana na wanajamii katika shughuli za kawaida za kijamii. Wazo hili la Finnegan lilitufaa katika utafiti wetu kwani nyimbo za amani husemeza masuala anuwai kwa umma na kwa njia ya kasi sawa na vyombo vya kupeperushia habari kama vile redio, runinga na magazeti.

Masuala ya kisiasa hufafanuliwa kwa urahisi kupitia nyimbo ziimbwazo hadharani kama anavyosema Tracey, (1948) akinukuliwa na Finnegan. Serikali nyingi zimetumia nyimbo ili kuendeleza sera zao za vyama tawala pamoja na kukuza uzalendo miongoni mwa umma. Tracey anaendelea kusema kuwa nyimbo huwa wenzo unaotumiwa kuwasilisha mawazo yanayoonekana kukashifu viongozi wanaopotoka katika jamii. Katika hali hii, mwimbaji hutumia jukwaa la uimbaji kwa madhumuni ya kuathiri huku akiepuka hatari zinazoambatana na mkabala wa moja kwa moja.

Baadhi ya nyimbo huwasilisha maudhui ambayo kwayo huwa vigumu kuyataja au kuyazungumzia hadharani bila haya. Kutokana na hali hii, mwimbaji hushirikisha lugha ya kitamathali ili kusemeza maudhui aliyokusudia pasi na kuwaudhi wasikilizaji wake. Katika jamii nyingi za Kiafrika, masuala yanayohusu ngono huwa hayasemwi hadharani hivyo kulazimu utumiaji wa lugha ya kitamathali kwa kupitia nyimbo.

Nyakati za ukoloni nchini Kenya zilishuhudia kuimarika  kwa nyimbo zilizotungwa na kuimbwa kwa lengo la kukuza juhudi za kupigania ukombozi. Nyimbo na ngoma za kiasili zilitumika katika enzi za *mau mau* kuwahamasisha wenyeji kuhusu haja ya kujikomboa kutoka minyororo ya utumwa wa kikoloni. Kenya ilipopata uhuru, nyimbo zilizoimbwa zilichukua sura mpya kwani zilikuwa zikisherehekea utawala wa weusi huku zikizungumzia hali ya kisiasa nchini. Wanamuziki wengi wakati huo walitoka katika taasisi za serikali kama vile *AP Utawala Band*, *Kenya Police Band* na *Maroon Commandos.* Nyimbo hizo nchini Kenya zilichezwa kupitia idhaa ya taifa na hata vilabuni. Maudhui ya nyimbo pia yamekuwa yakidhibitiwa na hali halisi nchini. Kwa mfano, ghasia za kikabila zilipozuka nchini Kenya kutokana na tofauti za kisiasa baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007, nyimbo za kuhimiza amani na utangamano ziliweza kutungwa na kuimbwa na wanamuziki mbalimbali nchini. Nyimbo zilizohubiri amani zilianza kupata umaarufu na zikawa zinachezwa katika vituo vingi vya utangazaji. Aidha misafara ya amani iliweza kucheza nyimbo za amani ili kuwahamasisha wananchi kuhusu thamani ya kutagusana kwa njia ya amani katika jamii.

Ghasia zimekuwa zikikumba taifa la Kenya kila uchaguzi wa kitaifa unapofanywa. Hali hii ilishuhudiwa wakati mfumo wa demokrasia ya vyama vingi ulipofufuliwa mwaka wa 1991. Matukio ya ghasia yamekuwa yakijirudia kila  kunapoandaliwa uchaguzi. Miaka ya 1992, 1997 na 2002 ilishuhudia misukosuko iliyoambatana na uharibifu wa mali na vifo vingi. Taifa la Kenya  lilipitia hali ngumu katika historia yake wakati wa uchaguzi wa mwaka wa 2007 (Kutol na wenziwe, 2009). Uchaguzi huo ulikumbwa na misukosuko pindi tu matokeo ya urais

yalipotangazwa na Rais Kibaki kutangazwa kuwa mshindi. Tangazo hilo halikuwapendeza wananchi wengi waishio maeneo ya mkoa wa Bonde la Ufa na Nyanza ambao walikuwa wafuasi sugu wa chama cha *Orange Democratic Movement* (ODM) kilichokuwa chama pinzani. Hali hii ilizua misururu ya ghasia kote nchini iliyotishia kuisambaratisha nchi ya Kenya kwa kuielekeza kwenye vita vya ndani kwa ndani (Githinji na wenziwe, 2007).

Mataifa mengi ya Kiafrika yamepitia michafuko inayosababishwa na tofauti za kisiasa na mizozo ya uongozi. Kwa sababu hii, muungano wa nchi za Afrika (AU) wakati wote huwa mbioni kujaribu kuizuia au kuidhibiti michafuko hiyo inapotukia. Ibok (2000) ameonyesha namna ambavyo juhudi mbalimbali zimejaribiwa katika harakati za kuhakikisha kuwa amani imedumishwa katika bara la Afrika. Ghasia zimeshuhudiwa katika mataifa mengi barani Afrika yakiwemo Burundi, Angola, The Comoros, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Somalia, Sudan miongoni mwa mengine. Nchini Sudan kwa mfano, juhudi za kuleta maridhiano zaelekea kugonga mwamba kwa kuwa hakujatokea azma ya uungwaji mkono kutoka kwa viongozi wenyewe. Fauka ya hayo, ukosefu wa uwazi na uwajibikaji katika uongozi wa kisiasa umechangia katika kuendeleza ufisadi na ukabila nchini humo. Tatizo hili limekuza uhasama na kutoaminiana miongoni mwa makabila na matabaka tofauti katika jamii ambao huwa vigumu kuuondoa. Muungano wa Afrika (AU) umejaribu kuhusisha makundi ya majeshi na hata raia kutoka mataifa mengine ili yaendeleze mchakato wa kujenga amani na maridhiano ya kitaifa.

Katika nchi yetu ya Kenya, juhudi mbalimbali zilifanywa ili kudhibiti uwezekano wa utukiaji wa ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007. Sababu kuu hapa ilikuwa kwamba historia ya chaguzi kadhaa zilizokuwa zimeandaliwa awali zilionyesha kwamba urudiaji wa mkasa sawa na mikasa

iliyopita ungezuka. Mashirika mbalimbali yasiyokuwa ya kiserikali na mashirika ya umma yalijizatiti kubuni njia za kukinga uzukaji wa michafuko kabla ya kutukia.

Nebe (2012) akishughulikia suala la udhibiti wa ghasia nchini Kenya, anazungumzia baadhi ya mikakati iliyoshirikishwa kama vile *"Chagua Amani Zuia Noma"* ambayo iliweza kuvutia uhusika wa mashirika ya umma, vyombo vya habari, sekta za kibinafsi na mashirika ya kidini. Mkakati huo uliolenga kukuza amani miongoni mwa makabila mbalimbali ulizinduliwa rasmi tarehe 21 Septemba 2007, miezi mitatu tu kabla ya uchaguzi mkuu wa kitaifa (Jacqueline, Githinji na Karuoya, 2007). Muungano huu ulilenga maeneo yaliyodhaniwa kuwa na uwezekano wa ghasia kuzuka kama vile mlima Elgon, Kuresoi na kwingineko. Kampeni ziliendeshwa kupitia nyimbo za amani na video katika vyombo vya habari. Hata hivyo, wananchi wachache hususan wa tabaka la juu ndio waliofikiwa. Idadi kubwa ya umma iliwategemea wanasiasa waliowafikia kupitia kampeni zao zilizojawa na chuki na uchochezi wa hisia za kikabila. Hisia hizo zilizokuwa zimechocheka zilihitaji uchokozi tu kidogo nazo zilipuke. Kuzuka kwa ghasia kali baada ya uchaguzi wa 2007 kulidhihirisha kwamba juhudi za kuzizuia ghasia hizo ziligonga mwamba.

Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano ya Kenya (TJRC) ilibuniwa mwaka wa 2008 kupitia sheria ya bunge la Kenya nambari 6 ya 2008. Kubuniwa huko kulishauriwa na kutiwa sahihi kutokana na makubaliano ya kitaifa hususan ajenda ya nne kulikosimamiwa na Kofi Annan na kushuhudiwa na Benjamin Mkapa na Graca Machel. Azma kuu ya tume hii ilikuwa kuchunguza kiini na athari za ukiukaji wa haki za kibinadamu na masuala mengine ya kihistoria yalengayo uhalifu dhidi ya Wakenya. Kupitia tume hii, iliaminiwa kuwa ufanisi wa kujenga umoja,

maridhiano na uponyaji wa kitaifa ungefikiwa. Masuala yaliyochunguzwa yalitukia baina ya tarehe 12 Disemba 1963 na 28 Februari 2008. Rais wa Jamuhuri ya Kenya Uhuru Kenyatta alikabidhiwa ripoti ya tume hii mnamo tarehe 13 Mei 2013.

Juhudi nyingine ya kusaka utatuzi wa kudumu wa ghasia za kisiasa ilihusu ubuniwaji wa tume ya Kriegler na Waki. Lengo la tume hiyo lilikuwa kutathmini shughuli zote za uchaguzi wa 2007 ili kubaini visababishi vya ghasia zilizofuatia uchaguzi huo. Mapendekezo ya tume hiyo yalinuiwa kukinga uwezekano wa kuzuka kwa ghasia tena katika uchaguzi wowote ule ujao nchini. Shughuli za tume ya Kriegler na Waki zilifikia tamati kirasmi mnamo mwezi wa Oktoba 2008. Mapendekezo yalitiwa ndani ya bahasha na kuwasilishwa kwa Kofi Annan ambaye alikuwa mwenyekiti wa washauri walioalikwa kuwapatanisha viongozi wa kisiasa waliokuwa wakizozania matokeo ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 nchini Kenya. Ilibainika kwamba bahasha hiyo ilibeba majina ya washukiwa waliosemekana walihusika moja kwa moja katika ufadhili pamoja na uchochezi wa ghasia zenyewe. Kofi Annan aliiwasilisha bahasha hiyo iliyokuwa imefungwa, kwa kiongozi wa mashtaka wa mahakama ya ICC kule Uholanzi ili mashtaka yafunguliwe kirasmi dhidi ya washukiwa hao. Hatimaye, kesi ilipoanza, washukiwa sita walitajwa na kesi ikaendeshwa. Miongoni mwa washukiwa walikuwemo Rais Uhuru Kenyatta, Naibu wa Rais William Ruto, Henry Kosgey, kiongozi wa wakati huo wa idara ya Polisi Hussein Ali, Francis Muthaura na mwandishi wa habari Joshua Sang'.

Juhudi mbadala za kusaka amani miongoni mwa wanajamii zimetumika katika maeneo mengine nchini Kenya. Kairu katika *Daily Nation* (10.8.2016) anarejelea shirika lisilo la kiserikali linalojulikana kama *Horn of Africa Development Initiative* (HODI). Shirika hili lililoasisiwa na

Fatuma Abdulkadir Aden mwaka wa 2003, linahusika katika ukuzaji wa uwiano wa kijamii kati ya jamii za Gabbra na Borana zinazoishi Marsabit. Jamii hizi zimehusika mara kwa mara katika vita vikali vilivyosababisha vifo vingi. Mnamo Julai mwaka wa 2005, mamia ya washambulizi kutoka jamii ya Borana walivamia jamii ya Gabbra katika eneo la Turbi, Kaskazini Magharibi mwa Marsabit na kusababisha vifo vya watu zaidi ya sitini. Kiini cha ghasia kati yao kimekuwa ung'ang'aniaji wa maji na nyasi kwa mifugo wao. Fatuma ameshirikisha vijana na wanawake katika shughuli anuwai za shirika hili. Mchezo wa kandanda umetumika kwa ufanifu mkuu ambapo hujengwa kwa kauli mbiu *"hamna damu itakayomwagwa; ni jasho tu"*. Vijana huambiwa, *"fyatua ufunge bao; siyo kuua"*. Shirika hili la HODI limeimarika na kufikia washiriki zaidi ya elfu kumi ambao huhubiri amani huku wakishughulikia utatuzi wa changamoto zinazozikumba jamii husika kama vile desturi zilizopitwa na wakati mathalani ukeketaji wa wasichana na ndoa za mapema.

### 1.3 Suala la Utafiti

Tahakiki nyingi za awali zinazohusu nyimbo zimeshughulikia masuala anuwai. Baadhi yazo zimeshughulikia mambo kama vile fani, maudhui na uamilifu wa nyimbo. Tafiti nyingine zimelenga simulizi za ugonjwa wa UKIMWI katika nyimbo. Aidha uchunguzi mwingine ulishughulikia usemezano katika nyimbo za taarab. Kadiri tujuavyo, hakuna mhakiki wa nyimbo za amani ambaye ametumia nadharia ya usemezano katika uhakiki wake. Kwa hivyo, utafiti wetu ulichunguza ikiwa usemezano unaweza kupatikana katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu teule za Kenya.

## 1.4 MALENGO YA UTAFITI

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuhakiki usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu teule za Kenya baina ya mwaka wa 2008 na 2013.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Ili kulifikia lengo kuu la utafiti, uchunguzi huu uliongozwa na madhumuni mahususi yafuatayo:

1. Kuchunguza athari za muktadha halisi wa kijamii katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za amani.
2. Kufafanua dhana ya shani kama inavyojitokeza katika nyimbo za amani katika jamii tatu teule.
3. Kubainisha nyimbo kama kauli ambazo zinajibu na kutarajia majibu kuhusu amani.

## 1.5 Nadharia Tete

1. Usemezano katika nyimbo za amani hudhibitiwa na mazingira na muktadha halisi wa kijamii.
2. Dhana ya shani hujitokeza katika nyimbo za jamii za Kipsigis, Luo na Kisii.
3. Nyimbo za amani hujibu na kutarajia majibu kuhusu amani katika jamii.

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Taifa la Kenya lilipitia hali ngumu baada ya uchaguzi wa mwaka 2007. Ghasia miongoni mwa wafuasi wa vyama maarufu kwa wakati huo zilishuhudiwa. Ghasia zenyewe zilisababisha uharibifu mkubwa wa mali na vifo vya watu wengi mno. Wanajamii wa Kipsigis, Kisii na Luo, ambao ni majirani, walijikuta katika lindi kuu la vita miongoni mwao kutokana na tofauti zao za kisiasa. Mashambulizi yaliyoshuhudiwa yalitukia ghafla na wahasiriwa kulazimika kukimbilia kwa vituo vya walinda usalama kujinusuru. Shirika la msalaba mwekundu pamoja na mshirika mengine ya kibinafsi yalijenga kambi za wakimbizi wa ndani waliokimbia mavamizi katika makazi yao.

Juhudi mbalimbali zimefanywa ili kuzuia hali sawa na hiyo kutukia kwa mara nyingine. Miongoni mwa njia za usemezano zilizowahi kuhusishwa ni pamoja na kutafuta amani kwa kupitia michezo kama vile riadha, kandanda na mikutano ya hadhara. Aidha wanajamii wawakilishi kutoka jamii hasidi waliandaa mikutano ya mapatano iliyofanyika katika maeneo ya mipakani. Mikutano hiyo ilihusisha maandalizi ya vyakula vilivyoliwa kwa pamoja huku wakitalii njia mwafaka zitakazojaribiwa katika kusaka suluhsho la kudumu. Uzukaji wa ghasia hata baada ya juhudi hizi nyingi za kuzidhibiti ni ishara tosha kuwa harakati zenyewe hazikuzaa matunda. Nyimbo ni kipera cha fasihi simulizi kinachoweza kuzungumzia masuala anuwai katika jamii ikiwemo mizozo. Uwezo huu wa nyimbo ukipewa nafasi huweza kutumiwa kama njia mbadala ya kudhibiti kuzuka tena kwa ghasia za baada ya uchaguzi nchini.

Kulikuwa na haja ya kufanya utafiti huu ili kuonyesha jinsi nyimbo za jamii za Kipsigis, Kisii na Luo zinavyosemeza amani. Hili liliwezekana kwa kuchunguza sifa za usemezano katika nyimbo

za amani. Kwa kufanya hivyo, utafiti ulikuwa na mchango mkubwa katika kuhusisha utanzu wa fasihi simulizi na nadharia ya usemezano.

Kwa maoni ya yetu, kulikuwa na haja ya kufanya utafiti huu ili kuthibitisha kuwa usemezano katika nyimbo za amani huathiriwa na mazingira na muktadha halisi wa kijamii. Hali kadhalika kulikuwa na haja ya kufafanua dhana ya shani kama inavyojitokeza katika nyimbo za amani katika jamii na kubainisha nyimbo za amani kama kauli ambazo zinajibu na kutarajia majibu kuhusu amani.

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unahusu usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya. Kazi hii inatarajiwa kuwa na umuhimu hasa ikizingatiwa kuwa ghasia za baada ya kila uchaguzi wa kitaifa nchini Kenya zimekuwa donda ndugu.. Matokeo ya utafiti huu yatachangia katika kuishauri serikali ifumbate utumiaji wa nyimbo kama njia mbadala ya kuiponya jamii endapo itakumbwa na misukosuko sawa na ile iliyoshuhudiwa baada ya uchaguzi wa kitaifa wa 2007 nchini Kenya. Aidha, matokeo ya utafiti wenyewe yataweka msingi dhabiti kwa watafiti wajao ili wazamie zaidi katika kuzishughulikia nyimbo pendwa katika jamii. Masuala ya kijamii kama vile ugonjwa wa UKIMWI yamesemezwa na watunzi na waimbaji wengi wa nyimbo pendwa nchini, hivyo utafiti huu utakuwa kichocheo kwa watafiti wajao.

Utafiti huu pia utawafaidi wasomi na watafiti, kwa kuchangia ufahamu wa uhusiano uliopo kati ya fasihii simulizi na usemezano. Pia utaifafanua nafasi ya nadharia ya usemezano katika kuhakiki nyimbo za amani.

## 1.8 Upeo na mipaka

Jamii nyingi nchini Kenya zina nyimbo nyingi za amani zilizoimbwa katika nyakati mbalimbali. Nyimbo kama hizo huimbwa wakati wowote, kukiwa na vita ama hali ya utulivu. Utafiti wetu haukuweza kuzishughulikia nyimbo zote za amani kwa sababu ni nyingi mno. Kazi hii ilishughulikia nyimbo za amani zilizoimbwa katika jamii tatu teule za Kenya. Jamii zenyewe ni za Kisii, Kipsigis na Luo. Nyimbo zilizoimbwa kati ya mwaka wa 2008 na 2013 ndizo zilizoteuliwa. Uteuzi wa nyimbo hizi ulifanywa kimakusudi kwa sababu tofauti. Kwanza, tuliteua nyimbo zilizobeba maudhui ya amani na zilizoimbwa katika kipindi cha baina ya mwaka wa 2008 na 2013. Mwaka wa 2013 ulikuwa wa uchaguzi nchini hivyo ulijumuishwa katika uchunguzi huu. Pili, tuliteua nyimbo zilizoimbwa na wasanii kutoka maeneo ya Kaunti za Kericho, Bomet, Nyamira na Nyando. Eneo hili liliteuliwa kwa sababu jamii husika zilipigana zenyewe baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007. Kwa mujibu wa kazi hii, jumla ya nyimbo ishirini zilikusanywa kutoka jamii lugha hizo tofauti. Nyimbo tano kutoka kila jamii ziliteuliwa. Aidha, nyimbo zingine tano zilizoimbwa kwa lugha ya Kiswahili na wanamuziki kutoka jamii husika zilihakikiwa. Idadi iliyoshughulikiwa ilifikiwa kwa kuwa zilikidhi mahitaji ya utafiti wenyewe.

## 1.9 Kihitimisho

Katika sura hii, msingi wa jumla wa utafiti umewekwa kwa kueleza vipengele muhimu vya utangulizi, usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti na lengo kuu la utafiti. Hali kadhalika, malengo mahususi yanayoongoza utafiti huu yameelezwa pamoja na nadharia tete. Aidha, sababu ya kuchagua mada ya utafiti imefafanuliwa na pia kueleza umuhimu wa mada ya utafiti. Vipengele hivyo vilituelekeza katika mchakato wa uchunguzi wetu. Katika sura ifuatayo, mapitio ya maandishi yameshughulikiwa.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu mapitio ya maandishi na misingi ya kinadharia. Katika sura hii, tulihakiki maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti. Aidha, tulishughulikia

yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya usemezano na hatimaye tuliweza kutambulisha pengo la kitaaluma.

**2.2 Misingi ya Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya usemezano. Kwa mujibu wa Mbatia (2001), nadharia ni mfumo wa kimawazo wenye kanuni mahususi zinazotoa mwelekeo wa jinsi ya kuihakiki fasihi.

Nadharia iliyotumiwa katika uchunguzi wetu ni ile ya usemezano. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), nadharia ya usemezano iliasisiwa na Mikhail Bakhtin aliyeishi kati ya 1895 – 1975. Usemezano ni mtagusano unaohusu zaidi ya nafsi mbili, na mvutano katika mawasiliano. Bakhtin alichukua msimamo kwamba kazi ya fasihi lazima itilie mkazo muktadha maalumu wa kihistoria na jamii kwani umbo la fasihi ni chombo katika uhakiki wake wa jamii. Jambo hili lilitufaa katika utafiti wetu kwa kuchunguza muktadha maalum wa kihistoria miongoni mwa jamii za Kipsigis, Kisii na Luo ambamo nyimbo tunazozishughulikia ziliimbiwa. Tulifaidika kwa kuelewa jinsi waimbaji walivyoathiriwa na miktadha na mazingira yao katika utunzi na uimbaji wao.

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981), riwaya ndiyo sajili bora kuliko sajili nyinginezo katika kusemeza masuala anuwai ya kijamii. Hii ni kwa sababu lugha yake nzima imo katika usemezano. Yeye anasema kuwa lugha ya ushairi, kuanzia mwanzo hadi mwisho wake, ni kama mtu mmoja tu ndiye anayezungumza wala hakuna ushirika wowote. Katika lugha ya ushairi, ni mshairi tu ndiye asemaye wala hakuna mtu yeyote anayemjibu mshairi huyo kwa sababu lugha ya ushairi haikubali mwingilio wowote wa wasemezwa. Katika upande wa lugha ya riwaya, Bakhtin anadai kwamba riwaya pekee ndiyo inayochanganya sajili zote kwa pamoja na pia ndiyo pekee inayokubali maingiliano na hadhira yake. Aidha ndiyo inayojuvya kwamba kuna wahusika

wawili wanaoshirikiana katika kusemezana na basi ndipo riwaya inaendelea. Maelezo haya yalitufaidi katika utafiti wetu kwa kuuchochea uchunguzi zaidi na kuthibitisha kwamba nyimbo za amani kama ilivyo riwaya hudhihirisha sifa za usemezano.

Akijadili kuhusu neno, Bakhtin (1986) anasema kwamba neno ni pande mbili katika kitendo kimoja kwani kila neno humlenga msemezwa. Hili huwezekana kwani neno huwa katika mahusiano ya pande mbili, yaani msemeza na msemezwa. Jambo hili lilitufaidi katika kuchunguza ikiwa maneno yaliyo katika nyimbo za amani ni yenye uwili, hata ikiwa ni neno moja. Tumechunguza pia msemeza ni nani na anasemezana na nani katika nyimbo za amani. Kwa mujibu wa kazi hii, mwimbaji ndiye msemeza naye hadhira ni msemezwa.

Akizungumzia matamshi, Bakhtin (1986) anasema ya kwamba matamshi huwa katika sajili mbalimbali na msemeza. Mtu hujifunza kuzungumza kulingana na vile anavyosikia wengine wakiongea. Yale maneno ambayo msemeza atazungumza kwanza humjulisha msemezwa ni sajili gani atakayotumia kuyajibu. Hapa ndipo msemezwa huweza kuelewa yeye atatumia sajili gani katika kumjibu msemeza. Kauli hii ilitufaa katika kuchunguza sajili ambayo inapatikana katika nyimbo tulizozishughulikia na zinajitokeza kwa namna gani.

Mbali na msemeza (nafsi ya mtunzi au mwimbaji), kuna nafsi nyingine, “yeye” ambayo husemezana na msemeza. Kwa hivyo, kila mnenaji anavyoendelea kunena, huwa tayari

anachukua jukumu kubwa la kumjibu mnenewa. Majibu hayo si lazima yasikike. Kusisimka kwa msemezwa humjuza msemeza auchukue mkondo fulani katika usemezano wake. Kwa hivyo basi, lugha ya usemezano ni ile inayoingiliana na isiyokuwa na mwelekeo mmoja bali mielekeo miwili. Morson (1986) anadai kwamba usemezano hauwezeshwi iwapo kuna mnenaji na upande wa pili msikilizaji ambaye hafanyi kitu kingine ila kusikiliza tu. Nafsi ya "mimi" haiwezi kujitambua hadi itambue kwamba kuna nafsi ya "yeye". Nafsi moja haiwezi kujijua hadi pale ambapo itapata nafsi nyingine. Kwa hivyo "mimi" itajitambua kwa "yeye". Maana ya suala lolote haijulikani hadi ipate jibu kutoka kwa suala lingine. Kwa mfano, maana ya "amani" haijulikani hadi itakapozuka "vita", kwa hivyo jibu la amani ni vita. Katika kujibu ndiyo maana ya kitu inajulikana. Kuwako kwa kitu kutategemea kama kitu hicho kina maana (Holquist 1990). Walakini, "mimi" nitamtambua "yeye" kwa "yeye" kunijibu "mimi" na hapo ndipo kuwapo maana iliyokusudiwa.

Uzungumzi nafsia ni usemezano vilevile. Mukarovsky (1977) anadai kuwa katika uzungumzi nafsia, nafsi moja hujisemea yenyewe ikiwa ni kwa mawazo tu au inajiambia kwa sauti mpaka watu wakamsikia. Katika uzungumzi nafsia, nafsi moja inachukua nafsi mbili ili kutosheleza usemezano.

Kwa mujibu wa Morson (1986), majibizano kati ya mzungumzaji na mzungumziwa yanatokana na kuathiriana kwao. Hakuna mtu yeyote anayetoa tamko halafu akajigamba nalo kwamba yeye ndiye wa kwanza kulisema isipokuwa Adamu pekee kwani alikuwa mtu wa kwanza kufundishwa

maneno, (Bakhtin 1981). Kwa mujibu wa ufafanuzi huu, ni dhahiri kwamba hakuna atamkaye neno ila ameathiriwa kwa njia moja au nyingine. Ama atalipinga, atalitolea rai, ataliongeza au atalipunguza. Kutokana na maelezo haya, utafiti wetu ulifaidika na kuelewa kwamba matamshi hayatakwisha na kwamba hata kama nyimbo za amani zinazotafitiwa tayari zimeshaimbwa, bado nyimbo hizi zinawahamasisha waimbaji wengine wazijibu kwa njia yoyote ile, iwe ni kuzikataa au kukubaliana nazo.

Holquist (1990) akimnukuu Bakhtin, anaeleza kwamba riwaya pekee ndiyo sajili inayotegemea sana uathiriano wa matini nyingine. Riwaya hudondoa sana kazi nyingine kwa njia moja au nyingine na athari moja ni kuwa riwaya huathiri kazi nyingine ambazo hujidai kuwa safi na pweke na hazina chembe ya athari. Matini nyingi huathiriana na kutokana na kuwa nafsi mbili zikishajitambulisha kwamba zinapatikana, basi nafsi moja haitoanza kutamka hadi ijue nyingine inasema nini. Kwa hivyo, "mimi" tayari ashawaza jibu la "yeye" kabla ya "yeye" kulitamka. Na "mimi" naye hatamki ila amemsikia "yeye" akisema. Kulingana na maelezo haya, uathiriano ni kwenda nyuma (kumsikia mtu akisema) na kwenda mbele (kuathiri majibu ya atakayekuja hatimaye). Maelezo haya yalituandalia dira ya kutumia nadharia hii ya usemezano kama kipimo cha kuhakiki nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu teule za Kenya.

**2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti**

Sehemu hii inachunguza maandishi mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Tahakiki hizo zilitumiwa kumwelekeza mtafiti kuhusu mitazamo na mielekeo ya wataalamu mbalimbali

kuhusu mada ya utafiti. Katika kufanya hivi, mtafiti alibainisha pengo ambalo utafiti huu unakusudia kuliziba.

Nyimbo zimetumika katika harakati za kuizindua jamii kuinuka na kujikomboa kutokana na vitendo vya kidhalimu. Vershbow (2010) ameshughulikia nyimbo za ukombozi kutokana na utawala dhalimu wa Afrika Kusini na kudhihirisha uwezo wa nyimbo katika kuikomboa jamii. Wananchi weusi wa Afrika Kusini walifanikisha harakati zao za kujikomboa kutokana na udhalimu wa Makaburu waliowadhalilisha kwa miaka mingi. '*Toyi Toyi'* iliyo na chimbuko kule Zimbabwe, ni densi ya kivita iliyochezwa na Waafrika weusi wa Afirika Kusini nyakati za kutafuta ukombozi kutoka kwa utawala wa Kaburu. Kwenye mikutano ya kuwahamasisha raia kuhusu haja ya ukombozi, viongozi wa chama cha *Africa National Congress* (ANC) wangetoa kauli *'Amandla'* (nguvu/uwezo) nao wananchi au hadhira kuitikia *'Awethu'* (yetu/wetu). Kauli hizi zilinasa hisia za furaha, uchungu, hamasa, kuvunjika moyo na faraja. *Toyi toyi* ni kauli yenye nguvu zilizotumiwa na waliokandamizwa kuwasilishia malalamiko yao kwa serikali tawala. Nyimbo hizi zilitumiwa kusemeza masuala yaliyowazindua wananchi kuona haja ya kushiriki kikamilifu katika harakati zao za kujikomboa kutoka kwa Makaburu. Mfano wa wimbo wa ukombozi:

| | |
|---|---|
| *When your government gets you down* | serikali yako ikikugandamiza |
| *When you are sick of all those racist clowns* | ukichoshwa na hao makaburu |
| *Just when you think you're gonna drown* | na wakati waelekea kutamauka |
| *The best thing you can do when you want* | jambo bora la kutenda unapokaribia |
| *to lose your frown is to...* | kupoteza matumaini ni... |

*TOYI TOYI raise your fist in the air* TOYI TOYI inua konzi angani
*TOYI TOYI for a world that is fair* TOYI TOYI kwa dunia yenye haki
*TOYI TOYI raise your fist to the sky* TOYI TOYI inua konzi angani [1]

Kutokana na wimbo huu, inabainika kwamba suala la ubaguzi wa rangi limerejelewa na hilo likiwa tatizo sugu lililowahangaisha wanajamii katika taifa la Afrika Kusini. Waimbaji wanasemeza dhiki wanazozipitia na uamuzi wa mustakabali wao. Nyimbo hizi za *Toyi Toyi* zinadhihirisha mielekeo miwili katika kusemeza hali ya jamii ya wakati uliorejelewa. Nyimbo hizo zilitufaidi katika kubaini sifa za usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya.

1 Cape Town Magazine, (2002). *Amandla! A four part harmony Documentary*

Nyimbo husemeza masuala yanayohusu maisha kwa jumla. Gakahu (2008) amebainisha namna ambavyo nyimbo huelekeza jamii juu ya haja ya kuzidhibiti hisia zao ili kuuangamiza ugonjwa sugu wa UKIMWI. Uchunguzi huo ulilenga vijana hususan kwa kuwa wao ndio sehemu ya umma iliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa kwa kuwa wametawaliwa na fukuto la ujana. Akitumia nyimbo pendwa kama vile *'vuta pumzi'* iliyoimbwa na mwanamuziki *Juacali*, Gakahu anaonyesha jinsi wanaume wamekashifiwa vikali kwa sababu ya uchu wao uliokithiri. Wanaume wanaorejelewa huwakodolea macho wanawake wapitao njiani huku wakiwamezea mate. Wimbo unaeleza: *'tako lisipite tu mate yashamtoka, kila shimo unaona unadunga…'* Wanaume hapa wanaonywa dhidi ya uchu wa ngono kwani huwaangamiza maishani. Gakahu amedhihirisha

namna ambavyo usemezano umetumika kuionya jamii kuhusu mienendo hasi inayoweza kuyahatarisha maisha yao kwani UKIMWI haubagui yeyote. Mtunzi na mwimbaji wa wimbo vuta pumzi amedhihirishba nafsi tatu katika kazi yake. Kwanza kuna mwimbaji anayetoa ushauri, wa pili akawa msikilizaji wake na tatu ndiye msemezwa ambaye ni mwanaume asiyeweza kudhibiti hisia zake. Gakahu alijikita katika nafasi ya nyimbo katika kuelekeza vijana dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI lakini uchunguzi wetu ulihusu usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya.

Misukosuko imekuwa halia isiyoweza kuepukika katika jamii yoyote ile, na nyimbo zimetumika kuyapunguza makali ya sitofahamu hizo. Simson (2014) ameangazia namna ambavyo nyimbo zimetumiwa katika jitihada za kurejesha hali ya utangamano nchini Sudan Kusini. Mwanamuziki *Meen Mabior* kupitia nyimbo, amechangia kwa katika juhudi za kujenga jamii yenye ushikamano baada ya vita vilivyoikumba nchi hiyo mwishoni mwa mwaka wa 2013. Jeshi la *Sudan People's Liberation Army* (SPLA) lilitumia nyimbo kujitia motisha wakati wa kupigania ukombozi wa nchi yao. Ufanisi wao vitani ulipata msukumo mkubwa kutoka nyimbo zilizowapa himizo tele. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba nyimbo husemeza maudhui ya ujenzi wa jamii mpya baada ya vita. Maelezo haya yalitupa dira ya kuchunguza mchango wa nyimbo za amani katika kusemeza amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya.

Nyimbo zinaweza kusemeza mambo yanayoweza kuleta chuki miongoni mwa wanajamii. Stone (2010) akitoa mfano wa nchi ya Rwanda, amebainisha namna ambavyo vita vilichochewa kupitia nyimbo za uhasama mwaka wa 1994. Kabila la wengi la Hutu lilitumia propaganda kuliangamiza lile la Tutsi ambalo ni dogo. Kupitia vyombo vya habari, nyimbo zilitumiwa kuchochea mauaji ya kikatili yaliyodumu siku mia moja na kusababisha vifo vya Watutsi zaidi ya laki nane. Stone

(*The Independent* (17/01/2010) akishughulikia nyimbo za amani, aliwaangazia waimbaji Iain Swart na Jean-Paul Samputu. Wanamuziki hao walitunga wimbo *'Window of Peace'* na kushirikisha kikundi cha waimbaji waliokuwa wamewachwa mayatima katika mauaji yaliyotekelezwa na *Interahamwe.* Mwimbaji Samputu mwenyewe aliwapoteza wazazi wake kupitia mikono ya mwendani wake wa tangu utotoni. Aidha, washiriki wa kikundi hicho cha uimbaji walishuhudia mauaji ya wapendwa wao wakiwa wachanga mno. Mmoja wa waimbaji alisimulia tukio ambalo akiwa na umri wa miaka 12, alishuhudia mauaji ya wazazi wake kwa kukatwa kwa upanga na maiti zao kuteketezwa kisha kutupwa kwenye mto wa Nyabarango. Wimbo *'Rwandan Dream'* (ndoto ya Rwanda) uliozungumzia haja ya watu kuishi kwa amani na utangamano ulipata umaarufu mkubwa kule Rwanda. Athari za utungo huo zilidhihirika miongoni mwa wananchi ambao wameshirikiana kuijenga nchi yao upya. Uhakiki wetu ulikuwa tofauti na huu kwa kuwa tulizingatia namna nyimbo za amani zinavyosemeza maudhui ya amani miongonimmwa jamii tatu teule za Kenya.

Vyombo vya habari hutekeleza dhima kuu ya kutaarifu umma kuhusu matukio mbalimbali katika jamii. Kutol na wenziwe (2009) wameshughulikia mchango wa vyombo vya habari hususan magazeti ya "*Taifa Leo"* na "*The Standard"* katika kukabiliana na ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007/2008 nchini Kenya. Kutol na wenziwe wanadhihirisha kwamba kwa njia moja au nyingine, magazeti yalielekea kuchochea ari na hisia hasi na kupelekea kutatiza hali ya amani nchini Kenya.  Kwa mujibu wa ripoti ya Wachunzaji wa Muungano wa Nchi za Ulaya, vituo vingi vya habari nchini Kenya vilidhihirisha mapendeleo katika taarifa zao wakati wa matayarisho ya uchaguzi mkuu wa 2007. Ilibainika kwamba Shirika la Habari la Kenya (KBC) lilipendelea chama cha PNU na kukipa asilimia 76 hewani, nacho cha ODM kikipewa asilimia

13, ODM-K asilimia 5 na vyama vile vingine vikipewa kiasi kilichosalia cha asilimia 6 tu. Kazi hii imedhihirisha namna ambavyo vyombo vya habari vinavyoweza kusemeza masuala mbalimbali yanayokumba jamii. Masuala mengi husemezwa na viongozi kwa umma. Baadhi yayo yaweza kuchochea uhasama au wakati mwingine kutuliza hali tata. Sifa ya usemezano ya uwingi wa ndimi hudhihirika kupitia vyombo vya habari.

Baadhi ya wanajamii wamejaribu mikakati ya kutafuta amani ya kudumu. Odongo (2004) alishughulikia mchango wa wanawake katika kukuza amani nchini Kenya. Kazi hiyo ilijikita kwenye ghasia za mwaka wa 1992 zilizoshuhudiwa katika mkoa wa Bonde la Ufa. Ghasia hizo ambazo ziliwashirikisha jamii za Kikuyu na Kalenjin, zilielezwa kwamba zilitokana na mzozo wa umiliki wa ardhi. Wakalenjin waliwaona Wakikuyu kuwa wavamizi wa mashamba yao. Sababu kuu ya kushirikisha wanawake katika kazi hiyo ni kwamba wanawake na watoto huathirika zaidi panapozuka hali ya misukosuko katika jamii. Utafiti wetu ulizingatia namna ambavyo nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya zilivyoweza kusemeza suala la amani baada ya ghasia zilizozuka baada ya uchaguzi wa 2007 nchini Kenya.

Tahakiki ya wimbo wa msanii wa Kimarekani Cat Stevens, inadhihirisha jinsi ambavyo nyimbo huwa na uwezo mkubwa katika kuileta hali ya utulivu nyakati za misukosuko. Aaron (2011), ameshughulikia wimbo wa mwimbaji Cat Stevens. Cat Stevens aliutunga na kuuimba wimbo '*Peace Train'* (gari moshi la amani) mwaka wa 1971. Mwaka huu wa 1971 ulikuwa msimu uliokuwa na misukosuko katika taifa la Marekani kwa kuwa vita vya kule Vietnam vilikuwa vimechukua zaidi ya miaka minane tangu kuanza. Raia wengi wa Marekani walitaka vita hivyo

visitishwe na kurejeshwa nyumbani kwa askari ambao walikuwa wamesalia vitani. Katika wimbo wa Cat Stevens, maneno *I have been happy lately…I have been smiling lately* (siku hizi nina furaha… nimekuwa na tabasamu siku hizi) yaliibua matumaini ya hatima ya vita hivyo. Jamii ya Waamerika ilipata matumaini mapya juu ya hali tulivu ijayo. Cat Stevens akilinganisha amani na gari la moshi, aliweza kusemeza wazo la kupinga vita na chuki miongoni mwa umma kwa jumla.Stevens anadhihirisha hisia zake kwa kutumia taswira ya gari la moshi lipitalo ukingo wa kiza totoro unaowakilisha hisia za chuki.Anaendelea kusema kuwa kiza la chuki haliwezi kuepukika katika jamii. Kupitia juhudi za pamoja za wanajamii, dunia inaweza kuupitia ule ukingo wa misukosuko ikiwa kitu kimoja ndani ya lile gari la moshi la amani siku moja. Kazi hiyo inapendekeza njia mbadala ya kukuza amani katika jamii. Tahakiki ya wimbo huu *Peace Train* imeichochea azma ya kuzichunguza jinsi ambavyo nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya zinavyosemeza suala la amani katika jamii.

**2.4 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya Usemezano**

Bakhtin (1981) anadai kwamba usemezano haupo katika ushairi bali huwa katika riwaya pekee. Njogu (1993) ameyarekebisha madai haya kwa kuonyesha kwamba ushairi simulizi ni wa kiusemezano tukizingatia kuwepo na kushirikishwa kwa hadhira. Anaonyesha kuwa uriwaya upo katika ushairi wa Kiafrika. Kama riwaya, ushairi huwa ni kongamano la semi, sajili na lugha. Ushahidi wake anautoa katika ushairi wa Afrika Mashariki wa Gungu, Kimando na Gicaandi, Njogu anafafanua jinsi tungo hizi zinavyodhihirisha usemezano. Sifa zote zilizopewa riwaya zilipatikana katika ushairi. Kwa ajili ya utafiti huu, tulitumia sifa hizi za ushairi kuzihakiki nyimbo za amani zilizoteuliwa kimakusudi, tukifahamu fika kwamba nyimbo ni ushairi nao ushairi ni nyimbo. Utafiti huu ulitofautiana na wetu kwa kuwa sisi tulichunguza sifa za

usemezano katika nyimbo za amani ilihali Njogu (1993) alirekebisha madai ya Bakhtin kwamba usemezano upo tu katika riwaya.

Kea (2006) amechunguza usemezano katika nyimbo za taarab. Katika kazi yake amedhihirisha kuwa sifa za usemezano zipo katika nyimbo za taarab. Kea alilenga kuchunguza athari za muktadha na mazingira katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za taarab. Amedai kuwa kuna uhusiano kati ya muktadha na usemezano. Muktadha unaeleza taratibu na maana ambayo hubainishwa kwa kutumia urejelezi tofauti katika mazungumzo au maongezi. Ni kutokana na mtazamo huu ndipo alichunguza muktadha na mazingira ya utungaji na uimbaji wa nyimbo za taarab ambazo zilitungwa na Juma Bhalo na Maulidi Juma Iha. Mazingira ambayo yanakuza muktadha wa utunzi wa watribu hawa Juma Bhalo, Maulidi Juma Iha na Zuhura Swaleh ni mji wa Mombasa.

Kea anasema katika desturi za nWaswahili, majukumu ya wanawake ni kumtunza mume wake na wana wake na shughuli zao zote hulenga suala hilo. Wanawake huwajibika kuwafundisha mabinti zao maadili mema. Watoto hao wa kike wa Waswahili hushauriwa wawe wenye tabia njema kabisa. Hii ni kwa kuwa Uswahilini, mwanamke sio tu mtu mrembo wa sura bali pia wa tabia. Kwa mfano, Bhalo aliamua kutumia jazanda ya gunia zito ili kuelezea maudhui ya malezi katika jamii. Matumizi ya dhana hii hutupa kufahamu mazingira anamotungia wimbo. Wachukuzi bandarini hutumia magunia kuibebea mizigo. Aidha, gunia zito hapa huwakilisha msichana aliyeshinda wazazi wake kwa tabia yake oza tena mbovu. Bhalo anamfananisha na gunia lililojaa mzigo na hivyo kuwa jambo gumu kulibeba. Uchunguzi huu ulitupa dira katika kufahamu kwamba muktadha una athari katika kazi ya fasihi. Sababu hapa ni kuwa  mtunzi

hutunga kuhusu mambo yanayomzunguka katika mazingira yake anamokulia. Utafiti wa Kea umejikita katika usemezano katika nyimbo za taarab lakini wetu unaangazia usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii za Kenya.

Muriithi (2002) alishughulikia usemezano katika tamthilia ya Kiswahili. Akishirikisha tamthilia za *Mashetani*,(Hussein, 1971), *Kilio cha Haki*,(Mazrui, 1981) na *Amezidi* (Mohammed, 1995), aliweza kubainisha kuwa usemezano upo katika tamthilia ya Kiswahili. Yeye aliangazia lugha ya wahusika pale ambapo amesema kuwa wahusika hupewa lugha ambayo wanaitumia kwa kutegemea majukumu yao. Kulingana na Bakhtin (1981), lugha ambayo wahusika hupewa huwa mara nyingi inaonyesha matumaini na imani ya mwandishi kwa kuwa lugha yao huwa ya "wengine". Mwandishi hawezi kupanua mawazo na fikra zake kupitia kwa lugha anayowapa wahusika wake peke yake, hivyo basi lugha ya wahusika pamoja na lugha ya "wengine" hutumiwa ili kuleta uwingi wa ndimi.

Muriithi akimrejelea Pearce (1994) akifafanua usemezano, ametoa jazanda ya simu pale ambapo kuna wahusika angaa wawili, msemeza na msemezwa. Muriithi anasema kuwa msemeza wa mazungumzo ya rununu hana budi kuonyesha kuwepo kwa yule anayepokea simu; msikilizaji wake. Mahitaji ya mawasiliano humlazimisha kutoa sauti. Kwa hivyo inakuwa ni kama kwamba mzungumzaji na mzungumziwa huweza kuzungumzaambapo sauti ya mmoja wao huwa ni ya mzungumzaji na kwa upande mwingine kuna sauti ya msikilizaji. Kama vile simu, neno ni nafsi iliyoko na iliyomilikiwa na msemaji na msemewa kwa pamoja kwani hii ni sifa iliyoko kati ya hadhira na mbunaji. Utafiti huu ulitufaa kwa kutupa mwanga kuhusu namna ambavyo nadharia

ya usemezano inavyotumiwa kuhakiki kazi za fasihi hususan tamthilia na hata ushairi. Hata hivyo, uchunguzi huu umetofautiana na utafiti wetu huu unatafiti usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya.

Karama (1996) alifanya utafiti kuhusu usemezano katika ushairi wa Kiswahili. Aliteua utenzi wa Al-inkshafi. Karama alishughulikia kipengele kimojawapo cha usemezano nacho ni kuwepo kwa kuathiriana na maandishi mengine. Alidhihirisha haya kwa kuonyesha kuwa kuna mwangwi wa *Al- Inkishafi* katika *Tabaraka Dhul Ulaa* iliyotungwa na Hujjatul Din Muhammad bin Abdul Aziz Al – Waraq. *Al – Inkishafi* iliyoandikwa na Sayyid Abdalla na *Tabaraka Dhul Ulaa* zimeathiriana. Kazi hizi mbili zimeingiliana na kutegemeana. Kwa mujibu wa Karama, tendi hizi mbili zinaonekana kufanana kwa kuwa mianzo yao haikosi kulitaja jina la Mwenyezi Mungu. Katika ubeti wa kwanza wa *Tabaraka,* mtunzi Al Waraq hakuanza na utajo wa neno bismilahi kama vile alivyofanya Sayyid Abdalla bali alianza kwa kumsifu Mwenyezi Mungu, ambayo pia ni tafsiri nyingine ya "himdi", ambayo kwa maelezo marefu ni "kila jinsi ya sifa njema zamstahiki Mwenyezi Mungu" na baada ya kutoa shukurani zake, yeye anaanza tena kutaja utukufu wa Mwenyezi Mungu.

Aidha, Karama ameangazia majibu ya usemezano. Akirejelea *Al - Inkishafi,* anaeleza kuwa katika usemezano, majibu haswa ambayo mtu anapata ni ule msisimko wakati tamko fulani linapotamkwa. Msisimko huu mara nyingi unaweza kuwa wa kupinga, kutolea rai au kuzidisha nguvu. Mtu asipojibu kwa kutamka, ukimya ule wa msemezwa vilevile hufasiriwa na msemeza kuwa ni jibu. Hii ni kwa kuwa jibu si lazima litolewe papo kwa hapo bali hata kama jibu hilo

likiachwa mpaka baadaye, huo mshawasha alioupata msemezwa bado utachukuliwa kuwa ni jibu. Ni kutokana na majibu basi ndio dhana ya usemezano inajitokeza. Haya yanaonyesha kuwa matamshi yote yako katika usemezano. Hata kama mhusika ndio tu anaanza kutamka, matamshi yake hayatokani na ombwe tupu ila kuna aliyemtangulia katika kusema, ikiwa sio leo na si juzi ni siku nyingine yoyote. Hakuna binadamu anayeweza kudai kuwa ndiye wa kwanza kulisema tamko fulani (Bakhtin 1981:279).

Karama anadai kwamba *Inkishafi* ni jibu la Sayyid Abdalla kwa umma ambao ulikuwepo wakati huo na wa siku ambazo zitakuja. Ni mshawasha kwa kuwa kabla yake, kulitanguliwa na tendi nyingine ambazo zilikuwa maarufu kama jinsi ulivyo utendi wa *Al – Inkishafi* hivi leo. Mifano ni *Swifa ya mwana Munga* (1517) na *Hamziyya* (1652). Utafiti huu wa Karama ulituwezesha kufafanua kauli ya Bakhtin kwamba kuna kuathiriana kwa matini. Utafiti huu umetofautiana na wetu kwani tulichunguza usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya.

### 2.5 Utambulishaji wa Pengo la Kitaaluma

Wataalamu mbalimbali wamevutiwa na maudhui maarufu mathalani siasa, uchumi, masuala ya mahusiano na ya dini. Maandishi kadhaa yanayohusu usemezano katika nyimbo hujikita katika taarab. Tahakiki nyingine vilevile zimeshughulikia nyimbo kama kipera cha ushairi simulizi katika fasihi. Utafiti ulioshughulikia usemezano katika nyimbo za amani hata hivyo haujapata

kutekelezwa kwa kina hivyo tunadhamiria kuliziba pengo hili kwa kushughulikia nyimbo za amani.

## 2.6 Kihitimisho

Katika sura hii, masuala muhimu yameshughulikiwa yakiwemo mapitio ya maandishi, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya usemezano na hatimaye utambulishaji wa pengo la utafiti. Sura inayofuata itajadili mambo muhimu yaliyoshirikishwa katika michakato ya ukusanyaji data.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Utafiti huu ni wa kimaelezo ambapo nyimbo zilinukuliwa, kutafsiriwa na sifa za usemezano kufafanuliwa. Sehemu hii imejadili mbinu za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Ili kutimiza malengo ya utafiti wetu, tulitumia mbinu ya utafiti wa uchunguzi nyanjani na maktabani. Aidha, tulitumia vifaa vya kukusanya na kuchanganua data kama vile tepu rekoda, tarakilishi na runinga. Hatimaye tumejadili jinsi data ilivochanganuliwa.

### 3.1.1 Uchunguzi Nyanjani

Utafiti ulifanywa nyanjani kwa nia ya kukusanya nyimbo za amani. Nyimbo ambazo zilikidhi mahitaji ya uchunguzi wetu ya kuhubiri amani miongoni mwa wanajamii ziliteuliwa na kununuliwa. Uteuzi wa nyimbo ulifanyika kwa kuzingatia vipengele anuwai vya usemezano vilivyohitajika kwa ajili ya uchunguzi wetu. Mtafiti aliweza kutembelea maduka ya kuuza CD za nyimbo husika katika miji ya Kericho, Bomet, Nyamira Sondu na Kisumu. Mjini Kericho, mtafiti alitembelea duka la *'The Great Commission Singers'* ambapo nyimbo za Kikipsigis za kidini ziliweza kupatikana. Hali kadhalika, nyimbo zisizo za kidini zilinunuliwa kutoka duka la Mr. D sounds mjini Kericho.

Nyimbo za Kikisii zilichaguliwa na kununuliwa kutoka mji wa Nyamira. Akiandamana na mtafiti msaidizi, mtafiti aliyatembelea maduka mawili ambamo CD zilizokidhi mahitaji ya uchunguzi wetu ziliweza kununuliwa.

Mjini Bomet, CD za nyimbo zisizo za kidini ziliweza kupatikana katika duka la '*Makiche Music Store.*' Nyimbo zenye maudhui yanayooana na mahitaji ya uchunguzi huu ziliteuliwa kimakusudi na kununuliwa.

Katika kituo cha kibiashara cha Sondu na jiji la Kisumu, mtafiti alifanikiwa kuzichagua na kuzinunua CD zenye nyimbo zinazokidhi mahitaji ya utafiti wetu. Mtafiti msaidizi aliyeteuliwa kimakusudi, alimsaidia mtafiti katika uchaguzi wa nyimbo husika. Mkusanyiko wa nyimbo teule ulihifadhiwa katika kompyuta. Data zenyewe zilikuwa kwenye CD na video.

### 3.1.2 Utafiti wa Maktabani

Utafiti maktabani ulituwezesha kuyapitia na kuyahakiki maandishi mbalimbali kuhusu nyimbo na suala zima la amani. Mapitio ya maandishi husika yalituwezesha kupata habari zaidi kuhusu hali ya amani katika mataifa mengine ya kiafrika na hata ulimwenguni kwa jumla na pia nchini Kenya. Hali kadhalika, mapitio hayo ya maandishi yalitupa mwanga juu ya mikakati iliyowekwa ili kukabiliana na hali zinazotatiza ushikamano wa kijamii. Vitabu vyovyote vile ambavyo vinahusiana na usemezano pamoja na nyimbo vilisomwa. Hivi vilitupa data ambayo inahusiana na usemezano ambapo tulipata mihimili mahususi ya nadharia ambayo tumeitumia. Makala yoyote kuhusu nyimbo za amani pamoja na uhakiki wake yalisomwa pia ili kutusaidia kuelewa utanzu wa nyimbo ipasavyo na uhakiki wake ambao umefanywa. Kupitia data hii, tuliweza kufahamu matokeo ya uhakiki uliofanywa na wengine na hivyo tukaweza kuelewa vizuri walifanya nini, wakapata matokeo yapi na upungufu ni upi.

Aidha, tulitalii tovuti ili kupata habari zaidi kuhusiana na suala la utafiti. Pamoja na hayo, tulizuru maktaba ya Chuo Kikuu cha Kabianga na ya kitaifa mjini Kericho. Tulivitembelea vituo vya redio kama vile Redio Injili, Ramogi FM na Egesa FM ambapo tulipata nyimbo za wasanii walioteuliwa kwa ajili ya utafiti huu.

## 3.2 Sampuli

Kwa kutumia uteuzi wa sampuli ya kimakusudi, tulishughulikia jumla ya nyimbo arobaini (40). Uteuzi wa nyimbo zenyewe uliongozwa na vigezo vifuatavyo: kwanza maudhui yazo yalikuwa yamejikita kwenye amani katika jamii, pili nyimbo zenyewe zilikuwa zile zilizoimbwa na wanajamii walioteuliwa kwenye utafiti huu na mwisho zilikuwa zile zilizoimbwa baina ya mwaka 2007 na 2013. Kutokana na utaratibu huu, tuliweza kuteua nyimbo ishirini ambazo tuliona zingekidhi mahitaji ya uchunguzi wetu. Nyimbo tano (5) kutoka jamii ya Kipsigis, tano (5) zilizoimbwa kwa Kikisii, tano (5) zilizombwa kwa Kijaluo na tano (5) zilizoimbwa kwa Kiswahili na wasanii kutoka jamii hizo tatu. Watafiti wasaidizi kutoka jamii za Kisii na Luo walitusaidia kuzitambulisha nyimbo mahususi zilizotufaa. Wao wenyewe walizisikiliza na wakiongozwa na vile vigezo vya kimsingi tulivyowawekea, waliviteua kimakusudi nyimbo zenyewe. Nyimbo za jamii ya Kipsigis ziliteuliwa kimakusudi na mtafiti ambaye ni mzaliwa wa jamii hii. Watafiti hao wasaidizi kutoka jamii za Kisii na Luo waliotusaidia kuzitafsiri nyimbo kutoka jamii husika. Uteuzi wa nyimbo hizo ulizingatia vipengele vya usemezano vinavyodhihirika pamoja na maudhui ya kukuza amani miongoni mwa wanajamii husika.

Mbali na kuteua nyimbo, wasikilizaji wa nyimbo hizo waliteuliwa kimakusudi. Wahusika katika makundi teule walitarajiwa kusikiliza na au kutazama nyimbo zikichezwa kwenye CD kisha kuelekezwa kubainisha sifa za usemezano katika nyimbo husika.

**3.3 Vifaa vya Utafiti**

Kuna vifaa anuwai vinavoweza kutumiwa katika michakato ya kukusanyia, kuchanganulia na kuhifadhia data katika utafiti. Katika utafiti huu, tulitumia CD na VCD za nyimbo zilizoteuliwa kimakusudi. Aidha, tulitumia tarakilishi na runinga kama vifaa vya utafiti.

### 3.3.1 Runinga na Tarakilishi

Vyombo hivi vilitumiwa kuchezesha CD zenye nyimbo zilizoteuliwa kimakusudi. Kwa kutumia runinga, tuliweza kuchanganua nyimbo husika kiutendaji kwani hubainisha miondoko ya kimwili na ishara mbalimbali zinazoambatana na uimbaji. Tulisikiliza nyimbo zilizokuwa katika CD kwenye tarakilishi.

### 3.3.2 Uchanganuzi wa Data

Nyimbo zilizokusanywa zilipangwa kwa kutegemea mada kuu na kisha mada nyinginezo. Watafiti wasaidizi walinakili nyimbo zilizoteuliwa kwenye madaftari. Nyimbo za Kikisii na Kijaluo zilinukuliwa kwanza katika lugha chanzi kisha zikatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kabla ya kuchanganuliwa. Wapo wasemaji wengine wazawa wa lugha hizi mbili waliohakikisha kuwa kile kilichonakiliwa na kisha kutafsiriwa vilikuwa sahihi. Maelezo muhimu yaliyotokana na data hii yalidondolewa na kutumika katika kufafanulia masuala na hoja muhimu katika utafiti huu. Data hiyo ilichanganuliwa kwa kuzingatia vipengele vilivyotafitiwa na malengo ya utafiti, kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya usemezano.

Baada ya maneno kwenye nyimbo zilizoteuliwa kunukuliwa madaftarini na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, mtafiti alizipitia na kuzifasiri. Baadaye, mtafiti aliweza kuteua baadhi ya beti za nyimbo au wimbo mzima na kuutoa kama mfano ili kudhihirisha sifa za usemezano katika nyimbo hizi za amani. Sifa husika zilidhihirika katika baadhi ya beti za wimbo fulani au katika wimbo mzima.

### 3.3.3 Uwasilishaji wa Data

Tuliyanakili maneno yaliyomo kwenye nyimbo hizo kwenye madaftari ili kuyapata maudhui yaliyokidhi mahitaji ya uchunguzi wetu. Hatimaye, nyimbo hizi zilitumiwa katika uchanganuzi kwa kuzingatia sehemu zinazohusiana na suala la utafiti. Baadhi ya sehemu hizo ni vipengele vya usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Kenya.

### 3.4 Kihitimisho

Katika sura hii, tumedhihirisha mbinu zilizotumika katika utafiti wetu. masuala muhimu yameshughulikiwa yakiwemo mbinu za utafiti kwa jumla. Mambo muhimu yaliyoshughulikiwa ni kama vile ukusanyaji wa data, mchakato wa usampulishaji na vifaa vilivyotumiwa kukusanya data hiyo. Hatimaye, uchanganuzi wa data husika na uwasilishaji wa matokeo uliangaziwa.

Sura ifuatayo imeshughulikia uchanganuzi wa nyimbo za amani zilizoteuliwa kimakusudi kwa ajili ya uchunguzi huu kwa kuzibainisha sifa za usemezano zinazodhihirika katika nyimbo hizo. Uchanganuzi wa nyimbo zilizoteuliwa ulifanywa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya usemezano

# SURA YA NNE

# SIFA ZA USEMEZANO KATIKA NYIMBO ZA AMANI

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tulichunguza sifa za usemezano zinazopatikana katika nyimbo za amani kutoka jamii tatu za Kenya ambazo ni Kipsigis, Kisii na Luo. Kwa kufanya hivyo, tumeshughulikia malengo mahususi kwenye utafiti wetu. Kwanza, tumethibitisha kwamba usemezano katika nyimbo za amani huathiriwa na muktadha wa kijamii. Muktadha uliohusishwa katika uchunguzi wetu ni ule wa ghasia zilizoathiri jamii zenyewe. Hali kadhalika tulifafanua dhana ya shani kama inavyojitokeza katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu teule za Kenya. Hatimaye, nyimbo za amani zilibainishwa kama kauli ambazo zinajibu na kutarajia majibu kuhusu amani. Tulizingatia nyimbo za watunzi mbalimbali kutoka jamii tatu teule katika uchunguzi wetu. Tuliteuwa nyimbo ishirini kisha tukazihakiki kwa kuzingatia vipengele vya nadharia ya usemezano vilivyokidhi mahitaji ya utafiti huu.

## 4.1 Athari za muktadha na mazingira ya utunzi na uimbaji wa nyimbo za amani miongoni mwa jamii za Wakipsigis, Wakisii na Waluo

Mukarovsky (1977) akitoa sifa za usemezano, anasema kwamba kuna mahusiano ya washiriki wa mazungumzo na mazingira waliyomo. Mazingira haya huathiri moja kwa moja mwelekeo wa mazungumzo, na pia kuathiri mazungumzo wakati mazingira yanapokuwa maudhui ya mazungumzo. Hali kadhalika, kuna uhusiano kati ya muktadha na usemezano. Muktadha hufafanua taratibu na maana ambazo hubainishwa kwa urejelezi tofauti katika mazungumzo.

Bakhtin (1978,1981,1984,1990) anasema kwamba kazi za fasihi lazima itilie mkazo muktadha maalum wa kihistoria na kijamii. Ni katika mtazamo huu ndipo tulichunguza muktadha wa utunzi na uimbaji wa nyimbo za amani. Muktadha unaoathiri nyimbo za amani ni ule wa kisiasa ambao ulitokana na matokeo ya uchaguzi wa taifa la Kenya yaliyozozaniwa. Wagombea kiti cha urais wa Kenya walikuwa tisa wakiongozwa na aliyekuwa rais wa wakati huo Mwai Kibaki wa chama cha PNU na mpinzani wake wa karibu akiwa Raila Odinga wa chama cha ODM. Ripoti nyingi za matokeo zilidhihirisha kwamba chama cha ODM kilikuwa kikiongoza katika kura hizo. Licha ya kwamba matokeo yalionyesha kuwa Raila alikuwa mbele, tume ya uchaguzi (ECK) ilimtangaza Mwai Kibaki kuwa mshindi. Kibaki aliapishwa haraka haraka ingawa wachunzaji wengi wa uchaguzi wenyewe walikuwa wametoa uamuzi kwamba uchaguzi huo ulikumbwa na udanganyifu hivyo haungeaminika. Hatua ya kuapishwa kwa Kibaki kuwa rais kwa kipindi kingine ilipokelewa na wafuasi wa chama pinzani cha ODM kwa ghadhabu.

Ghasia zilizuka katika sehemu nyingi nchini Kenya na kusababisha uharibifu mkubwa wa mali na uhamishaji wa watu. Watu zaidi ya elfu moja walipoteza maisha na takriban laki nne kupoteza makazi yao. Athari za matokeo hayo ya uchaguzi wa mwaka 2007 zilifikia eneo la jamii za Kipsigis, Kisii na Luo ambazo ni majirani. Jamii ya Kipsigis na Luo zilikuwa zikiunga mkono chama cha ODM nayo jamii ya Kisii ikifuata PNU. Vita vilianza mara moja kati ya Wakipsigis na Wakisii ambapo watu wengi walipata hasara isiyomithilika. Kwa upande mwingine jamii ya Luo pia iliwashambulia Wakisii waliokuwa wakiishi miongoni mwao.

Usuli wa kudorora kwa uhusiano miongoni mwa jamii hizi tatu ni kwamba wanasiasa tayari walikuwa wamekuza mbegu za chuki za kikabila miongoni mwao. Maudhui yanayodhihirika katika nyimbo tulizoziteua yamekitwa katika matukio yaliyoshuhudiwa pindi tu tangazo la mshindi wa urais lilipowafikia wananchi.

Mwinjilisti Philip Rono katika wimbo *Ya Boriet* (Vita ni Vibaya), amejenga taswira dhahiri kuhusu matukio ya tarehe 29/12/2007. Tarehe inayorejelewa ilikuwa siku ambayo Mwai Kibaki alitangazwa mshindi na kisha kuapishwa kuwa rais kwa kipindi cha pili. Taswira inajengwa kupitia sauti ya king'ora mwanzoni mwa wimbo huu. King'ora ni cha gari la polisi lililokuwa likijaribu kukabiliana na raia waliokuwa wakitekeleza vitendo vya uharibifu. Mbali na hayo, milio ya risasi pamoja na kamsa zinaambatana na ile ya king'ora. Tukio hili lilirekodiwa mjini Kericho katika mtaa wa *Nyagacho* ambako Wakisii wengi waliishi na kumiliki mali zao. Wakikuyu nao hawakusazwa katika mashambulizi kutokana na msimamo wao wa kisiasa.

Mwimbaji huyu aliimba kwamba alishuhudia vita ambavyo hakuwa ameviona hapo awali. Anavilinganisha na vile vya Rwanda, Burundi na Somalia.

Wimbo *Ya boriet* katika ubeti wa pili unasimulia hali ilivyokuwa katika mazingira hayo ya ghasia:

**Mf. 1**

| | |
|---|---|
| *Kichei boriet wei, ne kitom agere* | Sijawahi kushuhudia vita jinsi ile |
| *Kibek biik we* | Watu walipoteza maisha |
| *Che matinye leelut* | Wasiokuwa na hatia |

(Kutoka: *Ya Boriet.* Msanii: Mwinjilisti Philip Rono)

Katika wimbo huu, mwimbaji anasemeza namna ambavyo vita vilisababisha watu wengi kupoteza maisha yao. Mazingira yanayodhihirika hapa ni yale ya vita ambapo mauaji yalitekelezwa. Usimulizi wa kisanaa kama sifa ya usemezano hali kadhalika umedhihirika katika wimbo huu. Matukio yanayosimuliwa katika wimbo huu yamewasilishwa katika nafsi ya kwanza. Mwimbaji amesimulia kisa cha kustaajabisha alichokishuhudia katika mji alimoishi wa Kericho.

Tunaona ya kwamba nafsi neni ni 'ni' lakini katika ukanusho wake 'si' (**si**jawahi), inayowakilisha nafsi ya kwanza umoja; nafsi hii ni ya msimulizi. Hii humaanisha ya kuwa mtunzi ndiye anayesimulia matukio kupitia wimbo wake.

Msimuliwa au msemewa ni mwanajamii ambaye amewakilishwa na kiambishi 'u' (**u**sije, **u**kasahau) kama inavyodhihirika katika mshororo wa kwanza ubeti wa pili wa wimbo huu:

**Mf. 2**

*Men koutun we amat in koutwon x2* tahadhari usije ukasahau, nami pia x2

(Kutoka: *Ya Boriet.* Msanii: Mwinjilisti Philip Rono)

Muktadha wa ghasia pia umemwelekeza mwimbaji kutoka jamii ya Wakisii Bwana Ong'eng'o, kuangazia mikasa iliyoandamana na ghasia za baada ya uchaguzi. Katika wimbo wake *Omorembe* (Amani) mwimbaji huyu analilia amani. Bwana Ong'eng'o anasimulia hali ilivyokuwa wakati wa ghasia hizo. Suala la mazingira na muktadha linadhihirika katika usimulizi huu wa Ong'eng'o. Ameonyesha jinsi ambavyo watu wangeweza kufa njaa kutokana na uhaba wa chakula uliosababishwa na usafirishaji wa bidhaa. Mtu hata awe na pesa hangeweza kununua chochote hivyo kukumbwa na balaa tupu. Usimulizi wake pia unaangazia tukio ambalo watu walipika chakula vizuri lakini wakakosa kukila. Baada ya kukiandaa chakula hicho, nduru ilisikika ambapo walilazimika kukimbilia usalama. Hali hii hakika ilidhihirika miongoni mwa jamii zilizoathirika katika ghasia husika. Vita hivyo havikupangwa kwa hivyo jamaa nyingi zilishambuliwa bila habari. Fauka ya hayo, mwimbaji huyu adokeza kuhusu watu wa jamii yake ya Wakisii kulazimika kuwa wakimbizi wakaishi katika hema. Wimbo huu uliimbwa kwa Kiswahili.Wimbo *Omorembe* katika ubeti wa tatu unasema:

**Mf. 3**

*Tunapika vizuri kuweka mezani x2*

*Baada ya maombi tunasikia nduru x2*

*Uuu amani, tunaomba amani x2*

*Tunaacha chakula kukimbilia usalama*

*Bila amani hatuna maisha x2*

*Nikiingiza mkono mfukoni, iko pesa hakuna cha kununua x2*

(Kutoka: *Omorembe*. Msanii: Ong'eng'o)

Katika wimbo huu hapa, mwimbaji amejitia uhusika katika mazingira yenyewe. Kwa kufanya hivi, msanii amefaulu kusemeza hekaheka zilizoshuhudiwa wakati huo wa ghasia. Mbali na hayo, Bwana Ong'eng'o amedhihihirisha dhiki zilizoambatana na taharuki za kivita ambapo walikosa bidhaa za kununua japo pesa walikuwa nazo mifukoni. Kauli hii inadhihirisha namna shughuli za kawaida kama vile biashara zilitatizika.

Utunzi na uimbaji wa wimbo *Omokimbizi* (Mkimbizi) ulioimbwa na Bwana Segero umeathiriwa na mazingira na muktadha katika jamii yake ya Wakisii. Anasemeza tukio la kusikitisha lililohusu mauaji ya kikatili dhidi ya jamii ya Wakisii. Bwana Segero anasimulia jinsi wanaume walivyopigwa na kukatwa vichwani kwa panga. Isitoshe, mali zao kama vile nyumba na magari ziliteketezwa kwa moto. Katika ubeti wa tatu wa wimbo *Omokimbizi,* msanii anasema:

**Mf. 4**

| | |
|---|---|
| *abasacha nigo bare goitwa babutorwa* | wanaume walikuwa wakipigwa na kukatwa |
| *emetwe chinyomba bagosambwa* | vichwa na nyumba zao kuteketezwa |
| *naboigo ne chigari x2* | pamoja na magari yao x2 |
| *amabati batogora netugo yosi baira* | mabati yaling'olewa na mali kuporwa |
| *abamama bwanyumwa koreche* | wanawake walibakwa |
| *Sagero tiga ikuane na umunuone* | Segero wacha nitamke kwa kinywa |

(Kutoka: Omokimbizi. Msanii: Bw. Segero)

Hapa mwimbaji anasimulia matukio kwa nafsi ya kwanza akiwa ameyashuhudia mwenyewe yakitekelezwa na wahuni kutoka kabila hasidi. Mbali na uharibifu wa mali na maisha, uporaji wa bidhaa zenye thamani ulitekelezwa. Mabati yaling'olewa kwenye nyumba zilizoezekwa kwayo. Matendo mengine ya kikatili yaliyotajwa pia yalihusu ubakaji wa wanawake.

Muktadha wa ghasia pia umepata kushughulikiwa kupitia wimbo *Dunia* ulioimbwa na kwaya ya *Borangi PAG* kutoka jamii ya Wakisii. Watunzi na waimbaji wa wimbo *Dunia* wanasimulia mikasa iliyowapata wahasiriwa wa ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007 nchini Kenya. Swali linalokaririwa kwenye wimbo huu ni kwa nini watu hupigana bure kila kunapofika mwaka wa uchaguzi. Mateso yaliyowapata wanawake kwa watoto msituni yameangaziwa. Tukio ambalo kanisa moja mjini Eldoret liliteketezwa limesimuliwa. Kisa hicho kilisababisha vifo vya wakimbizi hao waliokuwemo kanisani.

Katika ubeti wa pili wa wimbo *Dunia* hali halisi iliyotawala jamii imeelezwa hivi:

**Mf. 5**

***Kila*** *tunapofika uchaguzi*

*Mbona twapigana bure?*

*Tukumbukeni mateso tuliyopata wakati wa uchaguzi 2007*

*Hata wake na watoto waliteseka pale msituni yooyoo x2*

*Wengine walichomwa kanisani,*

(Kutoka: *Dunia*. Msanii: Borangi PAG choir)

Katika wimbo huu, mwimbaji anasemeza hadhira yake juu ya muktadha tatanishi uliosababishwa na michafuko iliyozuka kutokana na tofauti za kisiasa. Neno *'kila'* mwanzoni mwa ubeti wa kwanza wa wimbo limetumika kama urejelezi wa kisemezano. Kama asemavyo Morson (1989), wazo kuu la Bakhtin ni kwamba watu katu hawatamki neno la mwisho bali hutamka lile la pili kutoka mwisho. Hii ni kwa kuwa ubinadamu unajulikana kwa 'kutokwisha' kwake (1986:vii). Hili ni kwa sababu kila tamko ni jibu la tamko lingine na katika mfuatano huu huu wa majibu ndio kutomalizika kwa matamshi kwapatikana. Wimbo *Dunia* umetumia neno *'kila'* kurejelea ghasia zilizowahi kushuhudiwa nyakati zilizopita katika chaguzi *za miaka ya* 1992, 1997 na 2002.

Kwa mujibu wa Bakhtin, kila tamshi huwasilishwa kupitia sauti kadhaa ndani ya tamko moja. Uwepo wa sauti hizi (polifoni) huwa msingi unaodhibiti maana katika kila tamshi. Polifoni inarejelea uwezo wa tamko moja kubeba chembechembe za tamko la mtu mwingine hivyo kuibua uhusiano wa kiusemezano baina ya sauti mbili. Mhubiri Joel Kimeto alitoa albamu kwa heshima ya Wakenya zaidi ya elfu moja waliopoteza maisha, mali na kufurushwa kutoka makazi yao kutokana na ghasia baada ya uchaguzi wa 2007/2008. Maudhui ya nyimbo zenyewe yanawalenga Wakenya wote wakiwemo wanasiasa ambao walihitajika kuhubiri amani, mapenzi na maridhiano. Wimbo wa Mhubiri Kimetto wa *Sigiriet* (punda) unajibu kauli za wanasiasa wanaopalilia uhasama miongoni mwa wanajamii. Wimbo wenyewe unasimulia kisa kutoka bibilia ambapo Nabii Balaamu alimchapa punda ambaye alikuwa amekaidi kuendelea na safari kwa kuwa alikuwa amemwona malaika akiwa ameushika upanga mkononi mwake tayari

kuwaangamiza.. Wimbo wa *Sigiriet* unasimulia tukio lililohusisha Balaamu na Balaki na makubaliano yao juu ya taifa la Waisraeli lililokuwa limekiuka maadili yaliyokuwa yamewekwa na Mungu wao. Kisa hiki kimerekodiwa katika Bibilia takatifu (Hesabu sura ya 22). Mtunzi na mwimbaji huyu ametumia mhusika 'punda' kumwakilisha mwanachi mtawaliwa, na 'Balaamu' kuwakilisha viongozi. Punda alisimama njiani na kukataa kusonga mbele katika safari ya kuelekea nchi ya Israel. Tukio hili lilimghadhabisha Nabii Balaamu ambaye aliamua kumcharaza punda viboko vikali. Vichapo hivyo vikali vilimfanya punda kunena kama anenavyo binadamu, akimlalamikia bwana wake kwa kipigo alichompa ilhali hakuwa na kosa lolote. Kisa hiki kinaashiria hali ambayo viongozi wa nchi hutekeleza wajibu wao vibaya kwa kuwaelekeza wananchi kwenye maangamizi yaletwayo na vita vya kikabila.

Mwimbaji anasema katika ubeti wa nne wa wimbo wa *Sigiriet*:

**Mf.6**

| | |
|---|---|
| *Kigeigei sigirok en kandoikyok* | Tumekuwa punda kwa viongozi wetu |
| *Kigoget Kenya kotokyi ole mi rotwet* | Wameendesha Kenya yetu kwenye upanga |
| *Mageere kamanuut en che indoochin* | Hawawathamini wanaowaongoza |

(Kutoka: *Sigiriet*. Msanii: Mhubiri Joel Kimeto)

Kutokana na wimbo huu , inadhihirika kwamba kipengele cha mwingilianomatini kimehusishwa. Hii ni kwa sababu matukio ya bibilia yameingizwa katika matini ya kuwaelekeza wanajamii kuwa macho ili waweze kung'amua mbinu za kijanja zinazotumiwa na viongozi ili waweze kuyatimiza matakwa yao ya kisiasa. Mwanasiasa amelaumiwa hapa kuwa ndiye kiini cha

sitofahamu katika jamii. Kwa kuangazia mbinu zao potovu, mwimbaji anaishauri jamii dhidi ya kutumiwa vibaya na kwamba wakati wa *'punda'* kukataa *'safari'* hii ya maangamizi umefika.

Bwana Segero katika wimbo *Omorembe Toiyo* (Hakuna Amani) amedhihirisha jinsi ambavyo wanajamii wamegonganishwa na wanasiasa kiasi cha kushindwa kueleza haswa ni nani aliyeanzisha ghasia hizo. Kilichosalia kilikuwa lawama zilizoelekezwa kwa makabila mengine. Ubeti wa tatu wa wimbo *Omorembe Toiyo* unasema:

**Mf. 7**

| | |
|---|---|
| *Gikobararia Abasigisi butebia na* | nikiwauliza Wakipsigis wananiambia |
| *Abagusii bakorwani* | wanasema ni Wakisii wanawapiga |
| *Gikobararia Abagusii butebia na* | nikiwauliza Wakisii wananiambia |
| *Abasigisi bakorwani* | wanasema Wakipsigis wanawapiga |

(Kutoka: *Omorembe Toiyo*. Msanii: Bw. Segero)

Wimbo huu umedhihirisha kipengele cha majibizano ambapo vikundi viwili vinabadilishana usemi. Bakhtin (1981, 1984) ameishughulikia dhana ya majibizano kama inavyojitokeza katika utanzu wa riwaya kama ilivotumiwa na mwasisi huyu. Mwimbaji hapa ameangazia namna ambavyo jamii za Wakipsigis na Wakisii wanajibizana kwa kulaumiana juu ya ni nani aliyeanzisha mapigano kati yao.

### 4.2.0 Kuathiriana katika nyimbo za amani

Kauli ni mwangwi wa kauli nyingine. Katika kufahamu kauli  ya pili, lazima ya kwanza ijulikane vizuri. Katika usemezano, matini mbalimbali huweza kuathiriana na kuhusiana (Bakhtin, 1981). Uhusiano huu unadhihirika pale ambapo matini zile hutajwa wazi au kutumiwa ili kufafanua mawazo zaidi. Sifa hii hujitokeza pale ambapo mwimbaji anataka maudhui fulani yaeleweke vyema zaidi. Katika kufafanua zaidi maudhui yake, mtunzi huweza kutumia matini zingine kama vile za kihistoria, kidini, kifasihi na kadhalika katika wimbo wake. Aidha, huathiriwa na matini zingine kwa njia moja au nyingine hivyo kumfanya azitaje matini hizo katika uwasilishaji wa maudhui yake. Kwa hivyo, kipengele cha mwingilianomatini ambacho ni cha usemezano kimeshirikishwa katika nyimbo ili kufanikisha mawasiliano mwafaka.

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981), hakuna mtu yeyote anayetoa tamko halafu akajigamba kuwa yeye ndiye wa kwanza kulisema. Adamu ndiye wa kwanza kutumia maneno, kwani yeye ndiye wa kwanza kufunzwa maneno (Bakhtin, 1981). Kwa hivyo hakuna atamkaye neno ila ameathiriwa na huenda akalipinga, akalitolea rai, akalipunguza au kuliongezea maana. Kutokana na mtazamo huu, tulichunguza uathiriano katika nyimbo za amani kama mojawapo ya sifa za usemezano katika utanzu huu.

### 4.2.1  Athari za sajili katika nyimbo za amani

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), sajili ni dhana inayotumiwa kueleza sifa za kilugha zinazofungamana na kudhibitiwa na muktadha maalum. Lugha hiyo inaweza kuwa ya kimaandishi au kimaongezi. Lugha inayotumiwa katika muktadha fulani huwa na sifa kadha

zinazobainishwa na muktadha wake. Uteuzi wake wa kimsamiati, sarufi, uakifishi, kiimbo na sauti huathiriwa na matarajio fulani ya kimuktadha.

Bakhtin (1981) anaeleza kwamba sajili mbalimbali hutumiwa ili kuweza kupatikana usemezano katika matini. Aidha, Bakhtin (1986) anasema kwamba sajili ni lugha ambayo huzoeleka kutumiwa katika mawanda fulani hadi matamshi hayo yakajiimarisha katika mawanda mahususi. Jambo hili hutokea kwa sababu amali anazofanya mwanadamu humwathiri na hata matamshi nayo huathirika katika lugha ambayo anaitumia. Matamshi haya huonyesha malengo yake kutokana na maudhui, mitindo ya kiisimu na mtindo wa kuyatunga matamshi yenyewe.

Kila neno huwa pekee yake, lakini kila lugha huweza kueleweka katika muktadha fulani maalum. Hii ndiyo iitwayo sajili. Bakhtin (1986) anasema kwamba maana imefungika katika muktadha, na matamshi hayakufungika. Kutofungika huko kwa matamshi anakuita ndimi za usemi. Ndimi hizi hutokea kwa sababu katika wakati fulani, mahali fulani, kuna nguvu fulani ambazo zitalipa neno lililotamkwa maana hapo hapo. Neno hili wakati mwingine na pahali pengine litakuwa na maana tofauti. Kauli hizi za Bakhtin zililipa mwongozo lengo la utafiti huu la kubainisha sifa za usemezano katika nyimbo za amani, hususan sifa ya matumizi ya sajili. Sajili kama mojawapo ya sifa za usemezano imetumika kufanikisha uendelezaji wa amali za kijamii.

#### 4.2.1.1 Sajili ya dini

Sajili ya dini hupatikana katika vitabu vya dini, kama vile Biblia na Korani, vitabu vya mafunzo na masimulizi ya kidini, ibada, mahubiri na mijadala ya kidini. Msamiati wa kawaida unawakilisha maana za kidini zinazofasili uhusiano bora wa watu na Mungu au miungu kwa upande mmoja na uhusiano adilifu wa waumini wenyewe. Sajili ya dini hutumika sana katika nyimbo za amani. Hali hii inatokana na sababu ya kwamba mafundisho mengi ya kidini yameelekezwa katika haja ya utangamano wa kijamii. Kwa mujibu wa Crystal na Davy (1969), sajili ya dini huwa na sifa zifuatazo: msamiati wa kikale kutumiwa, baadhi ya maelezo kuzingatia maneno ya utamaduni, marudio na mara nyingi maneno kudondolewa kama vifungu, sentensi ndefu ndefu kutumiwa pamoja na viunganishi vingi, kuwepo kwa matumizi ya mafumbo, methali, kufuata kaida maalumu katika mianzo na mwisho wa usemi na kutumia sauti ya kuvutia au ya kusihi.

Aidha, sajili ya dini kama anavyosema Ndung'u (2001), huwa na sifa kama vile kuchanganya msimbo, mshikamano wa kimsamiati, urejeshi, uunganishi, ubadilishanaji na udondoshi, matumizi ya ishara, maswali ya balagha, matumizi ya visa na matukio ili kurahisisha kueleweka kwa ujumbe.

Imani katika dini ya kikristo imekita mizizi miongoni mwa jamii tatu zilizoshirikishwa katika uchunguzi wetu. Utunzi na uimbaji wa nyimbo za amani umeathiriwa na imani ya dini hii ya Kikristo. Maudhui mengi yameoanishwa na matukio yapatikanayo katika Bibilia takatifu.

Kinachodhihirika kwa kiwango kikubwa ni unukuzi wa vifungu vingi kutoka maandiko kwenye Bibilia.

Nyimbo nyingi zilizokusanywa zinarejelea maandiko katika Bibilia. Wakristo hushikilia kwamba imani yao inafaa iwaelekeze wawe watu watakaochangia kuleta haki na amani katika jamii. Aidha, mafundisho ya Yesu Kristo yalijikita katika haja ya kuhubiri amani, mapenzi na maridhiano.

Wimbo *Lazaro* ulioimbwa na Mhubiri Kimetto, unasimulia kisa kinachopatikana kwenye Bibilia kuhusu rafiki ya Yesu aitwaye Lazaro. Lazaro huyo aliugua na kuaga dunia kisha akazikwa. Yesu alipopokea habari kuhusu mauti hayo, alihuzunika mno na akaamua kuitembelea jamaa hiyo. Martha, dada yake marehemu alimpokea Yesu kwa kilio kikuu akimwambia kwamba angekuwepo (Yesu), Lazaro asingeaga dunia. Sababu ya kusema vile ni kwamba Martha alifahamu fika kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kuzuia mauko ya kaka yake Lazaro

Kimetto anaonyesha usambamba wa kimaana kwa kulitumia tukio lile katika hali iliyoikumba nchi yetu na hususan eneo linalohusishwa katika uchunguzi huu. Ghasia zile zimelinganishwa na mauti yaliyompata Lazaro na msiba uliokumba jamaa yake kutokana na mauti hayo. Wimbo huu unashikilia kwamba aliko Yesu, kuna ufanisi wa kila namna. Katika ubeti wa sita wimbo unadhihirisha kauli hii:

**Mf. 8**

| | |
|---|---|
| *Ndo kimi Jesu Kenya inyon* | kama Yesu angekuwa Kenya yetu |
| *Ta kima kitumdo korotik* | damu haingemwagika |
| *Nda kimi Jesu kwenunyon* | Yesu angekuwa miongoni mwetu |
| *Ko ta kimenye en kalyet* | tungekuwa tunaishi kwa amani |

(Kutoka: *Lazaro.* Msanii: Mhubiri Joel Kimeto)

Kutokana na ubeti huu wa wimbo matini iliyotolewa kutoka Bibilia imetumika. Mwimbaji amerejelea kisa hiki kwa kusudi la kusemezana na hadhira yake juu ya kumwamini Yesu ambaye ndiye kiini cha amani katika maisha. Aidha ametoa ushauri kwa wanajamii kukuza uhusiano mwema uliojengwa kwa uaminifu miongoni mwao.

Sifa zaidi za sajili ya dini zinadhihirika katika wimbo *Dunia* ulioimbwa na kwaya ya Borangi PAG. Wimbo huu umerejelea mafudisho ya Kikristo yapatikanayo katika Bibilia. Katika ubeti wa tatu wa wimbo huu, mwimbaji amemsawiri Yesu kuwa mwenye upendo wa ajabu na kwamba amani hupatikana kwake. Wimbo huu huwaelekeza wanajamii kuamini kuwa Yesu ana uwezo kuwapa amani na upendo wa kweli na wa kudumu. Katika ubeti wa tatu wa wimbo *Dunia* ujumbe huu umedhihirika:

**Mf.9**

*Tangaza **agape***

*Upendo wa Yesu wa ajabu*

*Amani tutapata kwa Yesu tutapata*

(Kutoka: *Dunia*. Msanii: PAG Borangi Choir)

Katika ubeti huu, neno ***agape*** lenye asili yake katika Kigiriki humaanisha mapenzi kati ya binadamu na Mungu wake. Ni mapenzi ya kikristo yanayoambatana na kule kuyajali masilahi ya binadamu mwenzako. Mwimbaji hapa anawahimiza wananchi waweze kuiga ule upendo wa Yesu. Msamiati uliotumika hususan ni ule unaoambatana na dini ya Kikristo. Maneno kama vile maombi, upendo wa Yesu na amani ipatikanayo kwa Yesu, ni lugha inayofungamana na mafudisho ya dini hii.

Aidha, wimbo *Sigiriet* (Punda) uliotungwa na kuimbwa na Mhubiri Joel Kimeto, umedhihirisha sifa za sajili ya dini. Wimbo *Sigiriet* unawakosoa wanasiasa wanaopalilia uhasama miongoni mwa wanajamii. Wimbo wenyewe unasimulia kisa kutoka bibilia ambapo Nabii Balaamu alimchapa punda ambaye alikuwa amekaidi kuendelea na safari kwa kuwa alikuwa amemwona malaika akiwa ameushika upanga mkononi mwake, tayari kuwaangamiza. Katika ubeti wa pili wa wimbo *Sigiriet*, wimbo unaeleza:

**Mf.10**

*Kigaguur laitoriat Baalam kochup Israel*  Mfalme alimwagiza Balaamu alaani Israeli

| | |
|---|---|
| *Soman en sirutik Koitosiek 22 x2* | Soma andiko katika Hesabu 22 x2 |
| *Kigaguur laitoriat Baalam kochup Israel* | Mfalme alimwagiza Balaamu alaani Israeli |
| *Kiyomisyi tuguk che eechen* | Alimwagizia mambo muhimu makuu |

(Kutoka: *Sigiriet* (Punda). Msanii: Mhubiri Joel Kimeto)

Kutokana na ubeti huu, kifungu cha Biblia cha Hesabu 22 kimenukuliwa. Hii ni sifa mojawapo katika sajili ya dini. Isitoshe, Balaam aliyetajwa alikuwa nabii katika enzi ya mfalme wa taifa la Israeli kama ilivyorekodiwa katika Bibilia. Majukumu ya manabii wa wakati huo yalihusu kuielekeza jamii pamoja na kutangaza adhabu kwa waliokiuka maadili. Adhabu mojawapo ilishirikisha laana kama ilivyotajwa katika ubeti huu hapo juu.

Isitoshe, wimbo *Ukabila* ulioimbwa na Bwana Silas Omondi unadhihirisha sifa muhimu katika sajili ya dini. Wimbo *Ukabila* ulichochewa na haja ya kuishauri jamii ya Kenya kujiepusha na siasa za kikabila hususan baada ya ghasia zilizozuka baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 nchini Kenya. Tume ya haki za kibinadamu nchini Kenya (KHRC), siasa za Kenya zimekuwa na tabia ya mivutano ya kikabila tangu uhuru mnamo 1963. Lakini haikuwa hadi 2007 ambapo mapigano kati ya makabila yalizuka. Tatizo hutukia wakati ambapo wanasiasa hutumia ukabila kwa masilahi yao ya kibinafsi na kuunda mgawanyiko ambao huzalisha ukabila. Katika ubeti wa kwanza wa wimbo *Ukabila*, msanii anasema:

**Mf.11**

*Ee Mungu wangu ninakupenda mimi x2*

*Umeniponya umenilinda Baba*

*Umetuponya umetulinda Kenya*

*Umebariki taifa letu Kenya*

*Taifa zuri, taifa lenye upendo*

*Umetuponya umetulinda Kenya*

*Aa aa halleluya x2*

(Kutoka: *Ukabila*. Msanii: Bwana Silas Omondi)

Kutokana na ubeti huu wa wimbo *Ukabila*, tunaona sifa ya sajili ya dini ya kutumia lugha inayomtolea Mwenyezi Mungu sifa na kumtukuza. Mungu amesawiriwa kuwa mwenye uwezo mkubwa katika kuiponya na kuilinda jamii ya Kenya mbali na kuipenda. Aidha neno *halleluyia* hutumiwa aghalabu kudhihirisha kiwango cha juu katika kumtukuza Mwenyezi Mungu.

#### 4.2.1.2 Sajili ya mtaani /vijana

Nyimbo za amani zimeathiriwa na matumizi ya sajili ya vijana. Sifa kuu katika lugha ya vijana ni mabadiliko na uchanganishaji msimbo. Watumiaji huteuwa msamiati mahususi pamoja na sarufi inayowafaa katika mawasiliano yao wenyewe kwa wenyewe. Kwa mujibu wa wanaisimu, kuna miundo miwili ya lugha katika isimujamii. Moja ni muundo wa kubadili msimbo na wa pili ni muundo wa kuchanganya msimbo. Weinrech (1953), aliyenukuliwa na Naseh (1997:202) anadai kwamba ubadilishanaji msimbo hutokea katika mazingira ya mazungumzo pale ‘watu wenye zaidi ya lugha moja’ wanapobadili msimbo kutoka lugha moja kwenda nyingine.

Maneno ya lugha ya Kiingereza yametumiwa katika nyimbo za amani ili kupitisha ujumbe maalumu. Maneno yenyewe yametumiwa kimakusudi kwa sababu vijana ndio walengwa, nao pia walishirikishwa katika michafuko ya baada ya uchaguzi wa kitaifa wa 2007. Isitoshe, lugha hii imehusishwa na utandawazi, yaani ulimwengu mzima waweza kuwasiliana kwayo. Nyimbo hukiuka mipaka na kutumika nje ya maeneo husika katika utafiti huu.

Lugha ya*'sheng'* ambayo hutumiwa kwa kiwango kikubwa na vijana imeibuka kutoka kwa Kiswahili na Kiingereza. Ghasia nyingi katika jamii huwashirikisha vijana kwa kuwa ni wepesi na wenye nguvu. Mbali na hayo, vijana wengi hawana ajira hivyo viongozi huwatumia vibaya kwa ajili ya masilahi yao maovu ya kibinafsi.

Katika ubeti wa nne (4) wa wimbo *Haki* uliotungwa na kuimbwa na Bwana Nyakundi, sifa za sajili ya vijana zinadhihirika. Ubeti huu umesheheni matumizi ya uhamishaji wa msimbo kwa kiwango cha juu.

**Mf. 12**

***Confessions in*** Kenya kuhusu ***conflict in***Kenya

***Justice delayed is justice denied***

***Let the wrong be charged***

Umoja bila haki, ni uongo

Uongo, ***corruption,*** porojo, ***impunity*** kando

***Solidarity***, juu ya ***maboundaries, on point***

(Kutoka: Haki. Msanii: Bw. Nyakundi)

Lugha iliyotumika hapo juu hueleweka kwa vijana kwani wana uzoevu wa kushirikisha uhamishaji msimbo katika mazungumzo yao ya kila siku. Kuchanganya msimbo hudhihirika katika kule kutumia lugha mbili tofauti katika neno moja. Katika utaratibu huu, baadhi ya maneno yameambishwa viambishi kama vile vya nafsi na ngeli. Mfano muafaka huonekana katika ubeti wa pili (2) wa wimbo *Ni Amani*. Mtunzi na mwimbaji wa wimbo husika ameshirikisha sifa hii kwa mapana na marefu kote kote katika wimbo wake.

**Mf.13**

Ndo maana tuko hapa tuna***preach*** hiyo ***justice***

Ma***blunder*** kibao ni kama twacheza na ***dice***

Bila ma***acomplice*** vipi wange***acomplish*** za ***ill motive***

(Kutoka: *Ni Amani*. Msanii: Bwana Nyakundi)

Kutokana na mshororo wa kwanza, neno tuna*preach* lina mzizi *preach* (hubiri) likiambishwa viambishi awali *tu*- na *–na*-. Maneno mengine ma*blunder*, ma*acomplish* na wangeacomplish vivyo hivyo yamefuata mfumo uo huo wa uambishaji.

#### 4.2.1.3 Sajili ya Siasa

Siasa ni njia ya kufanya maamuzi katika taifa, mji au hata kimataifa. Sehemu muhimu ya siasa ni majadiliano kati ya watu mbalimbali wenye nguvu au mamlaka. Katika demokrasia, kila mtu ana kiasi fulani ya nguvu, kwa hivyo siasa ya demokrasia ina maana ya watu wote kuchangia maamuzi.

Sajili ya siasa imedhihirika katika nyimbo za amani. Watunzi na waimbaji mbalimbali wametumia lugha ya kisiasa kuyafafanua maudhui yao ya kuwapatanisha wanajamii. Baadhi ya sifa za sajili hii ni kama vile kutumia msamiati

Lugha ya kisiasa imetumika katika wimbo wa Onyango Papa J wa *Mapatano*. Wimbo huu ulitungwa wakati wa ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 nchini Kenya. Mzozo uliozuka ulisababisha mauaji ya waandamanaji wengi kule Kisumu na miji mingine nchini Kenya. Umoja wa Mataifa uliingilia kati ili kutafuta suluhisho la kudumu la kisiasa. Washauri chini ya uongozi wa aliyekuwa katibu wa Umoja wa Mataifa (UN), Koffi Annan walifika nchini Kenya katika upeo wa ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007. Washiriki wenza walikuwa Rais Jakaya Kikwete wa Tanzania, Bi. Graca Machel na Bi. Condoleeza Rice, aliyekuwa katibu katika utawala wa rais George Bush kule Marekani. Madhumuni ya washauri hao yalikuwa kuujenga uwiano kati ya viongozi waliokuwa wakizozania hatamu za uongozi. Kwa kuwa mzozo wenyewe ulikuwa wa kisiasa, basi suluhisho lilikuwa liwe la kisiasa. Juhudi za washauri hao zilibuni serikali ya muungano iliyowaweka pamoja mahasidi wakuu wa kisiasa, yaani Mwai Kibaki na Raila Odinga. Katika ubeti wa tano wa wimbo *Mapatano:*

**Mf. 14**

*Baada ya mapatano tulienda bungeni x2*

*Wabunge wote waliapishwa usiku x2*

*Anyang Nyong'o aliapishwa usiku*

*Martha Karua aliapishwa usiku*

*Wetangula aliapishwa usiku*

*Omingo Magara aliapishwa usiku*

*Amolo Odinga aliapishwa usiku*

(Kutoka : *Mapatano*. Msanii: Onyi Papa J.)

Mwimbaji anatumia msamiati wa kisiasa kama vile *bunge* na *kuapishwa.* Bunge ni baraza la taifa la kutunga sheria linaloundwa na wajumbe waliochaguliwa na wananchi. Tukio la kuapishwa kwa wabunge huwa hatua inayowahalalisha waanze shughuli zao bungeni. Majina ya wabunge maarufu yametajwa.

Katika ubeti wa tatu wa wimbo *Mapatano*, mwimbaji anasema:

***Mf 15***

*Koffi Annan alileta coalition,*

*Koffi Annan alileta mediation, x2*

(Kutoka: *Mapatano*. Msanii: Onyi Papa J)

Matumizi ya neno '*coalition'* yanarejelea (serikali ya muungano) nayo '*mediation'* ni mashauriano kati ya pande mbili hasidi za kisiasa yaliyoleta maafikiano. Pande hizo mbili zilikuwa serikali ya Rais Kibaki na upinzani Raila Odinga. Kofi Annan, aliyekuwa katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa, aliwaongoza viongozi mashuhuri wa Afrika kusuluhisha mzozo wa kisiasa nchini. Hatima yake ilikuwa kubuniwa kwa serikali ya muungano ambapo tarehe 12 Februari 2008 Kibaki na Raila walitia sahihi mkataba wa kuunda serikali ya muungano. Jina lililorejelea muungano huo lilikuwa Serikali hii ya umoja wa kitaifa. Serikali hiyo iliyokuwa na mawaziri kutoka vyama tofauti vya kisiasa, ilitarajiwa kuhudumu kutoka Aprili 2008 hadi Aprili 2013. Mwimbaji hapa amedhihirisha uathiriano wa kisiasa katika utungo wake.

Aidha, wimbo *Sigiriet* (Punda) unawasuta viongozi wa kisiasa walio na mazoea ya kuwaelekeza wananchi kwenye hatari ya migogoro kupitia uchochezi wa kiukabila. Mwimbaji amedhamiria kuwahamasisha wanajamii kubaini mbinu zinazotumiwa na wanasiasa ili kuyafikia malengo ya ya kisiasa ambayo ni kupigiwa kura tu. Aghalabu huwasahau walowachagua pindi wanapotekelezewa matakwa yao.

Ubeti wa tatu unadhihirisha lugha hii ya kisiasa:

**Mf 16**

| | |
|---|---|
| *Kigeigei sigirook en bikchok che indoiweech* | Tumekuwa punda kwa viongozi |
| *Kigokweri emenyon kotokyige ole mi rotwet* | Wameielekeza nchi kuliko upanga |
| *Magere kamanut en bikwak che indochin* | Hawawathamini wanaowaongoza |

(Kutoka: *Sigiriet*. Msanii: Mhubiri Joel Kimetto)

Wimbo huu umedhihirisha athari za sajili ya siasa ambapo mtunzi anasemeza sauti za wanasiasa na raia wanaoongozwa. Akitumia kisa cha punda, amefaulu kuasa hadhira yake itahadhari dhidi ya wanasiasa wanaoweza kuaingiza katika hatari ya maangamizi. Aidha, ameonyesha namna ambavyo viongozi wenyewe wanavyojali haja zao za kibinafsi hivyo kutothamini za wananchi waliowachagua.

Wimbo *Haki Yetu* ulioimbwa na Queen Babito, umeangazia masuala nyeti katika siasa za nchi ya Kenya. Akirejelea uchaguzi wa mwaka wa 2007, analalamikia hali ambayo matokeo ya hesabu ya kura yalicheleweshwa hivyo kuzua hali ya taharuki kote nchini. Aidha, amesema kuwa jamii ya Luo imewaunga mikono wanasiasa kutoka makabila mengine lakini pindi wao viongozi waingiapo uongozini, huwapuuza. Mwimbaji anasema kwamba Wakenya wanataka Raila apewe haki yake ya kuiongoza Kenya.

Katika ubeti wa sita wa wimbo Haki Yetu, mwimbaji anasema:

**Mf 17**

| | |
|---|---|
| *Baba koso diponi wan niketowa e piny kae mondo* | wapi imeandikwa kwamba Wajaluo |
| *wabed ngas majowetewa idho kidhi pon godo olemo* | hawawezi kuiongoza nchi nyetu? |
| *koso lajni ne ok en pokwa mondo waluera godo* | nani kasema mahali pao ni upinzani |
| *koso bed ni nisingo nilojni wabiro kawe gi remo* | lazima damu imwagike ili mjaluo |
| *Baba koso obiro bedo sand mane J.M Kariuki obede* | aongoze? J.M Kariuki, Robert Ouko |

| | |
|---|---|
| *Robert Ouko obede, Tom Mboya obede, Odhiambo Mbayi en kanyo? Argwings Kodhek nobede. Anyiso wuod Oganda niya. Baba uchalo kaka Musa, nimer nachwado nam; manyi thii Israel okedho bahati mbaya notho makoremo piny mar Kanaan* | Tom Mboya, Odhiambo Mbayi, na Argwings Kodhek wote walijitoa mhanga ili waikomboe jamii yao. Raila kama Musa ni kiongozi pekee anayeweza kutukomboa |

( Kutoka: *Haki Yetu*. Msanii: Queen Babito)

Ubeti huu unaibua hisia nzito za kisiasa hasa kwa jamii ya Luo ambayo kwa muda mrefu wamepokonywa haki zao kisiasa. Wimbo huu unajibu kauli za wale viongozi wanaotawaliwa na taasubi za kikabila kuwa hamna jamii nyingine iliyo na uwezo wa kulitawala taifa la Kenya isipokuwa mmoja wao. Goldsworthy (1982) katika kitabu *Tom Mboya: The Man Kenya wanted to forget*, anasema kwamba Tom Mboya alikuwa mwanaharakati maarufu na aliyesifika kote nchini na barani Afrika. Umaarufu huo wake pamoja na kwamba nyota yake ya kisiasa ilionekana kung'aa kila kukicha, haikuwafurahisha tabaka la viongozi wa serikali ya miaka hiyo. Hatimaye Mboya aliuawa tarehe 5 July 1969.

Kwa mujibu wa Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano (TJRC), mauaji ya Odhiambo Mbai yana usuli wa kisiasa. Mbai alisemekana kuwa mmoja wa wale walioshinikiza kujumuishwa kwa mfumo wa ugatuzi katika katiba ya Kenya. Mbai alikuwa mwenyekiti wa kamati ya ugatuzi wakati wa maandalizi ya katiba mwaka wa 2004. Viongozi waliotajwa na ambao walipoteza maisha yao kwa hali zisizofahamika, walijitolea kuitetea jamii hususan dhidi ya unyanyasaji kutoka serikali za nyakati hizo. Idadi kubwa ya waliofikwa na mauti ilitoka katika jamii moja ya Luo.

### 4.3.0 Matumizi ya Tanzu Fupi za Fasihi Simulizi.

Tanzu fupi ni kipera cha fasihi simulizi kinachojumulisha sanaa simulizi zinazoundwa kwa maneno machache: sentensi moja au mbili hivi. King'ei na Kisovi (2005) wameorodhesha tanzu fupi za fasihi simulizi zifuatavyo: methali, semi, vitendawili, mafumbo, tashbihi, tanakali za sauti, majina na majigambo. Kuna matumizi ya tanzu fupi za fasihi simulizi katika nyimbo za amani. Nyimbo nyingi za amani zimetumia methali, tashbihi, mafumbo na misemo ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), tanzu hizi zilijengwa kimafumbo kwa lengo la kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudia kwa namna ya kufikirisha hadhira hiyo katika kupata maana ya tamathali husika. Vipera hivi aghalabu hutumiwa katika kazi nyingine za fasihi (na lugha kwa jumla) kama mapambo ya lugha.

Isitoshe, washairi na walumbi hutumia tamathali za usemi kwa mapana na marefu katika nyimbo zao na ulumbi wao. Finnegan (2012) naye anafafanua kwamba lugha za kiafrika hutumia msamiati teule kwa ubunifu unaokuza taswira kwa njia ya kusisimua. Kwa ajili ya utafiti wetu, tulizichunguza tanzu mbalimbali zilizoweza kutumiwa na watunzi na waimbaji wa nyimbo ili kuyafafanulia maudhui mbalimbali. Nyimbo teule zilichunguzwa ili kudhihirisha matumizi ya tamathali mbalimbali katika tungo zilizoshirikishwa katika kazi hii.

### 4.3.1 Matumizi ya Methali

Kwa mujibu wa Matei (2011) methali ni semi fupi fupi za kimapokeo zenye kueleza fikra, maarifa, hekima na mafunzo yanayotokana na uzoevu wa jamii mahususi. Aidha, methali hutokea katika mazungumzo mazito kama vile katika kutoa mawaidha au kama kielelezo na kifupisho cha hadithi. Kwa ajili ya uchunguzi wetu, tuliangazia methali mbalimbali zilizoshirikishwa katika tungo za amani.

Wimbo *Ya Boriet* (Vita ni vibaya) umesheheni ukwasi wa matumizi ya methali. Methali *kelus ak kemee meet ne kime teret* (Kufa kifo kile kilichokikumba chungu). Msanii akirejelea mauti yaliyowakumba wanajamii katika ghasia zilizokumba nchi yetu baada ya matokeo ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 kutangazwa. Dhana ya chungu kilichovunjika inarejelea kisa ambacho mtu alikigonga chungu kikavunjika vipandevipande. Katika jamii nyingi za jadi, wanajamii walitumia vyungu kubebea na kuhifadhia maji, kupikia na shughuli nyingine za kijamii. Kwa vile chungu hufinyangwa kwa udongo, kinapoanguka huvunjika vipande na hapo huwa mwisho wake. Ni muhali kuviunganisha vigae vya chungu hadi chungu kikatumika tena. Katika jamii inayotumia vyungu pamija na vibuyu kama vifaa vya kuhifadhi vinywaji, vifaa hivi huthaminiwa sana. Hata hivyo, kibuyu kikianguka na kuvunjika, huwa rahisi kuviunganisha vipande vyake na kibuyu kikatumika tena. Kifo kinapompata mtu husemwa kwamba amekufa kifo cha chungu kilichovujika. Methali hii imetumika kudhihirisha hali ya hatari kubwa ambayo ilitisha kuwaangamiza watu wengi. Ghasia husika zilitishia kuitumbukiza nchi ya Kenya katika vita vya

ndani kwa ndani. Jamaa nyingi kutoka jamii za Kipsigis, Kisii na Luo zilipoteza wapendwa wao kutokana na ghasia zilizozuka wakati huo.

Ubeti wa pili wa wimbo *Ya Boriet* (Vita ni Vibaya) unasema:

**Mf 18**

| | |
|---|---|
| *Ko kita kibeguu ak kelus ak kemee* | Tungeangamia mautini |
| *Meet ne kime teret* | Kifo cha chungu kilichovunjika |
| *Ya boriet wei, mamiten kit ne u x2* | Vita ni vibaya, hakina kisawe x2 |

(Kutoka: *Ya Boriet*. Msanii: Mhubiri Joel Kimetto)

Methali iliyotumiwa katika wimbo huu inatilia uzito ushauri wa mwimbaji kwa msemezwa wake. Uwili wa mwelekeo katika usemezaji wa wimbo huu unadhihirika kwa namna ambavyo mwimbaji anamsimulia msikilizaji wake matukio ya msimu huo wa ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 nchini Kenya.

Wimbo wa Mhubiri Kimetto wa *Ongebir Maat Koloo* (Kinga yashinda tiba) unasimulia kisa cha bibilia cha mwanamke Mshunami ambaye alimpoteza mwanawe wa pekee lakini hakuonyesha hisia zake za simanzi. Alizificha hisia hizo ili aweze kutafuta suluhisho kutoka kwa nabii Elisha aliyemwamini angetenda muujiza wa kumfufua mtoto huyo. Vivyo hivyo katika jamii, kuna mambo fulani ambayo hayajitokezi wazi kwani wanajamii huyaficha kutoka kwa wenzao kwa sababu ambazo hazieleweki. Wanajamii wanaonekana kujiandaa kwa vita lakini bado wanajitia

kuishi kwa amani. Wanajamii, hali kadhalika, hawaonyeshi mashaka yanayowakumba kutokana na chuki miongoni mwao. Mwimbaji ametumia methali *kibire maat koloo* kuwashauri watu wasikae na kungojea kutukia kwa vita wakati dalili zote zi dhahiri kama vile kujihami na kuwepo chuki za kikabila miongoni mwa dhiki nyingine. Akirejelea matukio ya vita vilivyoshuhudiwa katika nchi za Somalia na Rwanda, anawaonya wanajamii dhidi ya kuruhusu utengano unaotokana  na tofauti za kisiasa na kikabila.

Kwa ubeti ufuatao, mwimbaji anatoa ushauri kupita methali:

**Mf 19**

| | |
|---|---|
| *Ongebir maat koloo* | Kinga yashinda tiba |
| *Onetweech Kalenjin (olenji)* | Wafunze Wakalenjin *(kwamba)* |
| *Ongebir maat koloo* | Kinga yashinda tiba |
| *Omwachi Kosobeek (olenji)* | Wajuze Wakisii *(kuwa)* |
| *Kibire maat koloo* | Kinga yashinda tiba |
| *Si maigei emenyon Rwanda* | Ili taifa letu lisiwe kama Rwanda |
| *Mongeige Somalia* | Tusije tukawa kama Somalia. |

(Kutoka: *Ongebir Maat Koloo*. Msanii: Mhubiri Joel Kimetto)

Mwimbaji anasemeza nafsi za jamii zilizozozana kwenye ghasia za baada ya uchaguzi wa kitaifa wa mwaka wa 2007. Mwimbaji ambaye ni mzaliwa wa jamii ya Kipsigis ametumia methali hii ili kupitisha ujumbe wake kwa njia isiyo ya moja kwa moja huku akizishauri jamii zilizohusika kwenye mapigano kudumisha utangamano miongoni mwao.

### 4.3.2 Matumizi ya Sitiari

Sitiari ni uhamishaji wa maana kutoka kitu kimoja au dhana moja hadi kitu kingine au dhana nyingine. Vikoa vya maana vinavyohusika katika uhamishaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa moja ya msingi wa semantiki. Kinachohamishwa ni tabia au umbo au kazi ya kitu kwa kukihusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine (Kahigi, 1995).

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), sitiari ni tamathali ya usemi ielezayo sifa za kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine. Hii ni mbinu ya kiulinganishi kama tashbihi lakini ulinganishi huo haujitokezi waziwazi. Wataalamu hawa wanaonekana kukubaliana kuwa sitiari hujengekea kwenye uhamishaji wa maana. Watunzi na waimbaji hutumia sitiari kwa kiwango kikubwa ili kufanikisha malengo yao anuwai kwenye nyimbo zao.

Katika wimbo wa Mhubiri Kimetto wa *Sigiriet* (Punda), punda ametumika kisitiari kuelezea namna ambavyo wananchi wametumika sawa na punda wa huduma. Katika jamii nyingi duniani, punda ametumiwa kutekeleza shughuli ainati hususan zinazohitaji nguvu nyingi kwa mfano ubebaji mizigo. Mmiliki punda humpeleka au kumwelekeza kokote atakako naye mnyama huyo hana budi ila kuridhia bila walakini. Sitiari ya punda imetumika kudhihirisha jinsi ambavyo wananchi (punda) wanavyotumiwa vibaya na 'wanaowamiliki' ambao ni viongozi wao. Ni

‘punda’ wao hao wanawatwisha uongozi, nao viongozi kuwatumia ‘punda’ wao hao kuyatetea ‘masilahi’ ya viongozi wenyewe.

Katika ubeti wa tatu wa wimbo Sigiriet, mwimbaji ametumiaa mbinu hii:

**Mf 20**

| | |
|---|---|
| *Kigeigei sigirook en bikchok che indoiweech* | Tumekuwa ***punda*** kwa viongozi |
| *Kigeigei sigirook en kandoikab bolatosiek* | Tumekuwa ***punda*** kwa wanasiasa |
| *Kigokweri emenyon kotokyige ole mi rotwet* | Wameielekeza nchi kuliko ***upanga*** |
| *Kigoket Kenyanyon kotokyigei ole mi rotwet* | Wameelekeza Kenya kuliko ***upanga*** |

(Kutoka: *Sigiriet.* Msanii: Mhubiri Joel Kimetto)

Katika ubeti uu huu, neno *punda* limetumika kisitiari kuwakilisha wananchi au wapiga kura ambao daima huwatii viongozi wao kwa kila njia. *Upanga* kwa upande mwingine husimamia dhana ya vita au ghasia za kikabila. Baadhi ya viongozi walituhumiwa kuwa wachochezi na wafadhili wa mapigano yaliyozuka pindi tu matangazo ya matokeo ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 nchini Kenya. Wimbo huu unasemeza wanajamii wawe na uwezo wa kutambua mbinu zinazotumiwa na wanasiasa ili kuyatimiza malengo yao ya kisiasa.

Mwimbaji Bwana Segero katika wimbo *Omokimbizi* (Mkimbizi) ametumia sitiari ili kuupitisha ujumbe wake. Segero ametumia sitiari ya arusi katika wimbo wake. Akisimulia matukio ya upigaji kura wa kitaifa uliofanywa tarehe 27 mwezi wa disemba 2007, Bwana Segero anatoa

simulizi kuhusu  arusi ya makabila yote nchini Kenya. Katika utamaduni wa Abagusi, shughuli za kuomba kura hulinganishwa na tendo la kumrai mwanamwali ambaye umemtambua ili umwoe. Kwa muktadha huu, mwanasiasa huwa bwana arusi naye mpiga kura huwa mwanamwali. Bwana Segero alisema kuwa kabila la Wakisii liliwakaribisha maarusi ambapo sherehe ilifanyika hadi tamati. Tatizo lilizuka hatimaye wakati sanduku la mwanamwali lilibwa na hivyo kuzua fujo zilizosababisha maafa makubwa. Katika beti za nne, tano na sita za wimbo Omokimbizi, Bwana Segero anasema:

**Mf 21**

| | |
|---|---|
| *Chitariki 27 Disemba 2007 bwakonte* | tarehe 27 disemba 2007 tulifanya |
| *Enyangi chikabira ange chiosi Kenya* | **arusi** ya makabila karibu yote Kenya |
| *Chiarenge ne chia chie nyangi mpaka* | yalikuwa na nguo za arusi mpaka |
| *Omogusi bwesi* | Mkisii pia |
| | |
| *Omogusii tobwati monyomba* | Mkisii hana ukabila |
| *Akageni abanyanyangi obagusi* | aliwakaribisha **maarusi** bila kubagua |
| *Etaiyo mpaka enyangi ekaera* | hadi arusi ikafikia tamati |
| | |
| *Esanduku ya moriakari ekaibwa* | **sanduku la mwanamwali** likaibwa |
| *Omogusii ogaswa goshwa* | mkisii akatolewa kafara |
| *Oyosiriwa ne nibo yaye x2* | kupigwa na kupoteza mali yake x2 |

(Kutoka: *Omokimbizi*. Msanii: Bwana Segero)

Bwana Segero katika beti hizi tatu, ametumia sitiari ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wake kwa hadhira yake. Katika ubeti wa nne, neno *arusi* limetumika kurejelea upigaji kura uliofanyika

kote chini Kenya. Arusi huwa tukio linalowaleta pamoja watu ambao kwa kawaida huwa hawana uhusiano wowote wa kinasaba, kwa hivyo hutegemea hiari ya mwenzake. Suala la kampeni kwa kawaida linahusu kurai wapiga kura jinsi ambavyo mwanamume humbembeleza mwanamke. Sitiari ya *maarusi* katika ubeti wa tano imetumika kurejelea wanasiasa waliowania nafasi mbalimbali za uongozi wakati wa uchaguzi huo wa 2007 nchini Kenya. Wananchi waliwapokea vyema kwa sababu ya sera walizokuwa nazo na kuwapigia kura. Tatizo lililotajwa la *wizi wa sanduku la mwanamwali* ni sitiara inayorejelea udanganyifu uliokumba hesabu za kura baada ya mchakato mzima wa uchaguzi kutekelezwa.

### 4.3.3 Matumizi ya mbinu za sanaa katika utunzi wa nyimbo za amani.

Wamitila (2003) asema kwamba mbinu hurejelea vipengele vya kimtindo na kimuundo ambavyo hupatikana katika kazi yoyote ya kifasihi. Nyimbo kama tanzu nyingine za kifasihi hutumia mbinu kuntu katika kuwasilisha maudhui yanayolengwa. Baadhi ya mbinu zinazodhihirika katika nyimbo za amani ni usambamba na mbinu rejeshi.

#### 4.3.3.1 Mbinu ya Usambamba

Kwa mujibu wa Oyoyo (2013), usambamba ni aina maalumu ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambapo hupatikana katika kiwango cha kirai, kishazi au sentensi. Ufafanuzi huu walingana na ule wa Wamitila (2003) anayeeleza usambamba kuwa mbinu ambapo msanii anayarudia maneno fulani au maana fulani kwa muundo mwingine tofauti. Urudiaji huu unaweza kujitokeza katika viwango tofauti kama vya vipashio vya kisintaksia, virai, vishazi au sentensi. Usambamba

unaweza kuwa wa aina mbalimbali mathalani kisintaksia, kisemantiki, kidhamira au kiusawe. Usambamba huwa maarufu katika nyimbo kwani hujenga muwala.

Katika wimbo *Mapatano*, Onyi Papa J ametumia usambamba wa kiusawe kwa ufanifu. Dhana ya vita imerudiwa japo kwa maneno tofauti. Mwimbaji Onyi Papa J katika ubeti wa kwanza anasema:

**Mf 22**

*Ooh Kenya*
*Kenya nchi yetu*
*Tuko kitu kimoja nchini Kenya*
*Hapo awali* ***tulikuwa na vita x2***
*Hapo awali* ***watu walipigana***
*Hivi sasa tuko kitu kimoja x2*
(Kutoka : *Mapatano*. Msanii: Onyi Papa J)

Vifungu vilivyokolezwa wino vinawasilisha dhana ile ile moja ya vita vilivyoshuhudiwa. Mwimbaji alifanya hivi kwa kusudi la kusisitiza jambo analolizungumzia na kujenga muwala. Vita vinavyorejelewa katika kifungu hiki ni tukio la kihistoria nchini Kenya ambalo lilitikisa nchi nzima.

Mhubiri Joel Kimetto katika wimbo *Sigiriet* ametumia mbinu hii pia. Usambamba unaonekana ambapo mwimbaji amerudia wazo la viongozi kuwatumia wananchi vibaya kama punda wa huduma. Vifungu vilivyokolezwa rangi vinazungumzia dhana ile ile moja.

Mwimbaji katika ubeti wa tatu anasema:

**Mf 23**

| | |
|---|---|
| *Kigeigei sigirook en* ***bikchok che indoiweech*** | Tumekuwa punda kwa **viongozi** |
| *Kigeigei sigirook en* ***kandoikab bolatosiek*** | Tumekuwa punda kwa **wanasiasa** |
| ***Kigokweri emenyon*** *kotokyige ole mi rotwet* | **Wameielekeza nchi** kwa upanga |
| ***Kigoket Kenyanyon*** *kotokyigei ole mi rotwet* | **Wameendesha Kenya** kwa upanga |

(Kutoka: *Sigiriet*. Msanii: Mhubiri Joel Kimetto)

Maneno yaliyokolezwa wino katika ubeti huu yanarejea dhana moja sawa. Kwa mujibu wa wimbo *Sigiriet,* neno 'wanasiasa' ni kisawe cha 'viongozi'. Aidha, kifungu 'wameielekeza nchi' huwasilisha dhana sawa na 'wameendesha Kenya'. Mbinu hii imetumika ili kudokeza kwa uwazi kabisa ujumbe anaonuia msanii kwa jamii lengwa na pia kutia msisitizo wa maudhui. Ujumbe wenyewe ni kutoa tahadhari kwa wanajamii watambue kuwa wanasiasa si waaminifu na huweza kusababisha maangamizi katika taifa.

#### 4.3.3.2 Mbinu Rejeshi

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mbinu rejeshi ni mbinu ya kuyaelezea matukio yaliyotokea wakati wa nyuma ya wakati wa hadithi. Matukio yenyewe huwa nje ya wakati wa mwanzo wa hadithi. Matumizi ya mbinu rejeshi katika nyimbo huwa na jukumu kuu la kuunganisha usimulizi na maudhui yanayowasilishwa.

Watunzi na waimbaji wa nyimbo za amani kama wasimulizi wowote wa fasihi, wametumia mbinu rejeshi kwa kina. Maudhui yaliyowasilishwa kupitia nyimbo zenyewe yalihusu ghasia

zilizoikumba nchi ya Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka 2007. Malengo makuu ya nyimbo za amani yalikuwa kusemeza ujumbe kwa wanajamii kuzika tofauti zao za kikabila na kisiasa ili kuijenga jamii yenye utangamano. Wasanii wengi wamerejelea matukio ya awali katika mataifa mengine ambayo yamepitia hali za vita kutokana na tofauti za kisiasa na za kikabila. Mataifa yaliyorejelewa na takriban wasanii wote ni Rwanda, Somalia, Ethiopia na Sudan. Mengine yalikuwa Iraq, Siera Leone, Burundi na Uganda.

Katika ubeti wa nne wa wimbo *Ya Boriet* mwimbaji anasema

**Mf 24**

| | |
|---|---|
| *Kitam agase we, Rwanda ak Burundi* | Tulizoea kusikia, Rwanda na Burundi |
| *Ethiopia ak Somalia* | Ethiopia na Somalia |
| *Kitom agere* | Sijawahi kushuhudia |

(Kutoka: *Ya Boriet*. Msanii: Mwinjilisti Philip Rono)

Katika ubeti huu, msanii anamkumbusha msikilizaji wake kuhusu matukio ya awali katika mataifa ya bara la Afrika na ambayo misukosuko ilipata kuangaziwa kupitia vyombo vya habari.

### 4.4 Dhana ya shani katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii za Kipsigis, Kisii na Luo

Shani ni kipengele cha usemezano ambacho kinahusu jambo linaloshangaza na ambalo si kawaida yake kutokea, kwani linastaajabisha. Ni vituko. Ni kushiriki katika mambo ambayo yanaonekana kukera au kuudhi kama vile viongozi kunyanyasa wananchi. Kipengele hiki kina

misingi yake katika uchunguzi wa riwaya ya Mfaransa Francois Rabelais ambayo ilijaribu kuyasarifu maisha katika jamii ya kizungu ya karne ya kumi na sita. Mwamzandi (2002) akimrejelea Bakhtin, *Rabelais and His World* (1984), anaeleza kuwa Robelais anaonyesha jinsi jamii za wakati huo zilivyohiari kuivunja kwa makusudi miiko iliyowekwa katika enzi hizo za karne ya kumi na sita. Serikali na makanisa ya wakati huo yangetenga siku maalum ambazo wananchi na viongozi pia wangeshiriki katika mambo yanayoonekana muhali kutendwa siku zingine za kawaida. Shani imetumika kurejelea jumla ya mambo yanakiuka miiko na mbeko za wanajamii. Mambo haya kwa kweli ni ya kufedhehesha yanapopatikana katika miktadha ya jamii.

Watunzi na waimbaji wa nyimbo za amani wametumia shani kama kifaa kitumikishi cha kisanaa ambacho kinaonyesha ukinzani wa utesi dhidi ya viongozi walio na matakwa hasi katika jamii. Mwimbaji wa wimbo *Sigiriet* (Punda) anaangazia namna ambavyo viongozi huwatumia wananchi kwa masilahi yao ya kibinafsi. Uhusiano kati ya viongozi na umma umemithilishwa na ule wa bwana na punda wake. Mwimbaji huyu anaelekea kuwalaumu viongozi kwa matukio ya ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka 2007 nchini Kenya.

Katika ubeti ufuatao wa wimbo *Sigiriet,* mwimbaji anasema:

**Mf 25**

| | |
|---|---|
| *Kigeigei sigirook en kandoikab bolatosiek* | Tumekuwa punda kwa wanasiasa |
| *Kigokweri emenyon kotokyige ole mi rotwet* | Wameelekeza nchi yetu kwa upanga |

(Kutoka: *Sigiriet*. Msanii: Mhubiri Joel Kimetto)

Mwimbaji hapa anaonyesha jinsi ambavyo viongozi wa kisiasa wamekiuka maadili ya kijamii kwa kutothamini wananchi waliowachagua. Badala ya kuwatumikia, huwatelekeza kwa namna afanyavyo mmiliki wa punda. Mwelekeo huo wa viongozi huelekeza nchi kwenye vita (upanga).

Bwana Segero katika wimbo wake *Omokimbizi* (Mkimbizi) ameangazia ukiukaji wa kimaadili uliotekelezwa dhidi ya jamii ya Wakisii. Michafuko iliyotukia pindi matokeo ya uchaguzi wa 2007 yalipotangazwa ilisababisha hasara kubwa kwa jamii ya Wakisii. Wimbo huu umetumia shani kusimulia matukio ya kustaajabisha ya kipindi hicho cha ghasia.

Katika ubeti wa saba, mwimbaji Segero anasema

**Mf 26**

| | |
|---|---|
| *Abasacha nigo bare goitwa babutorwa* | wanaume walikuwa wakipigwa na kukatwa |
| *Emetwe, chinyomba bagosambwa* | vichwa, na nyumba zao kuteketezwa |
| *Naboigo ne chigari x2* | pamoja na magari x2 |

(Kutoka: *Omokimbizi*. Msanii: Bwana Segero)

Mwimbaji anasimulia namna Mkisii alivyodhulumiwa. Ameeleza kuwa nyumba za Wakisii ziliteketezwa baada ya bidhaa kuporwa na wavamizi wasiojulikana. Aidha, wanaume walikatwa kwa panga nao wanawake wakapitia madhila ya kubakwa. Maudhui yanayokuzwa katika wimbo huu ni ya chuki na kero. Jamii ya Kisii imetendewa ukatili unaodhihirisha kuwa watendaji waliongozwa na hisia zilizotawaliwa na chuki dhidi yao.

Kipengele cha shani aidha kimedhihirika katika wimbo *Dunia* ulioimbwa na Borangi PAG. Tukio la kusikitisha la ukiukaji wa haki za kibinadamu ambalo lilihusu uteketezaji wa watu

kanisani. Kisa hiki kilitukia katika mji wa Eldoret ambapo wafuasi wa chama cha ODM waliokuwa wamejawa na ghadhabu walikuwa wakiwavamia wale wa PNU kulipiza kisasi kwa sababu ya kupokonywa haki kwa kiongozi wao Raila Odinga. Shirika la habari la BBC (news.bbc.co.ke) liliripoti kwamba Wakenya takriban thelathini wakiwemo watoto wengi waliokuwa wamekimbilia kanisa la Kenya Assemblies of God Kiambaa kutafuta hifadhi, waliteketezwa moto na kufia mle. Wengi wa wale waliopoteza maisha walitoka katika jamii ya Kikuyu, jamii ya Mwai Kibaki aliyeonekana kuwa ndiye aliyemdhulumu Raila Odinga haki zake.

Katika mshororo wa kwanza wa ubeti wa pili wa wimbo *Dunia* msanii anasema:

**Mf 27**

*Wengine walimchomwa makanisani*

(Kutoka: *Dunia*. Msanii: Borangi PAG Choir)

Tukio la kuteketeza kanisa pamoja na watu waliokuwa wamejifungia mle halijapata kushuhudiwa mahali kwingine nchini. Huu ni ukatili uliokiuka maadili ya kijamii na usiokuwa na kifani.

Silas Omondi katika wimbo *Ukabila*, amesemeza kuhusu madhara yanayotokana na ukabila nchini. Katika ubeti wa pili na wa tatu, Omondi analaumu dhana ya ukabila kuwa ndicho chanzo cha ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007 nchini Kenya. Mauaji mengi yaliyotekelezwa yalitokana na ufuasi wa kikundi fulani cha kabila.

Katika ubeti wa pili, msanii anasema:

**Mf 28**

*Hamkujali ndugu zenu nyinyi*

*Watoto wetu walibaki mayatima*

*Kwa sababu ya ukabila Kenya*

(Kutoka: *Ukabila*. Msanii: Silas Omondi)

Matumizi ya shani inadhihirika hapa namna ambavyo roho ya ukatili imewaingia watu na kusababisha mauaji. Watoto wameachwa mayatima. Vitendo hivi vya kikatili hukiuka haki za kibinadamu.

Kutokana na sehemu iliyonukuliwa hapo juu, ni dhahiri kwamba wavamizi walitekeleza mauaji yao ya kikatili kwa sababu ya chuki nyingi za kikabila. Katika ubeti wa tatu, mwimbaji anawahimiza makabila mahasidi wawache vita. Makabila matatu yaliyotajwa hapa nayo ni Kikuyu, Luo na Kalenjin. Lengo la mwimbaji hapa ni kubainisha hasa makabila yaliyoshiriki zaidi katika mapigano, ikifahamika fika kwamba makabila ya Kalenjin na Luo yaliunga chama cha ODM ilihali Kikuyu likiunga PNU.

## 4.5 Tamko ni Jibu la Tamko lingine katika Nyimbo za Amani miongoni mwa Jamii za Kipsigis, Kisii na Luo

Usemezano hudhihirika pale watunzi wa nyimbo za amani miongoni mwa jamii za Kipsigis, Kisii na Luo wanaposemezana kwa kupitia tungo zao. Yaani utungo kuwa jibu la utungo mwingine. Morson (1989) anasema kwamba wazo kuu la Bakhtin ni kuwa watu katu hawatamki neno la mwisho bali la pili kutoka mwisho. Hii ni kwa sababu kila tamko ni jibu la tamko, na katika mfuatano huu huu wa majibu ndio kutomalizika kwa matamshi kwapatikana. Atamkaye neno huwa ameathiriwa kwa njia moja au nyingine. Ama atalipinga, atalitolea rai, ataliongeza au atalipunguza. Watunzi na waimbaji wa nyimbo za amani kutoka jamii hizi tatu katika uchunguzi wameshughulikia suala lile lile moja - haja ya kuishi kwa amani. Kwa mujibu wa nyimbo zenyewe, tamko la msanii kwa mfano kutoka kabila la Wakisii, hujibiwa na mwenzake kutoka kwa Wakalenjin. Aidha tulipata kuona kwamba msanii fulani kutoka jamii moja ameweza kuimba wimbo ulio na kauli zinazojibu kauli za mwenzake kutoka jamii ile ile yao.

Mwinjilisti Philip Rono katika wimbo *Ya Boriet* (Ubaya wa Vita) anaeleza madhara ya vita katika jamii ili kuwashauri wanajamii kutafuta amani siku zote. Katika beti za tatu na nne, mwimbaji amesimulia matukio ya vita katika mataifa ya Rwanda, Burundi, Ethiopia na Somalia ambapo watu wengi walipoteza maisha yao kama kuku walioangamizwa na homa kali.

Kauli ya mwimbwji wa *Ya Boriet* (Ubaya wa Vita) inapata kujibiwa katika wimbo *Ongebir Maat Koloo* (Kinga Yashida Tiba). Katika ubetu wa saba, jamii imetahadharishwa ijitahidi kutafuta amani miongoni mwao isije ikawa sawa na Rwanda au Somalia. Wimbo huu unasisitiza haja ya

kuielemisha kila jamii kuwa kinga yashinda tiba. Nyimbo hizi mbili zimedhihirisha kipengele cha usemezano kisemacho kwamba tamko hujibu tamko la awali. Jambo linalosisitizwa hapa ni kwamba jamii zinazohusishwa katika utafiti zichukue tahadhari zisije zikaingia kwenye dhiki sawa na Somalia au Rwanda ya wakati wa awali.

Katika ubeti wa sita wa wimbo *Mapatano*, mwimbaji Onyi Papa J anawahimiza wanajamii waache vita. Vita anavyorejelea Onyi vilitukia mwaka 2007 baada ya uchaguzi wa kitaifa nchini Kenya. Anahimiza makabila mbalimbali yaache mapigano kwani Wakenya ni kitu kimoja. Kila kabila limetajwa pamoja na silaha linaloitumia kwenye mapigano. Mkikuyu ameombwa aweke upanga chini, Mjaluo aache mawe, Mnandi aweke mshale chini naye Mkisii aache kutumia mkuki. Tamko la Onyi Papa J limepata kujibiwa katika ubeti wa pili wa wimbo *Omorembe Toiyo* ulioimbwa na Segero. Akieleza hali ilivyokuwa katika maeneo mbalimbali, Segero ametaja kwamba Wakipsigis walikuwa wamejihami kwa mishale nao Wamasai wakawa na mikuki yao. Silaha hizi za Wakipsigis na Wamasai hutumika kama kinga dhidi ya mashambulizi yoyote kutoka maadui. Wimbo huu kwa hivyo unajibu kauli zilizokuwa katika wimbo Mapatano kwa kuzidishia nguvu haja ya kusitisha mapigano kwa jamii hizi mbili.

Katika ubeti wa sita wa wimbo *Ongebir Maat Koloo* (Kinga Yashinda Tiba) Mhubiri Kimetto amesimulia namna wahasiriwa wa ghasia za baada ya uchaguzi walivyokumbwa na dhiki kuu. Baadhi ya matukio anayoyataja yalikuwemo kufurushwa kwao, wengine kuuwawa na makazi yao kubomolewa. Watu walilazimishwa kuishi kwenye hema zilizojengewa wakimbizi hao wa ndani. Kauli ya Kimetto imejibiwa na Segero katika ubeti wa tano wa wimbo wake *Omorembe Toyo* (Hakuna Amani). Wimbo huu unasimulia namna ambavyo nyumba ziliteketezwa na

wavamizi wakati wa ghasia hizo na kuwashurutisha wanajamii kukimbilia usalama. Wakimbizi hao walilazimika kutafuta hifadhi kwenye hema walimoishi.

Suala la wahasiriwa wa ghasia kukimbilia misituni kutafuta hifadhi limeangaziwa na Bwana Ong'eng'o katika wimbo wake *Omorembe* (Amani). Bwana Ong'eng'o asimulia namna ambavyo wanajamii wake walivyoacha chakula kilichokuwa mezani waliposikia nduru na kukimbilia usalama msituni. Jambo lili hili limeangaziwa na Bwana Segero katika ubeti wa saba wa wimbo *Omokimbizi* (Mkimbizi). Mwimbaji anaeleza jinsi walivyolazimika kukimbilia misituni waliposhuhudia mauaji ya watu wao. Wavamizi waliokuwa wamewafikia kwenye makazi yao waliyatekeleza mauaji kwa kuwakatakata kwa panga hivyo kuzua hali mbaya ya taharuki katika jamii. Aidha, Borangi PAG katika ubeti wa pili wa wimbo Dunia wameangazia mateso waliyoyapitia wake pamoja na watoto wao mle misituni. Wanajamii walilazimika kutafuta hifadhi mle kutokana na hatari ya nkuuliwa. Kutokana na nyimbo hizi mbali mbali, imedhihirika kwamba kauli ya mwimbaji mmoja imejibiwa na mwimbaji mwingine kwa kuizidishia nguvu. Kupitia uhusiano huu wa kauli, kipengele cha usemezano kwamba kila tamko huwa jibu la tamko lingine kimefanikishwa.

Katika wimbo *Haki*, mwimbaji Peter Nyakundi anachukua mwelekeo tofauti na wale wasanii wengine walioimba kuhusu amani. Kauli ya Nyakundi yaelekea kupinga kauli za wasanii wengine waliowahimiza wanajamii kusaka amani. Katika ubeti wa kwanza, unadhihirisha kwamba bila haki, hakuwezi kuwa na amani. Aidha katika ubeti wa pili wa wimbo huo *Haki*, msanii huyo anasema kwamba twahitaji amani ndio lakini pia tuwe na haki.

### 4.6 Kihitimisho

Sura imejadili vipengele mbalimbali vilivyotafitiwa katika kazi hii. Kwanza, ili kuyafikia malengo yake, imechunguza athari za mazingira katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za amani. Aidha imedhihirisha sifa za usemezano katika nyimbo za amani. Sifa hizi ni pamoja na kuathiriwa na mazingira pamoja na matini nyinginezo. Hali kadhalika, uwepo wa sajili ya matumizi ya lugha katika kuendeleza amali za kijamii na matumizi ya fani za lugha kufanikisha upitishaji wa maudhui. Mbali na hayo, dhana ya shani katika nyimbo za amani imejadiliwa pamoja na sifa ya kwamba tamko ni jibu la tamko lingine. Mihimili ya nadharia ya usemezano imetuongoza katika kuyafikia malengo yetu.

Sura inayofuata ni hatima yetu. Tumetoa hitimisho, matokeo ya uchunguzi wetu pamoja na kutathmini madhumuni ya utafiti kama yamefikiwa na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumetoa muhtasari wa kazi tuliyoipitia kwa kuelezea shabaha kuu ya utafiti, upeo wa utafiti na yaliyomo katika kila sura. Matokeo ya utafiti yamejadiliwa kwa kina, kwa kuelezea

jinsi utafiti huu ulivyofanikiwa katika kuyafikia malengo yake. Aidha, mapendekezo yametolewa katika sura hii.

### 5.1 Muhtasari wa kazi

Shabaha kuu ya utafiti huu ilikuwa ni kuhakiki usemezano katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii tatu za Wakenya baina ya mwaka 2008 na 2013. Jumla ya nyimbo ishirini zilihakikiwa. Nyimbo hizi ziliteuliwa kimakusudi kutoka nyimbo nyingi zilizoimbwa na wasanii kutoka jamii tatu hizo yaani Kipsigis, Kisii na Luo. Uhakiki huo ulitekelezwa ili kuwezesha utafiti huu kufikia lengo hilo.

Sura ya kwanza ya tasnifu hii iliuwekea utafiti msingi wa kijumla. Hapo, vipengee muhimu vilihusishwa. Vipengee hivyo ni pamoja na utangulizi, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti na nadharia tete. Isitoshe, sababu ya kuchagua mada ilifafanuliwa, umuhimu wa mada pia ulielezwa. Aidha, upeo na mipaka ya utafiti ilitambuliwa.

Sura ya pili ya tasnifu hii ilishughulikia tahakiki ya maadishi. Isitoshe, misingi ya kinadharia ilipitiwa. Kwa ajili ya utafiti wetu, nadharia ya usemezano ilifafanuliwa kwa kuangazia mihimili yake.

Fauka ya hayo, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti yalifafanuliwa ili kujenga msingi bora wa uchunguzi wetu. Mwisho, utambulishaji wa pengo la kitaaluma uliangaziwa. Katika sura ya tatu, mbinu zilizoshirikishwa katika utafiti zilifafanuliwa. Sehemu hiyo ilihusisha uteuzi wa sampuli,

ukusanyaji data maktabani na nyanjani. Hali kadhalika maelezo kuhusu vifaa vilivyotumika katika shughuli za utafiti yalitolewa. Hatimaye, michakato ya uchanganuzi wa data ilifafanuliwa.

Sura ya nne ililenga kuiwekea sura ya tano msingi. Hivi kwamba, ufafanuzi wa kihistoria juu ya vita miongoni mwa jamii tatu teule katika kazi hii. Historia hiyo imeshughulikia matukio ya kabla ya ukoloni kuanzia miaka ya 1800 hadi mwishoni mwa karne ya 20. Historia hii ilitupa mwanga katika kujadili masuala nyeti katika nyimbo hizi.

Sura ya tano ilinuia kuchunguza sifa za usemezano zinavyojitokeza katika nyimbo za amani miongoni mwa jamii za Kipsigis, Kisii na Luo. Sifa hizi ziliweza kudondolewa moja baada ya nyingine. Mihimili ya nadharia ya usemezano ilielekeza uchambuzi ili kumwezesha mtafiti kuyafikia malengo yake. Jumla ya nyimbo ishirini zilishughulikiwa katika kazi hii.

**5.2 Matokeo ya Utafiti**

Lengo la utafiti huu la kuthibitisha kuwa mazingira huathiri utunzi na uimbaji wa nyimbo za amani lilitimia. Ilidhihirika kwamba mazingira ya watunzi na waimbaji ndiyo ambayo hukuza muktadha wao wa utunzi na uimbaji. Katika kazi hii, imedhihirika kwamba mazingira huathiri moja kwa moja mwelekeo wa watunzi na waimbaji. Tuligundua kuwa mazingira huathiri utunzi na uimbaji kwa mbali wakati mazingira yanapokuwa maudhui katika utunzi na uimbaji huo. Ilibainika pia kuwa mazingira yanayowakuza na kuwaathiri waimbaji katika uimbaji huo hayawezi kuzungumziwa bila ya kuwekwa katika muktadha wa kihistoria. Kipengele cha kihistoria kinachorejelewa katika uchunguzi wetu kilikuwa vita vilivyozuka miongoni mwa jamii tatu teule za Wakenya baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa kitaifa wa mwaka wa 2007. Utafiti huu umeonyesha wazi kwamba mtunzi na mwimbaji wa nyimbo za amani hawezi

kutunga na kuimba katika ombwe. Yeye huathiriwa na mazingira anayotungia kazi yake, kwa kuwa yeye mwenyewe ni zao la mazingira hayo. Mtunzi na mwimbaji ni mwanajamii na huitumikia jamii ambayo imo katika mazingira fulani. Mwimbaji kwa hivyo hawezi kutunga na kuimba bila kuathiriwa kwa njia moja au nyingine na mazingira anamoishi au yaliyomkuza.

Suala la umuhimu wa mazingira katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za amani, ilidhihirisha kuwa kuna uhusiano wa nyimbo hizi na usemezano. Kama ilivyo katika usemezano, kwamba kuna mahusiano ya wahusika na mazingira waliyomo, ndivyo ilivyo katika nyimbo za amani kwani waimbaji huhusiana na mazingira yao katika utunzi na uimbaji wao. Kwa mtazamo huu, ilibainika kuwa usemezano upo katika nyimbo za amani.

Kazi hii pia ilishughulikia jinsi nyimbo za amani zinavyoendeleza amali za kijamii kupitia usemezano. Tuligundua kwamba katika kuwasilisha mawazo anuwai kwa wanajamii, waimbaji hushirikisha sajili mbalimbali za mazungumzo. Matumizi ya sajili za mazunngumzo katika nyimbo za amani yamebainika kwa kuwepo na mitindo tofauti ya matumizi ya lugha katika nyimbo hizi. Mifano inayojitokeza ni lugha ya kidini, siasa, vijana/ mitaani na kadhalika. Waimbaji walielekea kutumia mtindo fulani wa lugha katika kuelezea maudhui yao. Mtindo huo yamkini ni ule uliozoeleka katika mazingira ya mazungumzo yao.

Utafiti huu pia ulichunguza mbinu za lugha zilivyotumiwa kupitishia maudhui katika nyimbo teule za amani. Ilibainika kwamba mbinu hizo zilishirikishwa na watunzi na waimbaji katika tungo zao ili kuziboresha kazi zao huku wakidhibiti hisia za hadhira zao. Mbinu za lugha hujenga muwala na kuathiri nyimbo hivi kwamba huwezesha maudhui katika nyimbo

kufafanuliwa na kueleweka vizuri zaidi. Fani mbalimbali za lugha zilielezwa zikiwemo: taswira, kinaya, usambamba, methali na kadhalika.

### 5.3 Mapendekezo

Ijapokuwa utafiti umefanywa katika utanzu wa nyimbo za amani, kuna vipengele ambavyo bado vinahitaji kuchunguzwa zaidi. Ipo haja ya kuchunguza athari za utandawazi na biashara ya muziki huu katika utunzi na uimbaji wake. Swali nyeti hapa likiwa ni je, utandawazi na biashara ya muziki wa amani vinaimarisha au kudidimiza muziki wenyewe?

Utafiti huu pia wapendekeza kuwa uhusiano kati ya nyimbo za amani na dini uchunguzwe zaidi. Ijapokuwa utafiti huu umechunguza uhusiano huo kwa kuzingatia nadharia ya usemezano, kuna haja ya kulitafitia suala hili zaidi hasa kwa kutilia maanani nadharia ya mwingiliano-matini.

Ni maoni ya utafiti huu kwamba kwa kuwa nyimbo zinaweza kutumika kukuza chuki kupitia vyombo vya habari kama ilivyotukia katika taifa la Rwanda, kuna haja ya kulichunguza suala hili zaidi.

## MAREJELEO


Akombo, D.O. (2009). *Music and healing during post-election violence in Kenya*. https://normt.uib.no/isndex.php/voices/article/viewArtical/349/273 (17,April 2014)

Bakhtin, M. M. (1981), Michael, H. (ed), translation by Caryl Emerson and Michael Holquist, *The dialogic imagination: Four essays.* Austin, Texas: University of Texas University Press.

Bakhtin, M. M. (1984 Ed.). *Problems of Dostoevsky's poetics*. *Theory and history of literature.*Vol. Minneapolis: University of Minnesota Press.

Bakhtin, M. M. (1986 Ed.). *Speech genres and other essays*. Austin: University of Texas Press.

Bakhtin, M. M. (1990). *Art and answerability.*Austin: University of Texas Press.

Bakhtin, M. M. (1978) (Mhar..). Speech Genresand other late Essays

Chesaina, C. (1991). *Oral literature of the Kalenjin*. Nairobi: East African Publishers.

European Union Election Observation Mission. (2008). Kenya Final Report: GeneralElections 27, December 2007.

Finnegan, R. (2012). *Oral literature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press.

Gakahu, N. (2010). *The role of broadcast media in media in behavior change & H.I.V AIDS commununication to the youth:* A focus on Kenya Music industry. http://www.academic HYPERLINK "http://journals.org/jmcs"journals.org/jmcs (10/8/2014)

Goldsworthy, D. (1982). *Tom Mboya: The man Kenya wanted to forget*. Heinneman UK

Gumbe, E. (2015). *The role of women in inter-ethnic peace building in South Nyanza, Kenya, 1850-2008.*The International Journal of Humanities and Social Studies.(ISSN 2321 – 9203) www.theijhss.com

Hymes, Dell H. (1974). *Foundations in Sociolinguistics: An Ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Kahigi, K. K. (1995). Lugha katika vitabu vya watoto. Katika *kioo cha lugha: jarida la Kiswahili, isimu na fasihi.*Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es salaaam. Juzuru, Na.1 (uk. 21-36)

Kairu, P. (2016). Fatuma Abdulkadir Adan- Inclusive Security. www.nation.co.ke (10th August 2016)

Kea, P. (2006). *Usemezo katika Nyimbo za Taarab.* (M.A) Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kipuri (1983). *Oral Literature of the Maasai*. Nairobi: Heinemann.

Korir, K. (2014). *Appropriation of Kalenjin idioms in Selected songs of Joel Kimetto.* (Tasnifu)

Kutol, K., Mosol, K., na Simotwo, P. (2009). *Role of print media in conflict management during the 2007/2008 post-election violence in Kenya: The Case of The Standard and Taifa Leo Newspapers.* Journal of Intra African Studies (2009) Vol. 2.

Matei, A. K. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Nairobi: Oxford University Press.

Mukarovsky, J. (1977). *The word and the verbal art. Selected essays*. New Haven: Yale University Press.

Muriithi, J.J. (2002). Usemezano katika Tamthilia ya Kiswahili. (MA) Chuo Kikuu cha Kenyatta (Tasnifu)

Mbarwa, H. (1996). *Your Oral Literature*. Nairobi: Eagle H Publishers.

Morson, G.S Caryl.(1990). *Mikhail Bakhtin, Creation of Prosaics*. Stanford: Stanford University Press.

Mhrody (2012). Critical Analysis of Peace Train by Cat Stevens. https://www.studymode.com/essays/critical-analysis-of-peace-train-by1317233.html.(17/08/2014)

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mwamzandi, I. (2002). *Usemezano katika Umalenga wa Kiswahili. Shahada ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Egerton: Haijachapishwa.

Nandwa, J. na Bukkenya, A. (1983). *African Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longman.

Nandwa, J. na Bukkenya, A. (1976). *Oral Literature Among the Abaluhya*. M.A Thesis. University of Nairobi.

Naseh, L. (1997). Codeswitching between Persian and Swedish, Eurosla 7 Proceedings: 201-211.

Nebe, J.M. (2012). *Civil Conflict Management of post Election Violence 2007/2008 in Kenya-Project.* University of Tier / Germany.

Njogu, K. (1993). "Dialogic Poetry: A Contestation and Social Challenge in East Africa Poetic Genres" Phd Thesis. (Unpublished). Yale University.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Maupeu, H. (2007). *Songs and Politics in East Africa.* Dar es Salaam: Mkuki wa Nyota Publishers.

Njogu, K. na Maupeu, H. (1993). 'Dialogic Poetry: A Contestation and Social Challenge in East African Poetic Genres', Phd Thesis (Unpublished). Yale University

Njogu, K. na Maupeu, H. (2004).*Reading Poetry as Dialogue: An East African Literary Tradition*. Nairobi: JKF.

Nyawira, P.G. (2009). *Music as a social discourse: The contribution of popular music to the awareness and prevention of HIV/AIDS in Nairobi, Kenya*. (Tasnifu)

Ochieng’ R. W. (1986).*Kenya's People: People of the South-Western Highlands – Gusii*. Nairobi: Evans Brothers.

Odongo, G.A. (2004). *The Role of Women in Peace Building in Kenya: Focussing on 1992 Rift Valley land clashes*. (Tasnifu)

Omwenga, M. H. (2014). *A History of Cross border Conflicts between Kipsigis and Abagusii of Kenya,1963-2002*. (Tasnifu)

Oyoyo, J. O. (2013). *Tasnifu ya Uhakiki wa Fani katika Ngano tano za Kiswahili.* Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Pearce, L. (1994). *Reading Dialogics*. Routledge.

Raman, S., Peter, W., na Brooker, P. (2005). *A reader”s Guide to Contemporary Literary Theory*. Harlow, England: Pearson Education Limited.https://www.enoughproject.org/blogs/rebecca https://www.independent.co.uk/news/world/africa/songs-of-praise-how-rwanda-got-its -groove-back-1866944.html

Rotich, A. (2010). *Uchanganuzi wa Kiuamilifu katika Nyimbo za Watoto.* (Tasnifu) : Chuo cha Moi

Senkoro, F.E.M.K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Simatei,PeterTirop.(2010).*“KalenjinPopularMusicandtheContestationofNationalSpacein Kenya”*.Journalof EasternAfricanStudies.4.3,(2010):425-434.

Stone, A. (2010). *Stewart and Samputu’s Rwandan Dream.* https://www.independent.co.uk/news/world/africa/songs-of-praise-how-rwanda-got-its-groove-back-1866944-html. (17th Sunday 2010)

Tarde (1969). *On Communication and Social Influence Papers*. Chicago: Chicago University Press.

Thomas, A. Schmitz (2007). *Modern Literary Theory and Ancient Text: An introduction.* Main Street, Malden, MA 02148-5020, USA.

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

TUKI (2006). *English – Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

TJRC (2013). *Report of the Truth, Justice and Reconcilliation Commission Vol. 1*. Nairobi: TJRC

Vershbow, M.E. (2010). *The Sounds of Resistance: The role of Music in South Africa's Anti-Apartheid movement.* http://www.studentpulse.com/articles/265/the-sound-of-resistance-the-role-of-music-south-africa (17/08/2014)

Volosinov, V.N. na Mikhail Bakhtin (1986). *Marxism and the Philosophy of Language.* Cambridge, MA: Harvard University Press.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Mbinu na Vipengele vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications.

## KIAMBATISHO - NYIMBO MBALIMBALI

**1. NG'ELYEPTA** *(ULIMI)* na Joel Kimetto

| | |
|---|---|
| *Ongenai tugul kele ng'elyepta ko ya missing'* | tufahamu kuwa ulimi ni mbaya mno |
| *Ongeboisien en ng'omnatet ooh*! | Tuutumie kwa hekima ooh! |
| *Kisich Jakobo kole ngelyepta* | Yakobo alitambua kwamba ulimi |
| *Ko ming'in kot ago* | ni kiungo kidogo sana lakini |
| *Lasegei en tuguk che eechen x2* | hujivuna kwa mambo makuu x2 |
| | |
| *Kimwa Isaiah kole bwo* | Nabii Isaiah alimaka |
| *Karageer Jehovah ago a chi ne* | nimemwona Yehovah ilihali mimi ni |
| *Amurwon* mising' *kero nwanan kut* | mwovu naongea maneno machungu |
| *Ngwanan kut ak kemenye ak biik* | mdomo mkali na twaishi na watu |

| | |
|---|---|
| *Che ng'wonen kutuswekwak* | wenye midomo mikali |
| | |
| *kimwachini kandoikab kaniset* | tunawaambia viongozi wa kanisa |
| *kogochi kutuswek kiptaiyat* | kumpa Mungu midomo yao |
| *kosuut si komong'uneen che kororon* | kuitakasa ili mazuri yaweze kutoka |
| *che ibu kalyet* | yaletayo amani |
| *Ogilgei oigu kabaruneet amun* | Mjitahidi muwe kielelezo kwa sababu |
| *Ondochini biik che ngwnen kutuswekwak* | mwaongoza watu wenye midomo mikali |
| | |
| *Agot okwek kandoikab emenyon* | Hata enyi viongozi wa nchi yetu |
| *Oboisien ng'elyebwek en ng'omnatet* | tumieni ndimi zenu kwa hekima |
| *Matoibu ng'aleek che ibu toiyeet* | msiongee maneno yanyogawanya |
| *En emenyoon* | katika taifa letu |
| | |
| *Ng'wanan kut, keero ng'wanan kut* | mdomo wangu mkali, ona ni mkali |
| *ondochini biik che ng'wonen kutuswekwak* | mwaongoza watu wa midomo mikali |

**2. ONGEBIR MAAT KOLOO** (*KINGA YASHINDA TIBA*) na Joel Kimetto

| | |
|---|---|
| *Kimi chepyoso* | palikuwa na mama mmoja |
| *Ne kibo emetab Shunem ooh* | katika nchi ya Shunem |
| *Ne kigalenji maotiot isiche lakwet* | aliyeahidiwa na nabii atamzaa mwana |

| | |
|---|---|
| *Tun kosich lakwet, ne matian* | alijaliwa mtoto ambaye baada ya muda |
| *Kome lakwanato* | mtoto huyo kaaga dunia |
| *Kolabat kocheng' maotiot en ole kimi* x2 | mama kakimbia alikokuwa nabii x2 |
| | |
| *Kigeer maotiot Chepsunamindet* | Nabii alimwona mama Mshunami |
| *Komii ole loo* | kwa mbali |
| *Koyokto Gehazi otwogindenyin* | kamtuma mtumishi wake Gehazi |
| *Kolenji torokten ak iteben ilenji* | aende amkabili kisha amwuulize |
| | |
| *Tos ichamegei i?* | Je, u mzima? |
| *Chamegei maning'otiondeng'ung i?* | Mumeo yu mzima? |
| *Chamegei lakwet i?* | Mtoto yu mzima? |
| *Kowol kole kichamegei e kichamege* | akamjibu tu wazima e tu wzima |
| | |
| *Tos kichamegei oo bikyook?* | Je, tu wazima wenzangu? |
| *Tos kichamegei komanda kosobeek i*? | Je, tu wazima hadi kwa Wakisii? |
| *Tos kichamegei kot koit Mutendeek i?* | Je, tu wazima hadi kwa Wakuria? |
| *Ara kichamegei koboto Jaluoyek i?* | Je, tu wazima hadi kwa Waluya? |
| *Tos kichamegei oo bikyok i?* | Je, wenzangu tu wazima? |
| *Tos kichamegei en kotab Kalenjin?* | Je, jamii ya Kalenjin tu wazima? |
| *Tos kichamegei kot koit North Eastern?* | Je, tu wazima Kaskazini Mashariki? |
| *Tos kichamegei kot komanda Mombasa?* | Je, tu wazima hadi Mombasa? |
| *Ara kichamegei kot koit Kegoek i?* | Na tu wazima hata kwa Wakikuyu? |

| | |
|---|---|
| *Kichamegei kot koit Maasaek?* | Tu wazima hata kwa Wamaasai? |

***Pambio:***

| | |
|---|---|
| *Kichamegei e kichamegei* | Tu wazima naam tu wazima |

| | |
|---|---|
| *Olen kichamegei ago ale biik kariik*? | Mnasema mu wazima na watu wajihami? |
| *Olen kichamegei korire emenyon i?* | Mwasema mu wazima na taifa linalia? |
| *Olen kichamegei ketumdoi korotiik i?* | Mwasema mu wazima na damu yamwagika? |
| *Kileen kichamegei komiten suriet i?* | Twasema hatujambo ilhali kuna chuki? |
| *Kileen kichamegei komiten ukabila i?* | Twasema hatujambo ilihali kuna ukabila? |
| *Keer che seretos matinye ole menye* | Tazama masikini hawana makazi |
| *Keer che nyalildos kikibuteen goriikwak* | Tazama masikini nyumba zao zilibomolewa |
| *Keer che nyalildos matinye sigikwak* | Tazama masikini ni mayatima |
| *Keer che seretos kikobeet sigikwaak* | Tazama masikini waliwapoteza wazazi |
| *Onetweech Kosobeek (olenji)* | Wafunze Wakisii *(kwamba)* |
| *Ongebir maat koloo* | Kinga yashinda tiba |
| *Onetweech Kalenjin (olenji)* | Wafunze Wakalenjin *(kwamba)* |
| *Ongebir maat koloo* | Kinga yashinda tiba |
| *Onetweech Kegoek (olenji)* | Wafunze Wakikuyu *(kwamba)* |
| *Ongebir maat koloo* | Kinga yashinda tiba |
| *Omwachi Maasaek (olenji)* | Wajuze Wamaasai *(kuwa)* |
| *Kibire maat koloo* | Kinga yashinda tiba |
| *Si maigei emenyon Rwanda* | Ili taifa letu lisiwe kama Rwanda |

| | |
|---|---|
| *Mongeige Somalia* | Tusije tukawa kama Somalia. |

**3. YA BORIET (VITA NI VIBAYA) na Bw. Phillip Rono**

| | |
|---|---|
| *Men koutun wei amat in koutwon x2* | Tahadhari usije ukasahau, nami pia x2 |
| *Tuguk che kiyayak en tarigit 29 disemba* | Yaliyotukia tarehe 29 disemba |
| *Ye kingobata lewenisiet en emetab Kenya* | Baada ya uchaguzi katika taifa la Kenya |
| | |
| *Kichei boriet wei, ne tom agere* | Vita vikali vilizuka, sijashuhudia |
| *Kibek biik wei che matinye leluut* | Watu wasiokuwa na hatia waliaga dunia |
| *Nda ma Jehovah ne kitonoon koboteech* | Kama si Mungu aliyesimama nasi |
| *Ko kita kibeguu ak kelus ak kemee* | Tungeangamia mautini |
| *Meet ne kime teret* | Kifo sawa na cha chungu kilichovunjika |
| *Ya boriet wei, mamiten kit ne u x2* | Vita ni vibaya, hakina kisawe x2 |
| *Ongesaan boriet ko u kesegeet* | Tuambae vita kama *keseget* |
| *Ne kisaan ng'okto* | Alivyoambaa mbwa. |
| | |
| *Kitam agase we, Rwanda ak Burundi* | Tulizoea kusikia, Rwanda na Burundi |
| *Ethiopia ak Somalia* | Ethiopia na Somalia |
| *Kitom agree* | Sijawahi kushuhudia |
| | |
| *Kichei boriet we* | Vita vilishika |
| *En Rwanda ak Burundi* | Katika Rwanda na Burundi |
| *Kiibek biik wei ko u ngogeniik* | Watu walikufa kama kuku |
| *Che kabar amalda* | walioangamizwa na homa kali |

| | |
|---|---|
| *Ya boriet wei mamiten kit ne u* | Vita ni vibaya, havina kilinganisho |
| *Ongesaan boriet ko u keseget* | Tusahau kabisa vita kama *keseget* |
| *Ne kisaan ng'okto x2* | Alivyosahau mbwa x2 |
| *Kichei boriet we, en Iraq wee* | Vita vilishika nchini Iraq |
| *Kocheng bichu Gaddafi kot kobol* | Wakamsaka Gaddafi na kumfichua |
| *En ole kimi ak korwokyi ak koogeet* | Alimochificha wakamhukumu kifo |
| *Ak kogeer emet* | Na ulimwengu wote ukashuhudia |

| | |
|---|---|
| *Kararan kalyet wei* | Amani ni hali nzuri |
| *Mamiten kit neu x2* | Haina kifani x2 |
| *Ogot nda mamiten che kiame* | Hata ukikosa chakula |
| *Ko kararan komi kalyet* | Ni vyema kuwe na amani |
| *Ogot nda bete che kiame komie komi kalyet* | Hata ukikosa chakula amani ni muhimu |
| *Ongecheng' Jehovah asi kogoneech kalyet* | Mtafute Mungu ili atupe amani |
| *Kimoche kalyet en Kenya, makimache boriet* | Twataka amani Kenya wala si vita |

**4. SIGIRIET*(PUNDA)* na Mh. Joel Kimetto**

| | |
|---|---|
| *Kianyoru sigiriet ne kirorie en Kapsoit* | Nilimwona punda akikenua Kapsoit |
| *Kobwotwoon sigiriet ne kibo Baalam* | Nikakumbuka punda wa Baalamu |
| *Ne kiing'alaal x2* | Ambaye aliongea x2 |

| | |
|---|---|
| *Kigaguur laitoriat Baalam kochup Israel* | Mfalme alimwalika Baalamu alaani Israeli |

| | |
|---|---|
| *Soman en sirutik Koitosiek 22 x2* | Soma andiko katika Hesabu 22 x2 |
| *Kianyoru sigiriet ne kirorie en Kapsoit* | Nilimwona punda akikenua Kapsoit |
| *Kigaguur laitoriat Baalam kochup Israel* | Mfalme alimwalika Baalamu alaani Israeli |
| *Kiyamisyi tuguk che eechen* | Alimwagizia mambo muhimu makuu |
| | |
| *Che kimache koyai* | Alichotaka ayatekeleze |
| *Kiarorji tuguk che eech che kimoche* | Alimwelezea mambo makubwa aliyotaka |
| *Koyachi* | Amfanyie |
| *Kiba ngomi oret koesio sigiriet kwo* | Akiwa njiani, punda akaktaa kwenda mbele |
| *Kigeer malaikayat nemi tai* | Alimwona Malaika mbele yao |
| *Kokang'us rotwenyin x2* | Ameushika upanga mkononi x2 |
| | |
| *Kiyesio sigiriet kwo ole mi rotwet* | Punda alikataa kuelekea ulikokuwa upanga |
| *Konereech maotiot kobir sigiriet* | Nabii kakasirika na kuanza kumpiga punda |
| *Kwa kong'alal x2* | Hadi punda akanena x2 |
| | |
| *King'alal sigiriet en kutiit ko u chito x2* | Punda alinena kama binadamu x2 |
| *Kile sigiriet tos nee ne kaachililuun ra* | Akasema nimekukosea nini hadi |
| *Ibiroon mising' ago tom ayaun kiy ne ya* | Ukanichapa vibaya ilihali sijakukosea |
| *Kigeigei sigirook en bikchok che indoiweech* | Tumekuwa punda kwa viongozi |
| *Kigeigei sigirook en kandoikab bolatosiek* | Tumekuwa kama punda kwa wanasiasa |
| *Kigokweri emenyon kotokyige ole mi rotwet* | Wameielekeza nchi yetu uliko upanga |

| | |
|---|---|
| *Kigoket Kenyanyon kotokyigei ole mi rotwet* | Wameelekeza Kenya yetu uliko upanga |
| *Magere kamanut en bikwak che indochin* | Hawathamini wananchi wanaowaongoza |
| *Keere kelunoik che nyoruneen kandoisenywan* | Wanashughulikia masilahi yao binafsi |

| | |
|---|---|
| *Jehovah, nyon asi indoiweech* | Yehova, njoo ili utuongoze |
| *Kisaiin kele indochi Kenya inyon* | Tunakuomba uongoze Kenya yetu |
| *Ilitiit kandoik che indoiweech* | Waelekeze viongozi wetu |
| *Si komuuch icheek koyai mageeng'ung'* | Ili waweze kutenda mapenzi yako |

**5. NI AMANI na Bw. Nyakundi Peter**

***(Pambio)***

*Wakenya mtaani kila kona (Ni amani!)*

*Makabila siasa wananchi (Ni amani)*

*Hakuna hata kukosana sana (ni amani)*

*Kutafuta haki na ukweli (ni amani)   x2*

*Amani tu Wakenya hatutaki injustice*

*Ndo maana tuko hapa tunapreach hiyo justice*

*Mablunder kibao ni kama twacheza na dice*

*Na wengi ni wanyonge hawana choice wanahanda tu wanasare maacomplice*

*Bila maacomplice vipi wangeacomplish za ill motive*

*Unakaa unazubaa unashindwa vipi yaani amani itadumu nchini*

*Haki kwa hakika itahitajika kwanza ndio amani itafuata jo bila vita yee*

***Pambio***

*Wakenya mtaani kila kona (Ni amani!)*

*Makabila siasa wananchi (Ni amani)*

*Hakuna hata kukosana sana (ni amani)*

*Kutafuta haki na ukweli (ni amani) x2*

*Altitude ilirise na ikaendelea kurise*

*Instead of temperature kudrop zikarise*

*You see, akacome akasema welcome*

*Wadhii wakatajwa wakasema don't come*

*Mkenya analia daily na wanalia eti tuform inquiry na*

*Wanabuy time na madime through corruption*

*Waseme wamesolve crime, Wakenya wabaki wapi?*

***Pambio***

*Wakenya mtaani kila kona (Ni amani!)*

*Makabila siasa wananchi (Ni amani)*

*Hakuna hata kukosana sana (ni amani)*

*Kutafuta haki na ukweli (ni amani) x2*

*Forward forward once again my brother and my sister my dady and mum*

*Looking for peace, fighting everyday*

*So lets wake up lets preach peace*

*Justice, justice let it be known*

*Justice justice let it prevail, impunity bye bye*

*And never come again and now I'm for real*

***Pambio***

*Wakenya mtaani kila kona (Ni amani!)*

*Makabila siasa wananchi (Ni amani)*

*Hakuna hata kukosana sana (ni amani)*

*Kutafuta haki na ukweli (ni amani)   x2*

*Watu wengi mitaani wanasema wanataka peace*

*Justice kwenye streets, kwenye ghetto*

*Pia kanisa viongozi wahubiri*

*Tunapenda kila culture, religion,*

*Kila mtu, kila race tuishi kwa pamoja (peace)*

*Peace, justice yaani humility*

***Pambio***

*Wakenya mtaani kila kona (Ni amani!)*

*Makabila siasa wananchi (Ni amani)*

*Hakuna hata kukosana sana (ni amani)*

*Kutafuta haki na ukweli (ni amani)   x2*

*Wakati umefika za mwishoni wa dakika*

*Ndugu yangu chunga we hutasaidika*

*Kukosa amani we vita ni hakika*

*Wachana na kiburi we kijana wee!*

*Sitaki corruption, tribalism na hate*

*Sitaki utengano, umoja ndio nguvu*

*Nataka udugu sisi tuishi kwa amani*

*Nataka umoja, ndio haki ndio ngao*

***Pambio***

*Wakenya mtaani kila kona (Ni amani!)*

*Makabila siasa wananchi (Ni amani)*

*Hakuna hata kukosana sana (ni amani)*

*Kutafuta haki na ukweli (ni amani)   x2*

**6. HAKI na Bw. Nyakundi Peter**

*You know them! You know how they do!*

*Walisema wanataka haki (haki!)*

*Amani , lakini tuwe na haki (haki!)*

*Mitaani, mashinanai kwote! (haki!)    x2*

*Knock! Knock on the door'*

*I'm impunity lets pull out of the Rome statute*

*Them, no! nani alisema tukitoka tuko safe*

*Yes we want peace but we still want justice*

*Natetea wale waliotuwacha, natetea wale walilia*

*Natetea wale walidhulumiwa, yaah!*

***Pambio***

*Walisema wanataka haki (haki!)*

*Amani lakini tuwe na haki (haki!)*

*Mitaani walisema kwote (haki!)*

*Kericho huwa tunataka haki x2*

*Coming on stage, informing once again*

*It's all about love, it's all about justice*

*It's all about the people,it's all about the rights*

*It's all about me, it's all about you, it's all about us*

*For impunity No! No!, we don't want*

*For unity Yes! Yes! We can and that's right now*

*And that's the point*

*And that's the point*

***Pambio***

*Walisema wanataka haki (haki!)*

*Amani lakini tuwe na haki (haki!)*

*Mitaani walisema kwote (haki!)*

*Kericho huwa tunataka haki        x2*

*Confessions in Kenya kuhusu conflict in Kenya*

*Justice delayed is justice denied*

*Let the wrong be charged*

*Umoja bila haki, ni uongo*

*Uongo, corruption, porojo, impunity kando*

*Solidarity, juu ya maboundaries, on point*

***Pambio***

*Walisema wanataka haki (haki!)*

*Amani lakini tuwe na haki (haki!)*

*Mitaani walisema kwote (haki!)*

*Kericho huwa tunataka haki        x2*

*Walisema wanataka haki kwa hakika*

*Kilio chao sijui kama kimesikika but najua amani tu ndio wanataka*

*Wanadai tangu jadi wamesaka but mpaka now hawajaipata*

*Mola mbele, amani tu ndio itafuata lakini ni baada ya haki*

*Sometimes watulia mpaka unawonder Kenya a once just nation*

*Bila discrimination*

*Prosecution siyo persecution, so tulia haki tu ndio itafuata*

***Pambio***

*Walisema wanataka haki (haki!)*

*Amani lakini tuwe na haki (haki!)*

*walisema kwote (haki!)*

*Kericho huwa tunataka haki x2*

*Ni hakika kikosi cha polisi ni risasi*

*Kukushika kukufunga bila kesi, lakini haki yetu sisi tutapata kihalisi*

*Mimi na wewe, wewe na mimi*

*Tutendeane haki ndio tuishi kwa amani*

*Viongozi tusemezane kisha nyinyi muelewane*

*Mkizidi kuzozana hata sisi tutagongana*

*hata sisi tutagongana*

***Pambio***

*Walisema wanataka haki (haki!)*

*Amani lakini tuwe na haki (haki!)*

*Mitaani walisema kwote (haki!)*

*Kericho huwa tunataka haki x2*

**7. DUNIA na Borangi PAG**

*Dunia hii siyo kwetu ndugu yangu*

*Machafuko yaonyesha wazi siyo kwetu*

*Yaliyotabiriwa kweli yametimia*

*Waumini tukaeni macho kwa maombi x2*

*Kila tunapofika uchaguzi*

*Mbona twapigana bure*

*Tukumbukeni mateso tuliyopata wakati wa uchaguzi 2007*

*Hata wake na watoto waliteseka pale msituni yoyo*

*Wengine walichomwa makanisani*

*Amani uko wapi duniani*

*Tangaza agape*

*Upendo wa Yesu wa ajabu*

*Amani tutapata kwa Yesu tutapata*

*Tunaposoma Bibilia yatuambia kwamba*

*Mtakapoyaona mambo haya*

*Mitetemeko, njaa na vita duniani*

*Jua ya kwamba nyakati hizi ni za mwisho*

*Ni za mwisho*

*Kila tunapofika uchaguzi*

*Mbona twapigana bure*

*Tukumbukeni mateso tuliyopata wakati wa uchaguzi 2007*

*Hata wake na watoto waliteseka pale msituni yoyo*

**8. OMOREMBE** (AMANI) na Bw. Ong'eng'o

*Amani, amani, amani!*

*U amani x2*

*Naomba amani*

*Amani kwetu amani*

*Bila amani hatuna raha x2*

*Bila amani tutakufa njaa x2*

*Uu amani yashinda pesa x2*

*Oo amani yashinda mali x2*

*Afrika ni kwetu, oyee! x2*

*Ndugu tupendane, oyee! x2*

*Ong'eng'o*

*Nikiwa kwangu nyumbani x2*

*Ong'eng'o nalilia amani x2*

*Bila amani hatuna maisha x2*

*Nikiingiza mkono mfukoni, iko pesa hakuna cha kununua x2*

*Tunapika vizuri, kuweka mezani x2*

*Baada ya maombi tunasikia nduru x2*

*Uu amani , tunaomba amani*

*Tunaacha chakula kukimbilia usalama x2*

*Afrika ni kwetu, oyee! x2*

*Ndugu tupendane, oyee! x2*

**9. OMOKIMBIZI (MKIMBIZI) na Bw. Segero**

| | |
|---|---|
| *Eke nikio ekemunyereria kio omogusi* | Hii ndio ramani ya Mkisii kupigwa |
| *Nogochandwa bosabosa x2* | Kusumbuliwa bure x2 |
| | |
| *Segero baito ense ya inguririe nijisinye* | Segero nchi imehuzunika |
| *Chia enyacha kotukung'uta chire toroche* | na kando ya bahari inatumaliza |
| *Orore buya endagera egwanya erigeti* | kuwa makini, kitamu husakama |
| | |
| *Gokong'eta otaramera otaraitu choki* | wahitaji kutulia kwanza |
| *Onye obukibwa bogwaita chisembe* | kama ukabila utapiga *'chisembe'* |
| *Inki omogusi orangemwa munu* | ni kwa nini mkisii utakatwa kama |
| *enyama eng'undo x2* | nyama iliyooza x2 |
| | |
| *Chitariki 27 Disemba 2007 bwakonte* | tarehe 27 disemba 2007 tulifanya |
| *Enyangi chikabira ange chiosi Kenya* | arusi ya makabila karibu yote Kenya |
| *Chiarenge ne chia chie nyangi mpaka* | yalikuwa na nguo za arusi mpaka |
| *Omogusi bwesi* | Mkisii pia |

| | |
|---|---|
| *Omogusii tobwati monyomba* | Mkisii hana ukabila |
| *Akageni abanyanyangi obagusi* | aliwakaribisha maarusi bila kubagua |
| *Etaiyo mpaka enyangi ekaera* | hadi arusi ikafikia tamati |
| | |
| *Esanduku ya moriakari ekaib wa* | sanduku la mwanamwali likaibwa |
| *Omogusii ogaswa goshwa* | mkisii akatolewa kafara |
| *Oyosiriwa ne nibo yaye x2* | kupigwa na kupoteza mali yake x2 |
| | |
| *Tokarora amakweri na maiso* | tukashuhudia mauti kwa macho |
| *Tukumenya chisana ime*tu | katafuta hifadhi misituni |
| *Ensara ekaamba kongitera abana x2* | nusura tufe njaa pamoja na watoto x2 |
| | |
| *Omogusii ere nigoakaegure chisegi* | mkisii alikuwa akisikia kuwa vita |
| *ne chimbeaendu chibwate ubwaribu* | ni vibaya na husababisha uharibifu |
| *abasacha nigo bare goitwa babutorwa* | wanaume walipigwa na kukatwa |
| *emetwe chinyomba bagosambwa* | vichwa na nyumba zao kuteketezwa |
| *naboigo ne chigari x2* | pamoja na magari yao x2 |
| | |
| *amabati batogora netugo yosi baira* | mabati yaling'olewa na mali kuporwa |
| *abamama na abakungu bwanyumwa koreche* | kina mama na wake zao walibakwa |
| *Sagero tiga ikuane na umunuone* | Segero wacha nitamke kwa kinywa |

**10. OMOREMBE TOYO (AMANI HAKUNA) na Bw. Segero**

| | |
|---|---|
| *Obe omorembe x2Gaki toiyo x2* | amani x2 ukweli hakuna x2 |
| *Gaki tata twugosabire olete omorembe* | baba twakuomba utupe amani |

| | |
|---|---|
| *Tata twugosabire olete omorembe* | baba twakuomba utupe amani |
| *Orambole okoboko kwago gaki* | nyosha mkono wako kwa maadui |

| | |
|---|---|
| *Nindigereria Sugusu morembe toiyo* | nikiangalia Sugusu amani hakuna |
| *Iriangi na Bosonko morembe taiyo x2* | Iriangi na Bosonko amani hakuna x2 |
| *Nonye esemo ya Mocha morembe taiyo* | hata sehemu ya Mocha amani hakuna |
| *Nitarera iche Abasigisi ni chisara* | nikitembelea Wakipsigis ni mishale |
| *Baimogetie x2* | wameibeba x2 |
| *Gikobararia Abasigisi butebia na* | nikiwauliza Wakipsigis wananiambie |
| *Abagusii bakorwani* | wanasema ni Wakisii wanawapiga |
| *Gikobararia Abagusii butebia na*ni | kiwauliza Wakisii wananiambie |
| *Abasigisi bakorwani* | wanasema Wakipsigis wanawapiga |

| | |
|---|---|
| *Itarera Abamanyi na amatimo baigetie* | nikitembelea Wamasai mikuki wabeba |
| *Ikobubori Abamanyi niki na Abasigisi* | nikiwauliza Wamasai ni nini, ni Wakipsigis |
| *Togoita* | tunawapiga |
| *Tata nukoreire olete omorembe* | baba nakulilia utupe amani |
| *Orumbore okoboko kwayo gaki* | unyoooshe mkono wako |
| *Ebisaku obe gaki* | kwa ukabila |

| | |
|---|---|
| *Nindegereria ense ya Kenya* | nikiangalia nchi ya Kenya |
| *Morembe toiyo* | hakuna amani |
| *Chinyomba chiasamburu* | nyumba zimeteketezwa |
| *Abanto ni chiema bamenyete* | watu wanaishi ndani ya hema |
| *Nonye chinyomba tomenyete* | tunaishi ndani ya hema |

| | |
|---|---|
| *Tata nagosubire olete omorembex2* | Baba nakulilia ulete amanix2 |
| | |
| *Abaruhi batemire koronde basinyiru* | viongozi wamejaribu lakini wameshindwa |
| *Abaruhi batemire omorembe* | viongozi wamejaribu amani |
| *Koffi Annan korete omorembe toiyo x2* | Koffi Anan hajafanikiwa kuleta amani x2 |

**11. KALYET (AMANI) na Makiche Boys Band**

| | |
|---|---|
| *Kararan kalyet oo iman en emenyon x2* | amani ni nzuri kwetux2 |
| *Imanit ko longetab chi ago ribindenyon x2* | haki ni ngao na ulinzi wetu x2 |
| *Ogere en emenyon o kin komami kalyet x2* | tazama kwetu wakati wa ghasia x2 |
| *Kibetyo che kiame iman o ak kouit sobet x2* | chakula kilikosekana hali tata x2 |
| | |
| *Kararan kalyet o o iman en emenyon x2* | amani ni nzuri kwetu x2 |
| *An iyai chito che miach oo koberur iman x2* | ukitenda mema utabarikiwa x2 |
| *Melektangung' ko mawalaksei inyoru che miach* | mapatoyo yatakuwa mema x2 |
| | |
| *Kararan kalyet o o iman en emenyon x2* | amani ni nzuri kwetu x2 |
| | |
| *Imanitab chi komabete kipkoi x2* | haki ya mtu kamwe haipotei x2 |
| *Olon magerin kimugulmet kogerin Mungu x2* | Mungu ndiye atakutambua x2 |
| | |
| *Kararan kalyet o o iman en emenyon x2* | amani ni nzuri kwetu x2 |
| | |
| *Ongimutyoon che kait o en emenyon x2* | tuitulize migogoro kwetu x2 |

| | |
|---|---|
| *Magiyokto mugetut iman, ko kagichilil x2* | tusilipize kisasi, ni kosa x2 |

**12. LAZARO na Joel Kimetto**

| | |
|---|---|
| *Kimi chi ne kibo Betania* | kulikuwa mtu huko Betania |
| *Kigiguren kainenyin Lazaro* | jina lake Lazaro |
| *Kitun komian ine miando ne woo* | kuna siku aliugua ugonjwa mbaya |
| *Ago kimyan Lazaro kot kome* | Lazaro aliugua hadi akaaga dunia |
| *Kibwa biik che chang koriryo* | watu wengi walikuja kuomboleza |
| *Kinai Marta kole nyonei Jesu* | Marta alijua kwamba Yesu yuaja |
| *Kolabat kotorokta ak kolenji* | akaenda kumlaki na kumwambia |
| *Ndo kiimi we Jesu ko kimatamee* | ungekuwa Yesu, hangeaga dunia |
| *Ko ta kimamee Lazaro* | Lazaro hangeaga dunia |
| | |
| *Anogeer ogot en gorik che kimenye* | tukitazama hata katika nyumba zetu |
| *Mamite boiboiyet* | hamna amani |
| *Amun miten toiyet ak suriet* | kwa sababu kuna ugomvi na chuki |
| *Yon mami Jesu komi mami kalyet* | Yesu asipokuwa hamna amani |
| | |
| *Ndo kiimi we Jesu* | kama Yesu ungekuwa |
| *Ko ta kimakomee Lazaro* | Lazaro hangeaga dunia |
| | |
| *Nda mite Jesu kaniset* | Yesu akiwa katika kanisa |
| *Ko mamaitos ng'echerook kandoik* | viongozi hawatazozania nyadhifa |
| *Ndo miten Jesu kwenunyon* | Yesu akiwa miongoni mwetu |

| | |
|---|---|
| *Ko too kitebye en chamnyet* | tungekaa kwa upendo |
| | |
| *Ndo kiimi we Jesu* | kama Yesu ungekuwa |
| *Ko ta kimakomee Lazaro* | Lazaro hangeaga dunia |
| | |
| *Ongegeer en emenyon bo Kenya* | tazama katika nchi yetu Kenya |
| *Ye kimiten bororiosek che chang* | tukiwa makabila mengi |
| *Ndo mi Jesu kwenunyon* | Kama Yesu atakuwa miongoni mwetu |
| *Ko ta mamiten bororiondit* | hatungekuwa na ukabila |
| | |
| *Ndo kiimi we Jesu* | kama Yesu ungekuwa |
| *Ko ta kimakomee Lazaro* | Lazaro hangeaga dunia |
| | |
| *Ongegeer emenyon bo Kenya* | tazama nchi yetu ya Kenya |
| *Ole mi bororiosiek che chang* | kuna makabila mengi |
| *Ndo menye Jesu kwenunyon* | kama Yesu angeishi miongoni mwetu |
| *Ko to mamiten ukabila* | ukabila haungekuwa kwetu |
| | |
| *Ndo kiimi we Jesu* | kama Yesu ungekuwa |
| *Ko ta kimakomee Lazaro* | Lazaro hangeaga dunia |
| | |
| *Ndo kimi Jesu Kenya inyon* | kama Yesu angekuwa Kenya yetu |
| *Ta kima kitumdo korotik* | damu haingemwagika |
| *Nda kimi Jesu kwenunyon* | Yesu angekuwa miongoni mwetu |

| | |
|---|---|
| *Ko ta kimenye en kalyet* | tungekuwa tunaishi kwa amani |
| | |
| *Ndo kiimi we Jesu* | kama Yesu ungekuwa |
| *Ko ta kimakomee Lazaro* | Lazaro hangeaga dunia |
| | |
| *Ongetaach Jesu we tupchosiek* | tumpokee Yesu ndugu zangu |
| *Ak ongeguur konyo kwenunyon* | na tumkaribishe kati yetu |
| *Ak ongesigun nebo iman* | na tuokoke ya hakika |
| *Asi ketebii en kalyet* | ili tukae kwa amani |
| | |
| *Ndo kiimi we Jesu* | kama Yesu ungekuwa |
| *Ko ta kimakomee Lazaro* | Lazaro hangeaga dunia |
| | |
| *Kiing'et Jesu Lazaro* | Yesu alimfufua Lazaro |
| *Komong'une che kigobek* | akatoka kwa wafu |
| *Ano kegur konyo emenyon* | tumkaribishe Yesu kwetu |
| *Asi kemeng'isien en kalyet* | ili tuishi kwa amani. |

**13. MAPATANO na Onyi Papa J**

*Ooh Kenya*

*Kenya nchi yetu*

*Tuko kitu kimoja nchini Kenya*

*Hapo awali tulikuwa na vita x2*

*Hapo awali watu walipigana*

*Hivi sasa tuko kitu kimoja x2*

*Ooh Waluiya*

*Tuwache vita*

*Wananchi tuwe kitu kimoja x2*

*Tuwache vita tuko kitu kimoja x2*

*Koffi Annan alileta coalition*

*Koffi Annan alileta mediation x2*

*Graca Machel hongera mama*

*Condolisa Rice hongera mama*

*Rais Kikwete hongera baba*

*Ni kwenye mapatano oo x2*

*Kati ya wawili*

*Kwenye mapatano kati ya wawili*

*Rais Kibaki hogera baba x2*

*Ndugu Amolo hongera baba*

*Baada ya mapatano tulienda bungeni x2*

*Wabunge wote waliapishwa usiku x2*

*Anyang Nyong'o aliapishwa usiku*

*Martha Karua aliapishwa usiku*

*Wetangula aliapishwa usiku*

*Omingo Magara aliapishwa usiku*

*Amolo Odinga aliapishwa usiku*

*Okemo aliapishwa usiku*

*Fred Gumo aliapishwa usiku*

*Otieno Kajwang aliapishwa usiku*

*Wabunge wote waliapishwa usiku*

*Ooh hivi sasa kazi ianze x2*

*Coalition government naifurahia sana x2*

*Ni kwa nini naifurahia sana*

*Coalition government hakuna wizi*

*Coalition government hamuna wizi*

*Ukijaribu kuiba itabidi ukae pembeni*

*Ukijaribu kuiba itabidi ukae kando*

*Utaacha kazi na wengine wataendelea*

*Kenya tuwache vita*

*Wanakenya tuwache vita*

*Makabila yote tuwache vita*

*Naomba Wakikuyu weka panga chini*

*Wajadhe weka mawe chini*

*Wanandi weka mshale chini*

*Waluya weka panga chini*

*Hata Wakisii weka mkuki chini*

*Tuko kitu kimoja tuwache vita*

*Koffi Annan alileta mediation*

*Coalition government ina maendeleo tele*

*William Ruto sambaza mbegu*

*Otieno Kajwang sambaza passport*

*Mama Ngilu sambaza maji*

*Orengo sambaza ardhi*

*Balala watalii warudi Kenya*

*Ongeri*

*sambaza elimu*

**14. KARARAN KALYET na Makiche Boys Band**

| | |
|---|---|
| *Kararan kalyet oo iman en emenyon* | amani kitu kizuri katika nchi yetu x2 |
| *Imanit ko long'et ak ribindenyon* | haki ni ngao na ulinzi wetu x2 |
| | |
| *Ogere en emenyon kin ko mami kalyet* | mliona kwetu wakati wa vita x2 |
| *Kibetyo che kiame iman kouit banda* | chakula kilikosekana, hali ngumu x2 |
| | |
| *Kararan kalyet oo iman en emenyon* | amani kitu kizuri katika nchi yetu x2 |
| *Imanit ko long'et ak ribindenyon* | haki ni ngao na ulinzi wetu x2 |
| | |
| *An iyai chi che miach ko berur iman* | ukitenda mema kweli ni baraka x2 |
| *Melektang'ung' ko mawalaksei* | malipo yako hayabadiliki |
| *Inyoru che miach x2* | mazuri yatakuandama x2 |
| | |
| *Kararan kalyet oo iman en emenyon* | amani kitu kizuri katika nchi yetu x2 |
| *Imanit ko long'et ak ribindenyon* | haki ni ngao na ulinzi wetu x2 |

| | |
|---|---|
| *Imanitab chi ko mabete kipkoi* | haki ya mtu haitapotea kamwe x2 |
| *Olon magerin chi kogeerin Mungu* | mja akikupuuza, Mungu atakurehemu x2 |
| | |
| *Ongimutyon che kait en emenyon* | tuvumiliane kwa shida zitukumbazo x2 |
| *Magiyokto muget ko kechilil* | usilipize kisasi utakuwa umekosa x2 |
| | |
| *Kararan kalyet oo iman en emenyon* | amani kitu kizuri katika nchi yetu x2 |
| *Imanit ko long'et ak ribindenyon* | haki ni ngao na ulinzi wetu x2 |

**15. UKABILA na Silas Omondi**

*Ee Mungu wangu ninakupenda mimi*
*Umeniponya umenilinda Baba*
*Umetuponya umetulinda Kenya*
*Umebariki taifa letu Kenya*
*Taifa zuri taifa lenye upendo*

*Umetuponya umetulinda Kenya*
*Ona Wakenya mlipigana nyinyi*
*Mwaka 2007 mlipigana*
*Mwaka 2008 mlipigana*
*Hamkujali ndugu zenu nyinyi*
*Watoto wetu walibaki mayatima*
*Kwa sababu ya ukabila Kenya*

*Ukabila tuwache ukabila*
*Wakikuyu tuweke panga chini*
*Wajaluo tuweke mawe chini*

*Wakale tuweke mishale chini*

*Rais uhuru tupendane*
*William Ruto tupendane*
*Raila Odinga tupendane*
*Kalonzo Musyoka tupendane*
*Wetangula sote tupendane*

*Wapokot muwache bunduki*
*Waturkana muwache bunduki*
*Ukabila ni mbaya*
*Ukabila huleta vita*
*Ukabila huleta chuki*
*Ukabila adui mkubwa*
*Ukabila tuwache ukabila*

**16. NG'ATO BER MAPARO CHIEN na Atoby**

| | |
|---|---|
| *Wuod Onyango agona thum omin Ken wer nang'o* | mwana wa Onyango, ndugu ya Ken |
| *To en ang'o, gima nyocha aneno* | niruhusu niimbe kwa uwezo wangu |
| *Ak agomb neno kendo Tobby jagomba x2* | niwaeleze yale niliyoyapitia x2 |
| | |
| *I ga alofu ariyo gi abiriyo anena ang'o jawaya* | mwaka 2007 ulikuwa wakati mgumu |
| *Masira to en ang'o en ang;o wuod Ugenya* | mie Tobby kutoka kwetu Ugenya |
| *Tobby we apariye x2* | siamini kilichonisibu x2 |
| | |
| *Bang lang'o ombulu jawaya wabet piny* | tulipiga kura kwa uchangamvu |
| *Warito kwaka jangoma x2* | tulipotoka wapi jamani x2 |
| *Ne warito nyaka saa auchiel otieno* | tulishinda tukisubiri matokeo |
| *Ji penjere ni en arijo mikwaro no kwamare* | watu wamekosa subira sana |
| | |
| *Dwoko anogo jawaya Omin Ken we awachanue* | wapiga kura sasa wamekasirika |
| *Opanga oting jawaya marungu oting acham kenye* | wamejihami marungu nani atatusaidia |
| *to en ang'o wuod Ugenya Tobby yoo* | tukae tukitarajia mema rafiki yangu |

| | |
|---|---|
| *gini ng'wana Kibira ka en gi Morris osiepa* | Morris wa Kibira |

**17. HAKI YETU na Queen Babito**

| | |
|---|---|
| *Abiro nyar Gilana awuoro, piny otimo much* | siyaamini ninayoyaona yakitujia |
| *tindo achom kenye karingo ogwang' okwalo* | waovu wametuibia kura zetu tena |
| *kura, uwi marang'ongo piny yuak,* | wananchi wanalalamikia tukio hili |
| *Kivuitu olando duoko, abaoutan oganda kedo* | hawataki matokeo ghushi ya Kivuitu |
| *kendgi, jii oremo ni haki marwa emadwaro,* | tunadai haki yetu katika uchaguzi |
| *haki yetu tarik pier adek, disemba 2007* | tarehe thelathini disemba 2007 |

| | |
|---|---|
| *Agwambo ochopo piyo kod William Ruto gi* | Raila, William Ruto, Nyong'o, Nyagah |
| *Nyong'o, Nyaga gi Ngilu, Balala Kosgei gi* | Balala, Ngilu, Kosgei, Ndolo, Mudavadi |
| *Ndolo, Mudavadi ochopo, Bishop Margaret* | Bishop Margaret na Orengo pamoja |
| *oketo lemo, Orengo iye awang' Kivuitu kwalo* | walimkabili Kivuitu kule KICC |
| *tochungo, can you hear me Mr. chairman, No!* | Orengo alitaka asikizwe na mwenyekiti |
| *No! No! Please Mr. Chairman let me talk* | kwa sauti ya la! La! La! Akasema kuwa |
| *Iraq koparo Sudan, kanokelo ofujo node* | Iraq, Sudan, Somalia , Rwanda, Liberia |
| *Ethiopia gi Somalia kata Rwanda kupara* | nchi nyingizimekumbwa na vita vikali |
| *Sudan owinjo gino, Liberia ringo godhiambo* | kwa sababu za kisiasa. |

| | |
|---|---|
| *Piny goo nduruu piny yuakni, piny goo nduru* | tusiruhusu nchi ichukue mwelekeo huu |
| *Joka bimbe okwalo kura tho rumo wan jo onagi* | tusikubali madikteta kutunyanyasa |
| *Wan joma beya ndii wan gimudwaro towathimo* | Wajaluo wawaunga wengine ila |
| *Kochopo marwa to odagi, wan joka anagi kura* | hawajawahi kuonyesha fadhili zao |
| *Newagoyo gi sironyo, Rift Valley, Coast ji oremo* | maeneo mengi nchini yametatizika |
| *Ni Amollo telo to udagi, joka waru beto oganda* | mbona Raila asipatiwe haki yake |
| *Mwandu wang rumo, dhamo thoo rumo, ibed* | mungiki wauwa wananchi, kila mahali |
| *Mama kata motto, ng'wech ringare piny goo nduru* | kunateketea, woporaji kila mahali |

| | |
|---|---|
| *Baba koso diponi wan niketowa e piny kae mondo* | wapi imeandikwa kwamba Wajaluo |
| *wabed ngas majowetewa idho kidhi pon godo olemo* | hawawezi kuiongoza nchi nyetu? |
| *koso lajni ne ok en pokwa mondo waluera godo* | nani kasema mahali pao ni upinzani |
| *koso bed ni nisingo nilojni wabiro kawe gi remo* | lazima damu imwagike ili mjaluo |
| *Baba koso obiro bedo sand mane J.M Kariuki obede* | aongoze? J.M Kariuki, Robert Ouko |
| *Robert Ouko obede, Tom Mboya obede, Odhiambo* | Tom Mboya, Odhiambo Mbayi, na |
| *Mbayi en kanyo? Argwings Kodhek nobede. Anyiso* | Argwings Kodhek wote walijitoa |
| *wuod Oganda niya. Baba uchalo kaka Musa, nimer* | mhanga ili waikomboe jamii yao. |
| *nachwado nam; manyi thii Israel okedho bahati* | Raila kama Musa ni kiongozi pekee |
| *mbaya notho makoremo piny mar Kanaan* | anayeweza kutufisha Kanaan |

**19. OMOREMBE na Rebecca Thomas**

| | |
|---|---|
| *Omorembe omorembe omorembe omorembe* | amani amani amani amani |
| *Ng'ai moroche omorembe omuya ogotoka x3* | waona wapi kimbilio cha amani |
| *Intebei omorembe omuya ng'ai ogotoka* | niambie wapi kimbilio cha amani |
| *Inkonyo omoremmbe omuya ng'ai ogotoka* | nisaidie nifikie kimbilio cha amani |
| *Saidia omorembe omuya ng'ai ogotoka* | nisaidie kwa kimbilio cha amani |
| *Basani bane omorembe omuya ng'ai ogotoka* | wenzangu nipate wapi kimbilio cha amani? |